

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Tano – Tarehe 11 Aprili, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae, Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali letu la kwanza leo Ofisi ya Rais, TAMISEMI litaulizwa na Mheshimiwa Lameck Okambo Airo.

Na. 35

**Hitaji la Jengo la Upasuaji Kata ya Koryo - Rorya**

**MHE. KISWAGA B. DESTERY (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO)** aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Koryo kwa kushirikiana na Mbunge wao na wananchi wa Rorya wanaoishi Mwanza, Arusha na Dar es Salaam wamejenga wodi ya akina mama na watoto pamoja na kununua jokofu lakini mapungufu yaliyopo sasa ni Jengo la upasuaji.

Je, Serikali sasa haioni ipo haja ya kusaidia jengo hilo pamoja na vifaa vyake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 mradi uliidhinishiwa shilingi milioni 30 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la upasuaji. Fedha zote zimepokelewa na tayari Halmashauri imeanza taratibu za kumpata mkandarasi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imepanga kutumia shilingi milioni 25 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo hilo.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, je, Serikali ina mpango gani wa kuzielekeza Halmashauri kutumia *force account* ili miradi midogo midogo kama hii iweze kutengenezwa kwa fedha ndogo na iweze kuleta *impact*?

Swali la pili, kwa kuwa jambo hili linafanana kabisa na vituo vya afya vilivyoko Jimbo la Magu katika kituo cha afya Lugeye pamoja na Nyanguge. Serikali ina mpango gani wa kuvijengea majengo ya upasuaji ili wananchi waweze kupata huduma karibu? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali hivi sasa si kutoa maelekezo, tayari tumeshatoa maelekezo hivi sasa na Halmashauri mbalimbali zinaendelea

kutumia *force account* na tumepeata mafanikio makubwa sana, kwa sababu maeneo mbalimbali unapopita hivi sasa mradi ambao zamani ulikuwa saa nyingine ulikuwa unagharimu shilingi milioni 150 utakuta sasa hivi milioni 70 mradi umekamilika tena upo katika ubora unaokusudiwa.

Kwahiyo Mheshimiwa Kiswaga ni kwamba sasa hivi jambo hilo linaendelea na linaendelea kwa ufanisi mkubwa, na nipende kuwashukuru sana Wenyeviti wa Halmashauri na Wakurugenzi ambao wanasmamia jambo hili kwa uzuri zaidi na hasa Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, katika suala zima la Jimbo la Magu ambalo Mheshimiwa Mbunge umesema na ni kweli, katika harakati za Serikali tuna mpango ambao si muda mrefu sana tutakuja kuuanza katika kituo chako kimoja cha afya tutakuja kujenga Jengo la upasauji na kuweka vifaa tiba vyote. Kwa hiyo, naomba nikushauri Mheshimiwa Mbunge kwamba usiwe na wasiwasi Serikali yako kama kila siku inavyopiga kelele hapa Bungeni itaendelea kushirikiana nanyi na ujenzi huo Mungu akijaalia utaanza hata kabla ya mwezi wa sita.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Paresto.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Katika Mkoa wa Arusha kuna majimbo saba na katika majimbo hayo majimbo mawili yana jiografia ngumu sana ikiwemo Jimbo la Longido na Jimbo la Ngorongoro. Je, Serikali iko tayari sasa katika bajeti tunayoiendea kutazama majimbo haya kwa mujibu wa jiografia yao ili wananchi wanaoishi katika maeneo hayo waweze kupata huduma za afya kwa urahisi na kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba

Serikali inapeleka nguvu kubwa sana katika eneo hilo, na ndio maana juzi juzi nilikuwa katika Wilaya hizo zote mbili; Wilaya ya Longido pamoja na Wilaya ya Ngorongoro, katika Wilaya ya Ngorongoro siyo muda mrefu sana Mungu akijaalia katika kipindi hiki cha katikati tutakwenda kuwekeza nguvu kubwa sana kwa kupeleka takribani milioni 700. Lengo kubwa ni kwamba maeneo yale yana jiografia tata sana wananchi waweze kupata huduma kujua kwamba Serikali yao ipo vitani katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma hiyo inayokusudiwa.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna wilaya nyingi mpya ambazo zina matatizo sana ya hata kutokuwa na Hospitali za Wilaya. Na kwa kuwa majibu yake anasema kwamba kuna fedha ambazo zimetengwa, je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kunihakikisha kwamba katika Wilaya ya Busega kituo cha Nasa hizo fedha zitapatikana lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Dkt. Chegeni unafahamu na wewe kule kwako umenikaribisha, nakushukuru sana. Hicho kituo cha afya ulichokisema mionganoni mwa maeneo ambayo yana changamoto, na akina mama wanapata shida kubwa sana kupata huduma za upasuaji. Nilikueleza wazi kwamba katika kipindi cha huu mwaka tutafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba tunajenga jengo la upasuaji kama nilivyosema katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuwa na imani, kwamba Serikali kwa kuititia Wizara ya afya tuna mkakati mpana sana kuhakikisha kwamba tunapelekea huduma katika maeneo hayo na Mungu akijaalia kabla ya mwezi wa sita tunaweza tukaenda kuweka jiwe la msingi sawa sawa na kituo cha afya cha Malya kule kwa ndugu yangu Ndassa. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kiwelu.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika hospitali yetu ya Wilaya ya Siha hatuna hatuna jokofu na imekuwa inaleta usumbufu sana kwenye kuhifadhi miili ya marehemu wetu.

Je, ni lini Serikali itatuletea jokofu kupunguza upungufu huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Hospitali ya Siha takribani wiki sita zilizopita nilikuwa pale Siha na namshukuru sana Mbunge tulikuwepo pamoja na tulitembelea hospitali ile na kipindi kilichopita hapa nilitoa maelekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyofika pale Siha, kutokana na changamoto tuliyobaini pale, kwamba tumepeleka fedha lakini matumizi yale ya fedha tumeona hayaelekezwi sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kabla ya jokofu kuanza kuna suala zima la fedha tulizozi peleka pale lazima zitumike vizuri na tumeshatoa maelekezo hayo. Lengo letu ni kwamba lile jengo, *floorya juu* iweze kukamilika vizuri lakini hatuachi hapo kwa sababu changamoto kubwa ya pale lazima tuhakikisha hospitali ile inafanya kazi vizuri na Serikali itaweka nguvu za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishapeleka zaidi ya milioni 250, inafanya kazi lakini suala la jokofu litakuwa ni kipaumbele chetu ili kuhakikisha, lengo kubwa hospitali ile inafanya vizuri kwa wananchi wa Siha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Anatropia.

Na. 36

### **Kyerwa Kuwa Makao Makuu ya Wilaya**

**MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliluiza:-

Mkao Makuu ya Wilaya ya Kyerwa yamewekwa katika Kata ya Kyerwa.

Je, ni mchakato gani ulifanyika mpaka Kata ya Kyerwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili eneo liwe na makao makuu ya Wilaya lazima wananchi washirikishwe kuitia mikutano mikuu ya Vijiji na Halmashauri za Vijiji, Kamati za Maendeleo za Kata, Mabaraza ya Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuza wa kuifanya Kata ya Kyerwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya ya Kyerwa ultolewa baada ya kuitishwa na Baraza la Madiwani katika kikao cha tarehe 30 hadi 31 Oktoba, 2012 na Kamati ya Ushauri ya Mkoza wa Kagera katika kikao chake cha tarehe 15 Machi, 2013 hivyo uamuza wa mwisho kuhusu eneo la Rubwera katika Kata ya Kyerwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya Kyerwa ulizingatia mapendekezo ya vikao hivyo vya kisheria.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa michakato hii inachukua muda mrefu sana ambayo inaanzia kwenye ngazi za vijiji mpaka juu kama Naibu Waziri alivyosema.

Je, endapo michakato hii katika ngazi za chini itakamilika mapema, nini kauli ya Serikali Kuu ili na wao waharakishe na wananchi hawa wapate haki zao?

Swali la pili, kwa kuwa tunapokaribia wakati wa Uchaguzi Mkuu, Serikali imekuwa na hali ya kugawa kata zetu na vijiji ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma kwa karibu. Naomba nifahamu Serikali ina mpango gani kuanza mchakato huo mapema kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kuondoa usumbufu na maandalizi pia ya muhimu kwa wananchi hawa ambao maeneo yao ni makubwa na Kata zao ni kubwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza katia sehemu ya kwanza ni kwamba mchakato umekamilika na Makao Makuu ya Halmashauri imeshathibitishwa ndio ile ambayo imetajwa pale isipokuwa Mheshimiwa Mbunge alikuwa na utata katika hayo Makao Makuu mapya, kwa hiyo mchakato huo ulishakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la kugawa wakati wa kuelekea kwenye uchaguzi nadhani hii sasa ni mamlaka zetu katika *Ward Council* zetu, vikao vyetu vile vya kisheria kama nilivyovisema, ambapo inaonesha baadaye jambo hili litaenda katika Tume ya Uchaguzi kupita Ofisi ya Waziri Mkuu.

Kwa hiyo, hakuna shaka naamini kwamba kila mtu katika maeneo yake anabaini changamoto zinazokabili eneo hilo na tutafaya maandalizi ya awali ilimradi kupusha ukakasi kwamba maeneo yanagawiwa muda mfupi kabla ya uchaguzi.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwa kuwa Wilaya ya Ngorongoro ni kubwa kuliko Mkoa wa Kilimanjaro, hali inayopelekea jiografia ya Wilaya hiyo kuwa ngumu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kugawa Wilaya hii ya Ngorongoro au kuweka Halmashauri mbili ili kuwasogezea wananchi wa Ngorongoro huduma kwa karibu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na Mheshimiwa Mbunge pale wa Jimbo hio la Ngorongoro ambalo Naibu Waziri wa Kilimo na ye ye alinialika niweze kufika kule jimboni kwake juzi juzi hapa nilikuwepo kule. Kwa umbali kweli jiografia ya Ngorongoro ina changamoto kubwa sana kwa sababu ukianzia hapa getini ukitoka hapa Karatu mpaka unafika Makao Makuu kule Loliondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nillipata fursa ya kutembelea mpaka Ziwa Natron kwenda shule ya sekondari ya Ziwa Natron. Jiografia ya Ngorongoro kweli ni kubwa zaidi, lakini mara nyingi sana maeneo haya yanagawanywa kutokana na *population*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia eneo kubwa la Ngorongoro ni hifadhi, lakini kama kutakuwa na haja ya kuweza kugawanya basi kwa mchako ule ule wa kisheria wananchi wa aeneo hilo watafanya hivyo na Serikali itaangalia kama kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini inawezekana tunaweza tukaangalia mbali kwa sababu Ngorongoro na Serengeti ukiangalia jiografia yao ina changamoto kubwa sana. Hili sasa tuwaachie wenye maeneo hayo mkaweza kufanya maamuzi sahihi kama ulivyo Mheshimiwa Catherine Magige unavyokuwa na wazo hilo, basi na Serikali itaangalia nini cha kufanya kwa maamuzi sahihi kwa maslahi mapana kwa wananchi wa Ngorongoro.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu.

Na. 37

### **Kupandisha Hadhi Kituo cha Afya cha Karatu**

**MHE. QAMBALO W. QULWI** aliluliza:-

Wilaya ya karatu ina umri wa zaidi ya mika 20 lakini bado haina Hospitali ya Wilaya jambo ambalo linawatesa wakazi wengi hasa wazee, akinamama na watoto.

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Kituo cha Afya cha Karatu kuwa Hospitali ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qambalo Qulwi, Mbunge wa Karatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya kupandisha hadhi kituo cha afya kuwa hospitali yanaanza katika Halmashauri yenyewe kupitia Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Mkoa. Taratibu hizi zikikamilika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatoa kibali baada ya kujiridhisha kupitia timu ya ukaguzi hivyo Halmashauri unashauriwa kuanzisha mchakato wa kujadili suala hilo katika vikao vya kisheria na kuwasilisha katika mamlaka husika kwa maamuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Qambalo.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi tena naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la kupandishwa hadhi kituo hiki limekwisha kujadilikanwa katika mamlaka zilizopo pale wilayani na hata mkoani, kwa hiyo kama ni suala la

mamlaka iliyobaki kushughulikia jambo hili ni mamlaka iliyoko juu ya hizo mbili. Je, ni lini sasa timu hiyo ya ukaguzi itatumwa ili upandishwaji hadhi wa kituo hiki uweze kukamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa safari ya kuelekea kupata Hospitali ya Wilaya ya Karatu imeanza, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kutenga fedha katika bajeti ya kuanzia mwaka huu na kuendelea ili miundombinu michache iliyobakia iweze kukamilika? Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *nill-cross check* mpaka jana kuangalia taarifa hizi *status zikoje*, lakini kwa taarifa nillizopata kule inaonekana mchakato ulikuwa haujakamilika vizuri. Kwa hiyo, naomba tushauriane tu, tutaangalia jinsi gani tutafanya ili wenzetu wa Halmashauri ili kama lile jambo limekwama halijafika katika mamlaka husika, hasa katika Wizara ya Afya waweweze kufanya hivyo ili Waziri wa Afya aweze kufanya maamuzi, nadhani jambo hilo litakuwa halina shida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wizara kuweza kutenga fedha, ni kweli, na unakumbuka nilikuja pale jimboni kwako na nilitoa maelekezo kadhaa ambapo nilikua sijaridhika na kufika pale nilikuta watu wamefunikwa *ma-blanket* ambayo yametolewa *store* baada ya kusikia Naibu Waziri anakuja pale; kwa hiyo nimegundua changamoto mbalimbali pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchakato wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya tutaendelea kufanya hivyo. Naomba niwasihii hasa ndugu zetu wa Halmashauri, anzeni mpango huo sasa kuanzia bajeti zenu za Halmashauri ikifika kwetu sisi Wizarani jambo letu kubwa liwe ni *ku-compile* vizuri na kufanya taratibu vizuri ili mchakato wa ujenzi wa hospitali ufanyike. Hoja yako ni hoja ya msingi na bahati nzuri eneo lile ni eneo la kitalii lazima tuwekeze vya kutosha tuwe na

hospitali yenyé maana pale hata mgeni akija aweze kupata huduma nzuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Chatanda, Mwamoto na Mbatia

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kunipa nafasi ili na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti tatizo la Karatu linafanana na tatizo la Korogwe MJINI. Korogwe MJINI haina hospitali, kwa maana ya Halmashauri ya MJI, na Wilaya yetu tumeamua kwa makusudi kabisa kujenga kwanza kituo cha afya ambacho tutakifanya kiwe hospitali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kutusaidia kutupiga jeki kwa sababu tunajenga kituo cha afya chenye ghorofa tatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niweke kumbukumbu sawa ni kwamba nipende kumshukuru Mama Mary Chatanda, Profesa Maji Marefu pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Korogwe kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ambapo nimetembelea mara kadhaa katika eneo lile. Nilivyofika pale nimekuta *initiative* mbalimbali wanazozifanya hasa katika suala zima la sekta ya elimu na sekta aya afya na bahati nzuri wanatumia hospitali ya ndugu yangu Profesa Maji Marefu, iko vijijini lakini *obvious* kijiografia iko mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa sababu mmeanza harakati za ujenzi, na kile kituo cha afya ni kituo cha afya makini inaonekana kuna viongozi makini eneo lile, Serikali itachukua wazo lile jema kuangalia wapi mmeishia, tukishirikiana nanyi kwa pamoja tufanyeje, kwa kuangalia resource tulizo nazo tusukume ili eneo la pale ambalo ni

katikati; watu wanaotoka Arusha hata ikipatikana ajali lazima watakimbiza pale, tuweze le tuweze kushirikiana kwa pamoja tujenge Hospitali ya Wilaya pale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nianze kwanza kwa kuishukuru Serikali kwa kusikiliza kilio cha watu wa Kilolo kwa ujenzi wa hospitali. Pamoja na hiyo, Mheshimiwa Waziri, itachukua muda mrefu hiyo hospitali kuweza kuisha. Lakini tatizo ambalo lipo ni kwamba Wagonjwa inabidi wapelekwe Kituo cha Afya Kidabaga ambacho hakijakamilika, hakina wodi ya watoto, wodi ya wazazi wala upasuaji, lakini inabidi sasa wasafirishwe waende kwenye hospitali ambayo iko zaidi ya kilometra 120. Tatizo hakuna gari Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hiyo utatusaidiaje ilituweze *either* kukarabatiwa vizuri kituo cha Kidabaga au tupate gari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi. Wako wengi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu tulifanya ziara pamoja na tukakuta hospitali yao ya Wilaya pale iko taabani. Tukafanya mawazo ya pamoja, na bahati nzuri ndani ya muda mfupi wakapaa shilingi bilioni 1.2. Lakini, kama hiyo haitoshi niwapongeze; kwasababu wameshafanya harakati na ujenzi unaendelea kule *site* na Mungu akitujaalia ndani ya wiki mbili hizi wakati tuko Bungeni nitakwenda kutembelea ili kuona ni jinsi gani ujenzi unaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kituo cha Afya cha Kidabaga nadhani unafahamu kwamba Serikali tutaweza kuweka nguvu kubwa pale kwasababu tukiangalia jiografia yake ni tata sana, tutaangalia namna ya kufanya. Tutapeleka fedha kwa ajili ya kujenga *theatre* ikiwezekana na wodi ya

wazazi. Lengo kubwa wananchi wa eneo lile waweze kupata huduma bora. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Mbatia. Jiandae Mheshimiwa Saumu.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Hospitali nyingi za Wilaya zina mkataba kati ya Serikali na mashirika hasa ya dini, Hospitali ya Kilema ikiwa moja wapo. Tunajenga maabara ya kisasa, nini *commitment* ya Serikali katika hospitali ya Kilema ili iweze ikatoa huduma zilizo bora katika Taifa hili?

**MWENYEKITI:** Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni seme ujenzi wa maabara ni jambo jema sana na sisi Seriali tunappreciate hiyo juhudî kubwa inayofanyika na ukiona hivyo maana yake tunasaidia juhudî za Serikali jinsi gani iweze kusaidia wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya *commitment* ya Serikali katika hilo naomba tuangalie jinsi gani tutafanya katika suala zima la mikataba hata suala zima la watendaji; kwa sababu wakati mwingine tunaweza tukawa na maabara lakini tukawa na watu ambao hawawezi kuendesha vizuri ile maabara. Kwa hiyo, *commitment* ya Serikali ni kuangalia jinsi gani tutafanya ili maaabara ikikamilika tuweze ku-deploy watu wazuri pale wa kuweza kufanya *analysis* ya maabara, wananchi wetu wakienda pale waweze kupata huduma bora hata magonjwa yao yaweze kudundulika vizuri zaidi.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nina swali moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha afya ambacho kiko katika kijiji cha Mwera, Kata ya Mwera ni kituo ambacho kwa muda mrefu sana kimepandishwa hadhi ya kuwa kituo

cha afya; lakini kituo kile hakina huduma zinazokidhi kuwa kaama kituo cha afya. Hakina gari la wagonjwa, lakini pia vipimo nya damu salama bado havipo katika hospitali ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua ni lini Serikali itakipa hadhi sahihi kituo kile ya kuwa kituo cha afya katika Wilaya ya Pangani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ni lini tu anataka kujua.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema lini kwanza naomba tuweke rekodi sawa za Mheshimiwa Mbunge kwamba kipindi kile mlinialika na Mheshimiwa Aweso tumefika pale Mwera na nikatoa maagizo kwamba kituo kile kutokana na yule mwekezaji pale Japo anawekeza aweze kujenga *theatre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru kwa sababu wodi ya wazazi imeedelea kujengwa, lakini hata hivyo Serikali kuufanya kuwe kituo cha afya lazima miundombinu ikamilike vizuri, ndiyo maana tukaona sasa hivi tujenge jengo la *theatre* pale kubwa lakini pia kujenga na wodi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana nikamuelekeza Mheshimiwa Aweso kwamba awaambie watu waiandae mapema ile *BOQ*. Tuta *deploy* pesa pale, kwa sababu watu wa pale wakikosa huduma, suala la kuvuka Mto Pangani ni changamoto kubwa sana na usiku vivbuko hakuna. Kwa ajili ya kuwaokoa Watanzania tumeamua kuweka nguvu kubwa za kutosha, fedha za kutosha kujenga jengo lile litakamilika huenda kabla ya mwezi wa saba mwaka huu ujenzi utakuwa umeshaanza. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

Na. 38

### **Kushamiri kwa Biashara ya Vyuma Chakavu**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** Aliuliza:-

Biashara ya vyuma chakavu imeshamiri sana Tanzania Bara na Visiwani na imesababisha madhara ya kuharibiwa na kuibwa kwa miundombinu yakiwemo mifuniko ya chemba na majitaka.

(a) Je, Serikali imejipangaje kupambana na wizi na uharibifu huo wa mali za Serikali na wakati walinzi wa maeneo husika wanashuhudia hayo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba hata usalama wa raia na mali zao uko mashakani?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**  
Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis kuwa biashara ya chuma chakavu imeshamiri hapa nchini na duniani kwa ujumla. Kuongezeka kwa mahitaji (*demand*) ya vyuma chakavu kulitumiwa na wahalifu kuharibu miundombinu iliyojengwa kwa vyuma kwa nia ya kupata chuma ili waiuze kama chuma chakavu. Maeneo yaliyoathirika sana ni mifumo ya kusafirisha umeme, reli, barabara kwa kutaja baadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na hujuma hizi mamlaka husika yaani *TANESCO*, *TANROADS* na *RAHCO* wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu na Jeshi la Polisi ikiwemo kutumia walinzi wa taasisi husika kulinda rasilimali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupata suluhu ya kudumu, Wizara yangu imekwishaandaa rasimu ya muswada wa sheria itakayoweka bayana taratibu na mfumo wa usimamizi na udhibiti wa biashara ya chuma chakavu katika hatua mbalimbali za uzalishaji, ukusanyaji, usambazaji, uuzaji na uyeyushaji wake kwa kuzingatia uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa manufaa ya Taifa. Aidha, muswada huo umeweka bayana adhabu itakayotolewa kwa mtu ye yote atakayebainika ku haribu miundombinu kwa sababu ya kuchukua chuma chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge na Watanzania kwa ujumla usalama wao na mali zao ziko salama. Aidha, nitumie fursa hii kuwaomba wananchi wote kutoa taarifa pindi wawaonapo mtu anayehujumu miundombinu kwa namna yoyote ile kwa lengo la kuchukua chuma chakavu au chuma. Kwa wenye viwanda na wafanyabiashara wa vyuma chakavu jiepusheni na ununuzi wa vyuma ambavyo asili yake inatia mashaka. Kama nilivyoeleza awali, tutaharakisha sheria ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia kutatua tatizo hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru Mheshimiwa Waziri alivyonyijibu vizuri na kwa ufasaha swali langu, lakini nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Waziri, je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuwepo vyombo vya awali vya kuhakiki aina au bidhaa mbalimbali ya vyuma chakavu kabla havijafika sokoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa nini usiwepo utaratibu wa kutofautisha biashara ya vyuma chakavu kabla ya ku haribu miundombinu ya Serikali ambayo sasa hivi imeenea nchi nzima kila mahali vinang'olewa? Kungekuwa na uhakiki kabla ya hivyo vyuma chakavu kuweza kufika sokoni na kuweza kuuzwa? Ahsante.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile dhana ya kutumia vyuma chakavu ambavyo kimsingi vinakuwa havitakiwi kwenda kuviyeyusha na kutengeneza chuma ni wazo zuri. Tatizo lililopo ni kwamba watu wenye tamaa, wahalifu ndiyo wanaharibu ile dhana nzuri, hawa ni wahalifu kama wahalifu wengine. Sasa chombo cha awali cha kuweza kuzuia watu hawa ni wananchi, kama inavyosema Katiba ya nchi yetu, ulinzi wan chi hii ni jukumu la wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye ile miundombini mikubwa kama ile ya *TANESCO* nilivyosema, *TANESCO* anaweka ulinzi akisaidiana na wananchi walio wema. Nina imani huo ndio mfumo mzuri wa kuweza kulinda miundombini yetu Tanzania nzima, Wizara yangu au Serikali haiwezi kutengeneza polisi wa kulinda vyuma kuanzia vile vya taasisi mpaka vyetu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutofautisha, kama ilivyo kwa wale wanaoharibu miundombini kwenda kujipatia pesa wapo hata wenye viwanda ambao wanapokea vyuma ambavyo wazi kabisa vinaonekana vimetoka kwenye miundombini ya Serikali au ya watu, hao mimi ndio nakula nao sahani moja. Ma-*inspector* wangu wanatembelea viwanda hivyo na ni vichache vinajulikana na naendelea kuwapa elimu, atakayebainika atajuta kwanini alifanya hivyo. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Sugu. Jiandae Mheshimiwa Mwakasaka, jiandae Mheshimiwa Raymond.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala la biashara ya vyuma chakavu inaonesha ni wazi kuna soko zuri la chuma nchini na nje ya nchi. Sasa kifupi tu, sijui mradi wa chuma Liganga na Mchuchuma umefikia wapi ili nchi ifaidike na soko hilo? Ahsante.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mchuchuma na Liganga; katika mpango wa Serikali wa miaka mitano wa ujenzi wa

uchumi wa viwanda, mchuma na Liganga ipo. Nilipofikia mimi; hili suala liko mezani kwangu. Nimepitia vivutio vyote vya mwekezaji alivyoweka, nimevikamilisha, vinakwenda kwenye mamlaka kusudi waweke sahihi, mwekezaji yuko tayari kuweka fidia na kuweza kuanza. Nikipata sahihi ya mamlaka tunaanza kazi.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hii biashara ya vyuma chakavu inavikumba pia viwanda vilivyobinafsishwa kwa muda mrefu sasa kikiwemo Kiwanda cha Nyuzi Tabora, na kwa kuwa kuna taarifa kwamba mashine nyingi mle ndani zimeuzwa kama chuma chakavu na kimefungwa kile kiwanda, je, Mheshimiwa Waziri, kwa sababu nimewahi kulalamika hapa Bungeni na kutoa taarifa kuhusu kufanyika kwa vyuma chakavu, ni lini tunaweza tukaenda tukakagua kile kiwanda kwa sababu sasa hivi umetoka kusema utakula nao sahani moja, tuweze kujua kama vile zile mashine hazijauzwa kama vyuma chakavu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi. Mheshimiwa Raymond jiandae baadae.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Nyuzi cha Tabora kina mwenye nacho (*owner*) kwa hiyo, mwenye mali anapoibwiwa mimi siwezi kwenda kuangalia mali yake yule, lakini taarifa nilizonazo kutoka kwa mwenye kiwanda ameniambia amepata soko la nyuzi na kiwanda hicho kitaanza kazi.

Kwa hiyo, mimi naweza kumbana yule kwa kupitia msajili wa hazina kwamba aanze kazi na ndio wajibu wangu. Sasa kama alizembea, mali ikaibiwa mle hilo nadhani ni suala la kila abiria achunge mzigo wake.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa hii. Ni takribani miaka kumi sasa toka hili

swali linaulizwa. Nakumbuka lile Bunge la Tisa niliuliza hili swalii mwaka 2007 na Bunge la Kumi aliuliza Mheshimiwa Maida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la Serikali siku zote ni kwamba muswada unaandalishiwa. Ni lini sasa muswada huo utaletwa hapa Bungeni ili uweze kuitishwa kama sheria?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mbunge najua una imani na mimi. Sasa upele umepata mkunaji, safari hii unaletwa chini ya uongozi wangu. (*Makof/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya ujenzi, Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima.

Na. 39

**Ujenzi wa Uwanja wa Ndege – Kijiji cha Manga**

**MHE. MUSSA R. SIMA** Aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa uwanja wa ndege katika eneo lilitengwa katika Kijiji cha Manga kwa msaada wa Benki ya Dunia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** Alijibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipata mkopo kutoka Benki ya Dunia ambapo sehemu ya mkopo huo imetumika kufanya upembuza yakinifu na usanifu wa kina wa viwanja 11 vya ndege vya Iringa, Njombe, Songea, Lindi, Kilwa Msoko, Tanga, Moshi, *Lake Manyara*, Musoma, kiwanja kipyaa katika Mkoa wa Simiyu na Singida kwa ajili ya ukarabati, upanuzi na ujenzi wa viwanja hivyo kwa kiwango cha lami.

Ninapenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kiwanja cha Singida unafanyika katika eneo la kiwanja cha sasa na si katika eneo jipya la Manga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafutaji wa fedha za kazi za ukarabati, upanuzi na ujenzi kutoka vyanzo mbalimbali utaanza baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambaao kwa sasaupo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kazi hii ya usanifu ikiendelea, Wizara yangu ilipata maombi ya Mkoa wa Singida ya kutaka wataalam kwenda kufanya tathmini ya awali ya eneo jipya linalopendekezwa katika eneo la Uhamaka karibu na kijiji cha Manga kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hilo la Uhamaka limependekezwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kipywa cha ndege cha Mkoa wa Singida katika mpango kabambe wa uendelezaji wa Manispaa ya Singida kwa mwaka 2015 – 2035. Tathmini ya awali iliyofanywa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege mnamo Februari, 2016 kuhusu eneo hilo lenye ukubwa wa hekta 2400 (kilometra sita kwa kilometra nne) imeonesha kuwa eneo pendekezwa linafaa kwa ujenzi wa kiwanja cha ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia matokeo ya tathmini, hatua zitakazofuata ni utwaaji rasmi wa eneo hilo unaohusisha ulipaji fidia ya mali za wananchi waliomo ndani upimaji wa eneo kwa ajili ya hatimiliki, usanifu wa miundombinu ya kiwanja, utafutaji wa fedha za ujenzi wa kiwanja na hatimaye ujenzi wenyewe.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa Singida Mjini ni mji ambaao unakua kwa kasi sana kwa sababu Serikali imehamia Dodoma, Serikali haioni haja sasa ya kutenga fedha kwenye bajeti ya mwaka huu ili uweze

kuwalipa fidia wananchi wa kwenye hilo eneo la Manga na Uhamaka ilitoe hilo eneo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali imeanza ukarabati kwenye uwanja wa ndege wa sasa, je, Serikali itamaliza ukarabati huo lini ili na sisi tuweze kuutumia uwanja huo kwa kupanda ndege? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Sima na wananchi wa Mji wa Singida wawe na subira, tupate taarifa ya mwisho ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili hatua ya pili ifuate. Si rahisi tukaanza kutenga fedha kwa mwaka huu na hasa vipaumbele ambavyo tulipitisha mwaka huu, mtakumbuka ambavyo tulipitisha katika mpango wa mwaka huu wa fedha, vinahitaji rasilmali fedha nyingi na hivyo hii kazi tutaifanya mara badaa ya kazi hii ya upembuzi yakinifu kukamilika. Itakuwa sio rahisi kwa mwaka huu, mnafahamu kwamba bajeti ya mwaka huu tumeshaipitisha katika ngazi ya Kamati na hivi sasa tunaanza kuingiza katika hatua za Bunge Zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu ukarabati; nimhakikishie Mheshimiwa Sima kwamba kazi hii ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina itakapokamilika suala la ukarabati litafuata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali, atafuatia Mheshimiwa Bura.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nishukuru kwamba uwanja wa ndege wa Lindi upo kwenye mapendekezo ya Serikali ya kutaka kuufanyia ukarabati lakini kwa sasa wananchi wa Lindi tunakosa huduma ya ndege mpaka twende Mtwara kwa kuwa uwanja ule sasa hivi umekuwa ni chakavu sana. Nataka *commitment* ya Serikali, ni lini itakamilisha ukarabati wa uwanja wa ndege wa Lindi ili ndege zianze kutua kama kawaida?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli uwanja wa Lindi ni kati ya viwanja 11 vinavyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Kimsingi kazi hii itakapokamilika ndipo tutapata ratiba kamili ya tuanje wapi na tumalizie wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nimkakishie Mheshimiwa Bobali, kwamba kutokana na umuhimu wa kuhakikisha wananchi wa Lindi nao wanakuwa na kiwanja cha ndege, tutahakikisha katika kuangalia *priority*, na lindi tutaiangalia kwa macho matatu. (*Makofii*)

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa kupanua uwanja wa ndege wa Dodoma, lakini upanuzi huo umeathiri sana barabara ya *Area D round about* ya Shabiby, na wananchi wanaotoka *Area Dna Majengo Mapya* hurudi mpaka Kisasa kuja mjini kilometra nyingi.

Je, Serikali iko tayari kujenga barabara nyingine ya lami kuwapunguzia safari ndefu wananchi wanaokaa maeneo ya *Area Dna Majengo Mapya?* (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunahitaji kuangalia upya namna *Area C* na *Area D* inavyoweza kufikika ukitokea Dar es Salaam bila mzunguko huo mkubwa kwa kuhakikisha tutapata barabara nyingine badala ya ile ambayo sasa hivi imefungwa kwa ajili ya kiwanja cha ndege. Kwa hiyo, namhakikishia Serikali nayo inalifkiria na tutalifanyi kazi kwa haraka hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Sokombi, halafu Mheshimiwa Kangi.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa sababu pia uwanja wa Musoma upo kwenye ajenda hiyo na kwamba upembuzi yakinifu umeshafanya. Kwa sababu kutengwa fedha ni kitu kingine na ujenzi ni kitu kingine, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi katika uwanja wa Musoma?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Sokombi na wananchi wote wa Mji wa Musoma na viunga vyake ambao kwa kawaida wamezoea kutumia uwanja wa ndege wa Musoma kwa safari zao kwamba Serikali iko makini na katika muda wa hivi karibuni kama mtakumbuka tuliwaambia katika viwanja vitatu vya mwanzo tutakavyohakikisha kwamba ujenzi wake unaanza haraka ni pamoja na Musoma, Nduli na Mtwara.

Naomba nimhakikishie Serikali ipo mbioni kuhakikisha viwanja hivi vitatu vinapata fedha na uzuri wake fedha za viwanja hivi vitatu vinatarajia ataketupa fedha maana sio mfadhilli ni mkopehsaji hivi karibuni.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa fursa niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ya msingi ametamka neno fidia, kuhusiana na kuwafidia wale watakaoathirika na ujenzi wa kiwanja cha ndege Singida. Kwa kuwa neno hilo fidia amewatonesha na kuwakumbusha wananchi wa Mwibara ambao barabara ya Bunda, Kisoria na Nasio kwa miaka mingei hawajafidiwa. Je, wananchi hao wanataka kumsikia Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini watafidhiwa au kwenye mwelekeo wa bajeti fidia ya Mwibara ipo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lugola amekuwa akifatilia sana suala la fidia katika eneo lake, na naomba nitumie fursa hii kumdhiihirishia yale ambayo tumekuwa tukimwambia ofisini na maeneo mengine ambako amekuwa aktuuiliza swali hili ni sahihi, kwamba tunatafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia na kwa kweli nimhakikishie mara tutakapopata hizo fedha suala la fidia hilo tutalishughulikia kwa kazi sana.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Manispaa ya Iringa na kiwanja cha ndege cha Nduli kimekaa kimkakati, ukizingatia kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii inaboresha *Southen Sackett* kwa ajili ya kuimarisha utalii Kusini mwa Tanzania. Ni lini sasa Serikali ilikuwa imeahidi kwamba kiwanja hiki kitaboreshwa kama ambavyo Waziri amesema kwamba ni miongoni mwa viwanja 11 ili Manispaa ya Iringa iweze kukua kiuchumi na kimkakati kwa ajili ya *ku-boost* uchumi wa Taifa ambao kimsingi uchumi unaenda chini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilijibu swali la Mheshimiwa Sokombi, kwamba katika viwanja ambavyo tunatarajia kupata mkopo hivi karibuni ni kiwanja cha Musoma, Nduli na Mtware. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Msigwa kwamba kiwanja cha Nduli nacho kipo katika mtazamo wa mbele sana ili kuhakikisha kwamba utalii unaongezeka katika mbuga yetu ile ya Ruaha na kuleta mapato makubwa kwa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabati, ajiandae Mheshimiwa Waitara ambaye atakuwa wa mwisho.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye Kamati ya Miundombinu; kwa kuwa uwanja huo huo wa Nduli tayari kuna pesa zimetengwa kwa ajili ya ukarabati huo lakini pia mradi huu umeshakubaliwa na wananchi kwa sababu Serikali tayari ilishakaa na wananchi waliopo katika eneo lile. Sasa naomba jibu kutoka kwa Serikali, kwa sababu kuna wananchi ambao wamekuwa wakiendeleza maeneo ambayo yataguswa sasa ni lini itaweka alama na ili wasiyaendeleze maeneo yale ili wakati wa kulipa fidia pesa iwe kidogo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, jiandae Mheshimiwa Waitara!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ritta Kabati amekuwa akihoji haya masuala ndani ya Kamati ya Miundombimu na mimi niendelee kumpongeza kwa namna anavyochukua hatua kuwatetea wananchi na kuhakikisha kwamba maslahi yao yanazingatiwa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kama ambavyo nimekuwa nikimhakikishia mara nydingi katika Vikao vya Kamati, kwamba kazi hii ya kuweka alama tutaifanya hivi karibuni. Naongelea si zaidi ya miezi mitatu, minne ijayo kazi hii itakuwa imekamilika ili kuhakikisha kwamba wananchi wa pale wanajua mipaka ya maeneo tutakayotumia katika kukarabati na kupanua ule uwanja wa Nduli.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Tunaunga mkono juhudi ambayo inafanyika ya kuboresha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam. Lakini kuna malalamiko ya muda mrefu ya wananchi wa Kata ya Kipawa, Ukonga - Kipunguni, Kigiragira kule Buyuni, wanadai fidia Serikali mpaka leo na wameshindwa kufanya shughuli za kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua ni lini mgogoro huo utamalizwa na Serikali ili uwanja ukamilike na wananchi wakaendelea kuwa na amani na kuishi maisha

ambayo na wenyewe wanapaswa kuishi kama binadamu wa kawaida hapa Tanzania? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kumthibitishia Mheshimiwa Waitara pamoja na jirani yake Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, Mbunge wa Segerea kwamba kazi milioifanya, mtakumbuka mimi ndio Mbunge wa Segerea alinileta kukutana na wale wananchi wa Kipunguni, kuhusiana na suala hili. Niwaombe kwamba tulidhamiria suala hili tutalimaliza katika miaka hii mitano. Mnafahamu baadhi ya maeneo tumeshaanza kulipa fidia, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa unalifahamu hilo na umelifuatilia kwa kasi sana na ninakuhakikishia pamoja na Mheshimiwa Waitara kwamba wananchi wale watalipwa fidia katika miaka hii mitano. Kuna matatizo ambayo yapo katika suala hili la fidia.

**MWENYEKITI:** *Order please!*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunashughulikia matatizo yaliyoingiliwa katika suala hili la fidia, kuna wajanja wachache walitumia fursa wakatumia fedha vibaya na tumepelekea *PCCB* wanafanya kazi, tutakapopata taarifa *PCCB* tutakuja kulimaliza hili suala la fidia katika wale ambao wamebakia kulipa.

**MWENYEKITI:** Ashante Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Kigola.

Na. 40

**Mradi wa Maji Mufindi**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza kujenga mradi wa maji wa Sawala, Mtwango, Rufuna na Kibao?

## **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa Sawala - Kibao ambao utahudumia vijiji vya Sawala, Mtwango, Rufuna na Kibao vilivyopo katika Kata ya Mtwango uliana kutekelezwa tarehe 01/06/2015 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 01/06/2016 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huo ulipangwa kufanyika kwa awamu tatu ambazo ni kujenga *intake* na kupeleka maji kijiji cha Sawala, kujenga mfumo wa bomba kuu kutoka kijiji cha Sawala hadi Kibao na kujenga mtandao wa kusambaza maji katika vijiji vya Mtwango, Rufuna na Kibao. Awamu ya kwanza utekelezaji umefanyika katika kijiji cha Sawala kwa mkataba wa gharama ya shilingi milioni 644.21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa, jumla ya shilingi milioni 261.64 zimetumika kwenye mradi. Kazi zilizotekelawa hadi sasa ni pamoja na ujenzi wa *intake, sump well, pump house*, ulazaji wa bomba kuu, ujenzi wa tenki la mita za ujazo 200, ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 16 na sehemu ya mabomba ya usambazaji kilometra 3.4; kwa wastani kazi iliyofanyika imefikia asilimia 50 kwa kijiji cha Sawala tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo haukuweza kukamilika kwa wakati kutohana na mkandarasi kushindwa kukamilisha kazi kwa mujibu wa mkataba. Mwezi Novemba, 2016 Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilivunja mkataba na mkandarasi huyo, na kuamua kuutangaza upya tarehe 07/02/2017 ili kuweza kupata mkandarasii mwingine wa kumalizia kazi zilizobaki. Mkandarasi anatarajiwa kupatikana mwezi Juni, 2017 na kazi itakamilika katika mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigola.

Waheshimiwa Wabunge, leo kipindi cha bajeti maswali ni saa moja tu tumbakiwa na dakika saba tu za maswali. Maswali ambayo tutayachukua sasa ni ya msingi peke yake, kwa sababu ili tuwe na wachangiaji wengi kwenye bajeti. Mheshimiwa Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoa na majibu mazuri ya Naibu Wazirl ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kutangaza na kutafuta mkandarasi sasa hivi imeanza muda mrefu toka mwezi wa pili na imechukua karibu miezi sita sasa, ukisema mpaka Juni itachukua miezi sita. Swali langu, je, kutafuta mkandarasi kisheria inatakiwa miezi mingapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Jimbo langu la Mufindi Kusini tuna tatizo kubwa sana la maji, ukizingatia Serikali ilijenga matenki ya maji katika kijiji cha Igowole, Nyororo, Idunda, Itandula, Kiyowela matenki haya yote yameharibika sasa hivi yana miaka karibu sita, je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha watu wa Igowole na Nyororo na vijiji nilivyotaja vinaweza kupata maji na kukarabati mitando ambayo imeharibika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja anasema muda au mchakato wa kumpata Mkandarasi unakuwa mrefu sana unatumia muda gani; upo kwa mujibu wa sheria. Muda wa manunuzi upo kwa mujibu wa sheria ambayo ilipitishwa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kuna matenki 11 yaliyojengwa na sasa hayana maji, ni kweli tatizo hili nilikuta pia Nanyamba, kuna matenki zaidi ya saba ambayo

yalijengwa na *AMREF*na yalikuwa hayana maji. Matenki yale yalikuwa yamejengwa pamoja na visima. Sasa jumuiya za watumiaji maji ambazo tuliziunda tumekuta changamoto ziko nyigi unakuta kulikuwa na *pump, pump* imekufa, kuna jenereta, jeneretaimekufa. Wakati mwingine kisima kinakuwa kimekosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sasa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunachokifanya sasa hivi tumefanya uchunguzi tukakuta kwamba hzi jumuiya zinaelekea kushindwa kufanya hii kazi; lakini sio kwamba ni kwa sababu yao tu, hapana; ila ni kwa sababu ya miundombinu iliyowekwa hawana uwezo wa kuiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumechukua utaratibu wa kuweka *solar* na visima vilivyopo tutavisafisha maeneo yaliyokuwa na mtiririko tutayaweka vizuri kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma na yele matanki yanafanya kazi iliyotarajiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa niaba Mheshimiwa Chikota.

Na. 41

### **Kilimo cha Umwagiliaji Bonde la Mto Ruvuma**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA (K.n.y. MHE. HAWA A. GHASIA)** Aliuliza:-

Wananchi wa Kitere na Bonde la Mto Ruvuma wamekuwa wakijishughulisha na kilimo cha mpunga kwa miaka mingi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wakulima hao kuwa na kilimo cha umwagiliaji katika maeneo hayo?

## **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI Alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umwagiliaji wa Kitere uliana kutekelezwa mwanzoni mwa miaka ya 2000 ambapo shughuli zilihusisha ujenzi wa bwawa, mifereji na vigawa maji mashambani. Ujenzi huu ulifanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha na kukamilika Disemba, 2015. Mradi una jumla ya eneo la hekta 270 na wananchi wanaonufaika ni takribani 3,300 ambaao kwa sasa wanajihuisha na kilimo cha mpunga na mbogamboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya Bonde la Mto Ruvuma, mwaka 2012 Serikali kwa kushirikiana na *SADC* iliajiri mtaalam mshauri Kampuni ya *SWECO* toka Sweden aliyepewaa kazi ya kuainisha matumizi mbalimbali ya Bonde la Mto Ruvuma ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme, umwagiliaji na uhifadhi wa mazingira. Kazi hii tayari imekwishafanyika na taarifa ya mtaalamu mshauri imeainisha maeneo yote ambayo yatafanyiwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umwagiliaji wa Kitere na ile iliyopo katika Bonde la Mto Ruvuma tayari imekwisha ingizwa katika Mpango wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ambaao hivi sasa unafanyiwa mapitio ili uendane na hali halisi ya sasa.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara yangu imeyaweka maeneo hayo katika bajeti kwa ajili ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa lengo la kuendeleza maeneo hayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mosi, kuhusu Mradi wa Kitere pamoja kwamba majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanasema mradi umekamilika, lakini mradi huo umekamilika lakini haufanyi kazi kama unavyotakiwa na mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri shahidi amepita pale na hakuona hizi ekari 3,000 zimelimwa. Kwa hiyo, naomba kauli ya Serikali kwamba, kuna mkakati gani wa kukamilisha mapungufu yaliyopo ili mradi huo sasa uweze kufanya kazi pasavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kupitia Ofisi za Umwagiliaji Kanda, kuna miradi mingi hapa nchini ambayo haifanyi kazi. Juzi Kamati yetu ya *LAAC* ilikuwa Tabora, kuna mradi haufanyi kazi, kuna mradi Liwale, kuna mradi Mkuranga na miradi mingine. Sasa Serikali ina kauli gani kuhusu ushauri unaotolewa na ofisi hizi za umwagiliaji kanda ambazo miradi mingi ambayo inabuniwa na ofisi hizi huwa haifanyi kazi ipasavyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi nenda tu moja kwa moja kwenye hoja yake.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge Chikota, ambayo yote ni kama swalii moja kwamba, miradi hii haifanyi kazi vizuri. Lakini pia ameonesha kuwa na utata kidogo katika ushauri wa taasisi yetu inayohusika na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza katika swalii la msingi, Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba sasa hivi miradi yote hii ya umwagiliaji tunaifanya mapitio. Na tulichokibaini ni kwamba tulijenga skimu za umwagiliaji, lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi zile skimu za umwagiliaji zimekuwa ama zinafanya kazi mara moja kwa mwaka na wala sio mara mbili kutokana na ukosefu wa huduma ya maji kwa kuwa miradi hiyo hatukuijengea mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapitia katika mpango huu kabambe wa mwaka 2002 tuhakikishe kwamba, miradi hii sasa inafanyiwa usanifu na kutekelezwa kuhakikisha kwamba, inafanya kazi ile iliyotarajiwa. Lakini mapungufu pia yaliyojiteze katika miradi hiyo tutayapitia, ikiwa ni pamoja na kuimarisha tume yetu ambayo Waheshimiwa Wabunge ninyi wenyewe mmeunda Tume ya Umwagiliaji kwa ajili ya kusimamia moja kwa moja shughuli ya umwagiliaji.

Na. 42

**Tanzania Kupeleka Vikosi vya Kulinda Amani  
Ndani na Nje ya Afrika**

**MHE. ALLY SALEH ALLY** Aliuliza:-

Tanzania imekuwa ikipeleka vikosi vya kullinda amani ndani ya Afrika na sehemu nyingine duniani kadri mahitaji na hali inavyoruhusu na kutimiza dhima ya duniani.

(a) Je, mazoezi kama haya yanaimarisha jina la Tanzania kiasi gani katika jukumu hili?

(b) Kama miaka kumi iliyopita Tanzania imepeleka vikosi maeneo gani na kwa misingi gani?

(c) Changamoto gani zinakuwepo katika kukusanya vikosi hivyo kabla havijapelekwa nje ya nchi kwa kzi kama hizo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa na inatimiza wajibu wake wa kuzisaidia nchi zenye migogoro ili kuleta amani pale inapoombwa kufanya hivyo. Ushiriki wetu umetuletea

heshima kubwa duniani kwa mara zote kuonesha utayari wetu wa kutoa msaada kwa ulinzi wa amani pamoja na kazi nzuri unayofanywa na jeshi letu katika kutekeleza jukumu hilli.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka kumi iliyopita Tanzania imepeleka vikundi nya ulinzi wa amani katika maeneo yafuatayo;

- (i) Lebanon, kombania mbili toka mwaka 2008;
- (ii) Darfur, Sudan, kikosi kimoja toka mwaka 2009; na
- (iii) DRC zaidi ya kikosi kimoja toka mwaka 2013.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo katika kukusanya vikundi kabla ya kupelekwa nje ya nchi kwenye majukumu ya ulinzi wa amani ni zifuatazo:-

(i) Gharama za kuvihudumia vikosi hivyo vikiwa kwenye mafunzo;

(ii) Gharama ya vifaa nya wanajeshi vitakavyotumika eneo la uwajibikaji; na

(iii) Ugumu wa kupata mafunzo ya uhalisia wa maeneo wanakokwenda kwa mfano jangwani, misituni na kadhalika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Albeto.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wanaokwenda kwenye maeneo hayo ambako ni kwa kulinda amani mara nyingi hukutana na kujeruhija au kufariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa Tanzania tumeshuhudia wanajeshi hao wakirudi wakiwa wamefariki na wengine wakijeruhija. Je, Serikali, hasa kwenye watu waliofariki, ina utaratibu gani ambao unafanya familia za wanajeshi hao, wapiganaji haokuendelea na maisha baada ya *bread winner* wao kufariki? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, Mheshimiwa Waziri umezungumza hapa kuna matatizo wakati wa kutayarisha vikosi, lakini mimi naona hii ni fursa.

Je, Serikali haioni kwamba, kuna haja ya kujifunza na kutafuta utaalamu kutoka nchi ambazo zime-*specialize* katika masuala ya kulinda amani, ili iwe ni fursa ya kufungua kituo (*centre*) ya ku-*train* watu kwa ajili ya kulinda amani kwa ajili ya eneo hili la Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika baadhi ya maeneo ya ulinzi wa amani huwa vinatokea vifo na pengine pia huwa watu wanajeruhiwa, lakini upo utaratibu madhubuti wa kuwafidia kwa yote mawili. Nitoe tu taarifa kwamba kwa wale ambao wamepoteza maisha katika ulinzi wa amani Umoja wa Mataifa wenyewe unafidia na wanaporudishwa hapa familia zao zinapata maslahi yao yote kwa mujibu wa utumishi ambao mhusika alikuwa ameutekeleza hapa nchini.

Kwa hiyo, katika hili hakuna mgogoro, fidia huwa zinatolewa kama utaratibu unavyotaka kwa wote waliojeruhiwa pamoja na wale waliopoteza maisha kwa pande zote mbili, Umoja wa Mataifa na Serikali na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kujifunza kutoka maeneo mengine juu ya ulinzi wa amani; nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, hapa Tanzania tunacho chuo cha ulinzi wa amani. Tumepata msaada kutoka kwa Serikali ya Canada, wamekijenga na mara nydingi tunatoa mafunzo, si kwa Watanzania peke yao, ikiwemo na nchi nydingine za Afrika Mashariki wanakuja hapa kujifunza mafunzo haya ya ulinzi wa amani kwa hiyo, hili halina tatizo, tunaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi, nililosema ni upungufu wa fedha za matayarisho, si suala la mafunzo, mafunzo yapo na chuo tunacho na mafunzo yanaendelea pale kama kawaida.

Na. 43

**Mpango wa Kuunda Bodii Mpya ya Tumbaku (TTB)**

**MHE. MARGARET S. SITTA** Aliuliza:-

Pamoja na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kutatua matatizo ya wakulima wa tumbaku katika Mkoa wa Tabora akiwemo wa Wilaya ya Urambo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuunda Bodii ya Tumbaku (TTB) nyingine ili ianze kazi haraka iwezekanavyo baada ya Bodii ya Tumbaku iliyovunjwa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha pembejeo za msimu ujao zinamfikia mkulima wa tumbaku mapema wakati huu ambapo bodii husika imevunjwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, lenye Sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, A, ni kweli kuwa Serikali imevunja Bodii ya Tumbaku Tanzania kwa lengo la kufanya marekebisho katika utendaji kazi wa bodii. Hatua hii ya kuvunja Bodii ya Wakurugenzi haihusu kusitisha shughuli zinazotekelizwa katika tasnia hii ya tumbaku kwani wapo wataalam wanaoendeleza utekelezaji wa mpango uliopo na kuendeleza soko la tumbaku nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa uwepo wa Bodii ya Tumbaku nchini kwa maendeleo ya

tasnia hii ya tumbaku, utaratibu unaandaliwa wa kuunda Bodi mpya ya Wakurugenzi haraka iwezekanavyo na wananchi watataarifiwa kuititia tamko la Serikali mara baada ya taratibu kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo za muhimu kwenye zao la tumbaku ni pamoja na mbolea aina ya *NPK*, mbolea aina ya *CAN*, nyuzi za kufungia tumbaku wakati wa kuvuna na wakati wa masoko, vipande vyta magunia na madawa. Pembejeo hizo huagizwa kuititia vyama vikuu vyta ushirika kwa kila eneo kwa kuititia mchakato wa zabuni unaosimamiwa na kuratibiwa na vyama vikuu vyta ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa wakulima wanahitaji huduma muda wote hasa kipindi hiki cha kuelekea masoko ya tumbaku kwa msimu wa 2017/2018, Serikali kuititia Mrajisi wa Vyama vyta ushirika nchini ameshateuwa timu nydingine ambayo ipo Mkoani Tabora ikiendelea kuratibu na kusimamia masuala mbalimbali ya wakulima, ikiwa ni pamoja na kuandaa upatikanaji wa pembejeo kwa msimu ujao. Hivyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, pamoja na Bodi ya *WETCU* kuvunjwa, lakin kazi za chama kikuu zinaendelea kama kawaida.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu. Pamoja na majibu yako na jitihada kubwa inayochukuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kutatua changamoto za zao la tumbaku, naomba niulize maswli ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, msimu wa kuuza tumbaku, yaani msimu wa masoko ya tumbaku ni sasa, ni mwezi huu wa nne, Serikali inatoa kauli gani kuhusu yafuatayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uongozi wa *AMCOS* ambao umefutwa kutohana na agizo la Serikali na kuwaacha bila uongozi kipindi hiki ambacho masoko

yanaanza? Serikali inasema nini kuhusu suala hili? Ikiwemo *AMCOS* ya Utenge na Nsenga ambazo hazina uongozi hadi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali inasemaje kuhusu kuwasaidia wakulima ambao wamejithidi wao wenye kutokekopa, lakini hatimaye wamejikuta wanabebeshwa madeni yasiyowahusu na kuwaacha hoi kiuchumi. Serikali inatoa kauli gani? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uuzaaji wa tumbaku katika mazingira ambayo uongozi wa *AMCOS* umefutwa au umesimamishwa; taratibu zitaendelea kushughulikiwa kwa kupitia Chama Kikuu katika maana hiyo *WETCU* na kama nilivyokwishsema tayari *WETCU* imewekewa utaratibu wa mpito, ili kuweza kufanya kazi zake kama kawaida. Kwa hiyo, kama kuna *AMCOS* ambazo hazina uongozi uuzaaji wa tumbaku utaendelea kushughulikiwa na chama kikuu cha ushirika, lakini vilevile kwa kushirikiana na vyombo vingine kama Maafisa Ushirika, lakini vilevile kwa kupitia watendaji ambao bado wapo kwenye Bodi ya Tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusu wakulima ambao wanalazimika kubeba mzigو wa madeni ambayo yametokana na wao kuwepo kwenye vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya sababu zilizosababisha Mheshimiwa Waziri Mkuu kuchukua maamuzi mazito kuhusiana na *WETCU* na Bodi ya Tumbaku ni kwa sababu kulikuwa na usimamizi mbovu sana kuhusiana na madeni ya vyama vya ushirika, hali ambayo ilisababisha wakulima kimsingi kubebeshwa madeni ambayo kwa kiasi kikubwa hata matumizi ya fedha ambazo zimekopwa utaratibu wake haufahamiki sawasawa. Kwa hiyo, hatua ambazo zinachukuliwa ni ili kuondoa hiyo hali, ni ili ifahamike

kwamba, mikopo ambayo inachukuliwa inafanya kazi gani, lakini vilevile ni kuwawajibisha wale ambao wamekopa fedha na kuzitumia kwa njia ambazo ni kinyume na taratibu.

Na. 44

### **Wanafunzi Wanaopata Mikopo ya Elimu**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** Aliuliza:-

Kuna malalamiko makubwa kwa upande wa Zanzibar kuhusu idadi ndogo ya wanafunzi wanaopata Mkopo wa Elimu ya Juu jambo ambalo linapunguza idadi ya wataalamu kwa upande wa Zanzibar, hivyo kuingia katika soko la ajira katika Afrika ya Mashariki na Kati na kujengwa nchi yetu kwa ujumla.

(a) Je, Serikali haioni kuwa Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu inatakiwa kutenga asilimia maalum kwa wanafunzi kutoka Tanzania Zanzibar?

(b) Je, bajeti iliyotengwa kwa mwaka huo wa 2015/2016 ni kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Matta Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, lenye Sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu huzingatia matakwa ya sheria, kanuni, vigezo na miongozo itolewayo mara kwa mara na Serikali kuititia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Vigezo muhimu vinavyozingatiwa ni pamoja na kwamba muombaji awe ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, awe mhitaji, mlemavu au yatima. Aidha, muombaji anatakiwa kuwa amedahiliwa katika taasisi ya elimu ya juu

na awe anachukua programu za vipaumbele vya taifa ambavyo ni ualimu wa sayansi na hisabati, uhandisi wa gesi na mafuta, sayansi za afya na uhandisi wa kilimo na maji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 kiasi cha shilingi 480,599,067,500 kilitumika kwa ajili ya kugharamia mikopo pamoja na ruzuku kwa ajili ya wanafunzi 124,358.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwoneyekiti, ahsante sana kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nisawazishe jina langu, mimi naitwa Mattar Ali Salum, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akilijibu alijibu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake ambayo ameyatoa. Mheshimiwa Waziri, wapo wanafunzi wanaendelea kupata mikopo ya Serikali kwa kima kidogo hadi sasa, husababisha kukosa kukidhi mahitaji ya vyuo husika ambavyo wamepangjiwa. Je, Serikali ni kwa nini isiwaongezee fedha wanafunzi hawa ili waweze kukidhi mahitaji ya vyuo husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pilii, wako wanafunzi walikuwa wakipata mikopo kwa kipindi kirefu, ghafla Serikali imewafutia mikopo yao, sijui ni kwa nini. Je, Mheshimiwa Waziri, Serikali ina mpango gani wa kuwarejeshea mikopo hawa wanafunzi ili waweze kukidhi na kuendelea na masomo yao vizuri? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Mbunge, kama alivyorekebisha jina lake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kiuhalisia tulingependa kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi, lakini vilevile ingewezeekana hata kila mwanafunzi akapata

mkopo kwa kadiri ya mahitaji ya chuo anachosoma; lakini kwa sababu fedha hazitoshii inakuwa ni vigumu kufanya hivyo na tunaangalia zaidi ni uhitaji wa kiasi gani upo.

Kwa hiyo, kwa misingi hiyo niseme tu kwamba, Serikali itaendelea kutenga fedha ya kuona kwamba, inawasaidia wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu kufuta mikopo. Ni kweli kuna baadhi ya wanafunzi walifutiwa mikopo kutokana na kutokuwa na vigezo vinavyostahili. Hata hivyo Serikali imeendelea kulifanyia kazi suala hilo ili kuona kwamba, anayefutiwa mkopo iwe kweli ni mtu ambaye hana uhitaji. Kwa yule mwenye uhitaji na kwamba vigezo vyote vimetimia basi, baadhi yao tumeweza pia kuwarejeshea.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa maswali yote yamekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni walioko Jukwaa la Spika; tunao Waheshimiwa Wajumbe wanane wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Bajeti wakiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed, karibuni Bungeni. Hawa wamekuja kwenye mafunzo, watakutana na Kamati ya Bajeti muda huu ili wabadilishane mawazo kwa nia njema ya nchi yetu. (*Makof!*)

Pia tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni waliokuja kutembea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni, pamoja na Madiwani ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Mheshimiwa Charles Makoga na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Chumi, karibuni Bungeni. Mbunge wenu anawapenda, sasa tena na ninyi mumpende (*Makof!*)

Tangazo la semina; naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho, Jumatano, tarehe 12 mwezi huu, mwaka huu, kutakuwa na semina kwa Wabunge

wote kuhusu masuala ya hisa. Semina hiyo ambayo itaratibiwa na taasisi ya *Vodacom*, *Dar es Salaam Stock Exchange* na *Capital Market Security Authority* itafanyika katika Ukumbi wa Bunge kuanzia saa 7:00 mchana. Aidha, katika semina hiyo Wabunge watapata fursa ya kununua hisa za *Vodacom*. Katibu!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, hebu soma... unayo Kanuni hapo eeh? Soma Kanuni ya 52. Mheshimiwa Sugu kaa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 52 inasema; "Shughuli za Serikali zitaanza wakati Spika atakapomwita Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyetoa taarifa ya kuwasilisha Muswada au ya kutoa hoja Bungeni baada ya Katibu kusoma jambo linalohusika kwenye Orodha ya Shughuli."

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** (2) Baada ya Spika kutoa wito huo Mbunge ye yeyote binafsi hataruhusiwa kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge wala kuuliza swali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hizi kanuni tuzisome. Nikishamwita Katibu...Subirini, nikishamwita Katibu, naanza shughuli zangu. Nataka mniwahi, siyo mimi niwawahi ninyi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaah!

**MWENYEKITI:** Kwa vile mlikuwa hamjui na sasa mnajua...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Tulikuwahi.

**MWENYEKITI:** Subiri basi Sugu! Mheshimiwa Msigwa kaa kwanza. Kwa vile mlikuwa hamjui, sasa nimewajulisha, nawapa fursa leo Mheshimiwa Mchungaji Msigwa na Mheshimiwa Sugu. (*Makof*)

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na Sixtus Mapunda.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye Kanuni ya 68(7), naomba mwongozo wako wa kikanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Bilago, Mbunge wa CHADEMA na Mjumbe wa Kamati Kuu CHADEMA Taifa ambaye pia anawakilisha UKAWA, aliomba mwongozo kuhusu matusi ya Mbunge wa CCM, Mheshimiwa Mlinga dhidi ya Upinzani ambapo alieleza namna ambavyo Mbunge huyu anatoa matusi Bungeni, lakini anaachwa bila kuchukuliwa hatua zozote *with impunity* na ameshazoea. Lakini Naibu Spika alikuwa amekalia Kiti akamjibu Mheshimiwa Bilago, Mjumbe wa Kamati Kuu kwamba suala hilo kwa kuwa lilitokea jana yake, kanuni hairuhusu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita, akina Mheshimiwa Kangi Lugola wa CCM waliomba mwongozo kuhusu jambo lilitokea siku tatu zilizopita kwenye uchaguzi *EALA*, tena nje kwenye *press*. Japokuwa zilikuwa zimepita takribani siku tatu, mwongozo wao ulifanyiwa kazi, hatimaye Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Mbowe ambaye alihukumiwa kwa kuzungumza kwenye *press* na Mheshimiwa Mdee wakaitwa katika Kamati ya Maadili, tena kwa mkwara wa kukamatwa na polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni *double standard* ya hali ya juu na inaligawa Bunge. Unapoligawa Bunge, kwa kuwa humu kuna wawakilishi wa Taifa, maana yake unaligawa Taifa kule nje bila kujijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mwongozo wako, kwa nini kiti kinakuwa na *double standard* ya hali hiyo hasa anapokalia Naibu Spika? Kwa sababu Kanuni ya 64(7) inahusu jambo lilitotokea mapema, lakini haisemi jambo lilitotokea mapema leo, inaweza kuwa mapema leo, jana, juzi hata mapema mwezi uliopita kwa mujibu wa kanuni ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nasimama kwa kanuni hiyo hiyo ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi na ni ukweli usiopingika kwamba katika kipindi cha hivi karibuni wananchi pamoja na sisi Wabunge tuko kwenye taharuki kubwa kwa vitendo vinavyofanyika katika nchi yetu vya watu kutekwa na watu ambao hawajapewa mamlaka ya *ku-arrest* au *ku-interrogate* kufanya kazi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku mbili hizi kuna baadhi ya Wabunge wa pande zote mbili wameomba mwongozo ili Bunge liweze kujadili kwa manufaa ya Wabunge wenyewe na Taifa kwa ujumla kwa sababu sisi ndio wawakilishi wa wananchi lakini mwongozo huo umekataliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Spika jana amekataa, yeye ana walinzi, ana ma-*bodyguard*. Sisi Wabunge hatuna walinzi katika nchi hii. Watanzania wengi huko mitaani wanaishi kwa hofu na sisi ndio wasemaji wao. Masuala makubwa kama haya ninavyojua, mimi sio mwanasheria lakini chombo pekee kinachoruhusiwa *ku-arrest* na *ku-interrogate* ni Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yametokea matukio makubwa ya kutisha; tumeona watu ambao hata Wizara

ya Mambo ya Ndani inayohusika, inasema mtu aliyemnyooshea bastola Mheshimiwa Nape, sio Polisi, lakini mpaka sasa yupo kwenye *custody*, hajakamatwa. Watu walioenda kuteka *tv* ya *Clouds*, Jeshi la Polisi limesema hawakuwa polisi. Hawa watu hawajawa *arrested*. Sasa chombo kikubwa kama Bunge, tumekaa kimya, *business as usual* na Serikali katika kipindi chote hiki haijatoa tamko lolote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye Waziri wa Sheria hapa amekaa kimya, hasemi chochote kuhusu sheria inasemaje? Sasa hili ni Bunge gani ambalo tutaka kimya, mambo makubwa kama haya katika nchi yanatokea? Tunafanya nini hapa? Nilikuwa naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

### **MBUNGE FULANI:** Roma bado...

**MHE. MICH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Roma kisaikolojia inaonekana bado ametekwa. Mtu kama yule huwezi kum-*parade* kwenye vyombo vya habari; anatakiwa akutane na *psychologist* am-*counsel* kwanza. Sasa mnampeleka pale anatumika kama *stepping stone*. Bunge kazi yake ni kujadili mambo haya, tutakaa tunafanya nini? Huu ni mukutano wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, kazi yetu ni nini kama tunaomba haya mambo halafu Waziri anayehusika hasemi, Waziri wa Mambo ya Ndani amekaa kimya, haya mambo yanatokea katika nchi? Sasa tufanyeje kama Wabunge? Na sisi Wabunge tunanyamazishwa. Mheshimiwa Mwakyembe Wizara haimhusu, kasimama pale anatoa matangazo. Sasa sisi kama Wabunge tufanyeje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

### **MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni unayo nafasi na sitaki kuingilia utaratibu wako wa kikanuni wa kuweza kutoa ufanuzi wa miongozo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameiweka mbele yako kwa mujibu wa kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu wewe sasa kama Mwenyekiti wa Bunge hili na kwa kuwa mambo haya yameendelea kuzungumzwa, nadhani itakuwa vizuri Waheshimiwa Wabunge ambao wanazungumza jambo hili na kama wana ushahidi wa kutosha wa mambo haya... (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** ...Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bunge, wafanye utaratibu ili tuweze kulimaliza jambo lenyewe vizuri kwa kuzingatia maamuzi yaliyotokea, lakini kwa kuzingatia utaratibu pia wa kimfumo na wa kisheria. Kuna haja sisi Waheshimiwa Wabunge wote kwa pamoja tupate nafasi nzuri ya kupata uthibitisho wa mambo haya kupitia taratibu zinazotakiwa na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa na jambo hili liweze kufikia mwisho kwa kufuata sheria na taratibu zilizopo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, kwetu sisi Waheshimiwa Wabunge ambao tumekuwa tukilieleza jambo hili toka jana nadhani...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ah, wewe kaa chini!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kaa chini!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Huyu anaingilia mamlaka ya kiti.

**MWENYEKITI:** Kaa chini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ifike mahali sasa tuchukue nafasi yetu kama Wawakilishi wa Wananchi kulisaidia Taifa tulete uthibitisho mbele ya meza yako na hatua ziweze kuchukuliwa kwa kufuata kanuni, taratibu na sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba mwongozo, nilikuwa wa kwanza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, haya mambo yanazungumzwa...

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti unayumba.

**MWENYEKITI:** Mimi nayumba? Unataka nikutoe nje ujue ninavyoyumba? Aah, unataka nikutoe nje ujue ninavyoyumba? (*Makofii/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema *Chief Whip* hili suala kiti inalichukua na tutalifanyia maamuzi baadaye. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na

Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatia Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah na Mheshimiwa William Ngeleja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuweza kunipatia fursa hii nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba Waheshimiwa Wabunge kama tunatambua ni nini wananchi wametutuma kufanya kwenye Bunge hili Tukufu, basi tuwatendee haki kwa kufanya yale ambayo wametutuma kufanya na kutokujitoa ufahamu na kufanya kinyume na ambavyo tumetumwa na wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni na ninaomba Waheshimiwa Wabunge msome hotuba zote pamoja na kwamba mtakuwa mnayo mengine kichwani, lakini hotuba ya Upinzani kwa kweli imeeleza mengi na mazuri kwa Taifa letu, tuweze kuishauri vema Serikali ili tuweze kusonga mbele kama nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 nilisema kabisa wakati wa bajeti imepitishwa na niliandika kwenye mtandao wa Bunge, nikasema hii bajeti ikitekelezwa hata kwa asilimia 70 tu, nikatwe kichwa changu. Mbunge mmoja, ndugu yangu Mheshimiwa Chegeni akaingia *inbox* akaniambia unamaanisha nini? Sasa napenda nimwambie nilichokimaanisha ndiyo tunachokiona leo, kwamba mpaka leo bajeti ya maendeleo hata asilimia 40 hatujafika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kwamba kuliko kuja na bajeti ambazo hazina uhalisia, kama mpaka leo hatujafika asilimia 40, ile bajeti ya mwaka jana, tuchukue nusu yake ndiyo tulete. Tulete bajeti ambazo zinatekelezeka. Tusiandike matumaini kwenye makaratsi mwisho wa siku hata asilimia 50 tu hamfikishi. Tuwe na uhalisia ili hata unapokuwa umeelezwa kwamba mathalan Mkoa wa Mara Jimbo la Tarime Mjini kwenye maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tutaleta shilingi bilioni moja, basi na hiyo shilingi bilioni moja tuweze kuitekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningezungumzia tuliondoa *duty free* kwa majeshi kwa maana Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi, Askari wa Uhamiaji, Askari wa Majini na Magereza. Cha ajabu mpaka leo kumekuwa na *double standard*. Kuna wengine wameshalipwa mara mbili, kwa maana ya kila mwezi laki, laki; wameshalipwa shilingi laki sita. Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Askari Polisi, lakini Askari wa Uhamiaji, Majini na Magereza mpaka leo hawajalipwa. Ndugu zangu, tunataka kujuu ni kwa nini kunakuwa na *double standard*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu awaangalie ndugu zetu Magereza, wamekuwa wakionewa sana. Unakuta Askari Magereza ana *degree* lakini bado analipwa mshahara kama yule askari wa kidato cha nne. Leo mnawalipa hawa wengine, lakini hawa Askari Magereza nilliotatja mpaka leo hamjawalipa. Wale watu ni muhimu sana na ikizingatiwa kuna watu mnawapeleka kwa kesi za kubambikwa kule Magereza. Hawa watu wakiamua kugoma, wale watu waliopo magerezani kule kutakuwa hakukaliki. Kwanza mngekuwa mnatumia busara zaidi, mngewalipa wale kabla hata hamjawalipa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Naomba mzingatie hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna madeni wanadai ya mwaka 2012/2013; 2013/2014 mpaka leo hawajalipwa. Leo mfungwa akitoroka, hawa ndugu zetu wanapewa adhabu kutokwenda masomoni, wanapewa adhabu ya kukatwa fedha, maisha wanayoishi ni duni na kipato chao ni duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri husika tunaomba hawa ndugu zetu muazingatie na wenyewe waweze kupata hiyo *package* ambayo mliiondoa ya *duty free* nao waweze kupata stahiki zao kama mnavyowapa Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ametanabaisha kwamba wamejitätahidi sana katika

kuwawezesha wananchi, lakini ukisoma ameainisha kwamba kuna shilingi bilioni moja sijui pointi ngapi wamewapa vijana kwa mfuko wa vijana na shilingi bilioni 4.6 kuititia Halmashauri, kwamba ndiyo hapo wamewezesha wananchi. Hatuko *serious* na Serikali hampo *serious*. Mlituambia mmetenga milioni 50 kwa kila kijiji au mtaa, mpaka leo mtuambie mmetekeleza vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waziri Mkuu akija akasema kwamba Halmashauri zimejitalidi kupeleka *4.6 billion* kuwezesha wananchi ilhalii mkijua kuna Halmashauri nyingine hazina kipato cha kutosha, mathalan Halmashauri ya Mji wa Tarime, tumejitalidi, hapo zamani walikuwa hata hawatoi hela. Kwa mwaka huu, tumejitalidi tumetoa *ten million*. *Ten million only*; leo mnasema tunaweza kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itekeleze ile ahadi yao ya shilingi milioni 50 kila mtaa na kijiji; tumehamasisha wananchi wameunda vikundi mbalimbali na *SACCOS* tunazihitaji hizo shilingi milioni 50. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye elimu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndugu yangu amesema kabisa tumejitalidi kutoa elimu bure na vitu kama hivyo. Ni dhahiri baada ya kuja hii elimu bure sijui, wakasema kwamba usipopeleka motto, unafungwa; kweli tumeandikisha watoto wengi sana mashulenii, lakini hatuangalii idadi. Tunatakiwa tuangalie *qualityya* ile elimu ambayo tunaitoa. Leo mmesajili wanafunzi wengi, lakini walimu wanadai madeni mengi na hamjawapa mazingira mazuri ya kuwafanya wafundishe watoto wetu waweze kuelewa, hawana motisha yoyote ile, leo mnategemea kutakuwa na ufaulu mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmesema mmerekebisha madawati. Sawa, madawati kwanza kuna sehemu nyingine bado hayajatosheleza, madarasa hayatoshi. Wananchi wanajenga, Serikali inashindwa kwenda kuezeka, vitabu hamna pamoja na kwamba TWAVEZA jana wamesema *ratio* ni moja kwa tatu, lakini mimi kwangu darasa la kwanza na

la pili ni moja kwa tano; darasa la tatu mpaka la saba, kitabu kimoja; wanafunzi 50 mpaka wanafunzi 100. Hapo tunategemea elimu bure itatoka wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe *serious*, kama tunataka tutoe elimu ambayo ni nzuri kwa wanafunzi wetu, elimu bora, tuwekeze na walimu wawe na motisha, wapewe fedha stahiki, walipwe madeni yao na wawe na mazingira mazuri ya kufundishia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee afya. Hospitali ya Mji wa Tarime mmeandika kwamba bado ni Hospitali ya Wilaya ya Tarime, lakini mnaleta *OC* na *basket fund* ambazo zinatumika idadi ya wananchi wa Mji wa Tarime, wakati kiuhalisia wanahudumia wananchi wa Wilaya nzima ya Tarime, watumishi mmepunguza idadi wakati wanahudumia wananchi wa Wilaya nzima ya Tarime, wengine wanatoka Rarya na wengine Serengeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwepo na vigezo stahiki. Kama mnaona ni vyema hospitali ile iwe ya Wilaya, basi tunaomba *OC* na *basket funds* zije kwa idadi ya wananchi wa Wilaya ya Tarime na siyo idadi ya wananchi wa Mji wa Tarime. Mnawapa kazi kubwa watumishi, unakuta daktari anafanya masaa zaidi ya 30 wakati alitakiwa awe kazini kwa saa nane tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye maji. Kuna mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria ambao usanifu ulishafanyika na Benki ya Maendeleo ya Ufaransa wapo tayari ku-sponsorhuo mradi ambao unaanza Shirati, Ingili Juu, Utigi, Tarime mpaka Sirari. Kuanzia mwaka 2011 watu wamefanya *design* mpaka leo haujatekelezwa. Napenda kujua ili kutatua tatizo la maji Tarime, ni lini huu mradi utaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, fidia ya ardhi ya wananchi ambao Jeshi la Wananchi wa Tanzania wamechukua. Nimekuwa nikiimba sana hapa Bungeni na Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba unisikilize katika hili.

Mheshimiwa Mama Ritta Kabati mwache Waziri Mkuu anisikilize, maana nimekuwa nikiimba hii kuanzia mwaka 2007. Jeshi la Wananchi wa Tanzania limechukua maeneo ya wananchi wa Nyandoto, Nyamisangula na Nkende mpaka leo hawajalipwa. Kama... (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, ajiandae Mheshimiwa Munde.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo leo hii kusimama hapa. Pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na kupongeza hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa jinsi ilivyoelekeza Serikali kwa mwelekeo wa mwaka 2017/2018. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nitazunguka katika maeneo machache kabisa kuhusu ulinzi na usalama wa taifa, utawala bora na uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote duniani inaongozwa kwa kutegemea Katiba na Sheria. Ni hatari kubwa sana kuona Katiba na Sheria za nchi zinavunjwa wakati watawala wanasaidia na kufurahia. Narejea, Katiba na Sheria zinavunjwa katika nchi hii, watawala wanasaidia lakini pia wanafurahia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri zaidi ni uchaguzi haramu wa Zanzibar wa Machi, 2015. Uchaguzi huu ulivunja Katiba ya nchi, viongozi walifurahia na wamesaidia, lakini tunasema mapambano yanaendelea, haki ya Zanzibar tutaidai na tunaendelea kuidai na itapatikana kwa hali yoyote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitendo vya uvunjaji wa sheria kwa Msajili wa Vyama Siasa, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ni Kamati ya Bunge, inapofanya kazi Kamati ya Bunge ina maana Bunge zima linafanya kazi. Taarifa za Kamati ya Katiba na Sheria inaweka wazi kwamba Msajili wa Vyama vya Siasa amevunja Sheria za Vyama vya Siasa na kuingilia uhuru wa vyama vya siasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni taarifa ya Bunge na taarifa ya Bunge inakemea kitendo hiki cha Msajili wa Vyama vya Siasa. Kauli hii ni ya Bunge, siyo Kamati ya Katiba na Sheria. Waheshimiwa Wabunge wote lazima mwone hili lipo na limekemewa na Kamati ya Katiba na Sheria. Kwenda kinyume kwa Msajili kwa vitendo hivi, atakwenda kinyume na taarifa za Bunge. (*Makof*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip*.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia Kanuni ya 68(8) kumpa Taarifa mchangiaji wa hoja. Uksoma Taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria hakuna kifungu chochote katika Taarifa hiyo ambacho kimesema kwamba Msajili wa Vyama amevunja sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati imetoa ushauri kwenye Ofisi ya Msajili wa Vyama, imetoa ushauri kwa Msajili wa Vyama kuvilea na kuvishauri vyama na hajiasema Msajili wa Vyama amevunja sheria. Kwa hiyo, naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Mbunge asiiwekee Kamati ya Bunge maneno ambayo hayamo kwenye taarifa ya Kamati ya Bunge. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Rashid.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MBUNGE FULANI:** (*Aliongea nje ya kipaza sauti*).

**MWENYEKITI:** Sasa mpaka mumfundishe!

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo siikubali na Kamati ya Sheria ilmwita Msajili, ikamhoji (ukurasa wa 30 naendelea kusoma) na ikamwonya Msajili huyo. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba masikitiko yangu na nitaendelea kusikitika sana kuona Jeshi la Polisi linashiriki kisiaza wazi wazi na kuleta hujuma na kuvunja sheria wakati Jeshi la Polisi linalinda uvunjaji wa sheria. Nalaani sana vitendo hivi. Watu wote mnafahamu, mnajua na mnaona, halihitaji ushahidi, Serikali imenyamaza kimya. Hii nasema ni mkakati wa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi limepoteza mwelekeo kwa wananchi na litaendelea kupoteza mwelekeo kwa wananchi kwa sura hii, tutakuwa hatuna imani kabisa na Jeshi la Polisi. Na mimi nilishasema, sitaki kuchangia Jeshi la Polisi, sina imani kabisa na Jeshi la Polisi. Baadhi ya Jeshi la Polisi wanavunja sheria, Serikali ipo inayamaza kimya, wanashiriki uvunjaji wa majengo ya chama, Jeshi linalinda na linaangalia tu bila kuchukua hatua yoyote. Kitendo hiki ni kibaya sana kwa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msajili pamoja na washirika wake mlivunja Katiba ya Vyama vya Siasa na mlivunja Sheria za Usajili. Kwa kufanya hivyo, amevunja msingi mkubwa wa utawala bora na kwa misingi hiyo, amevunja demokrasia nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Msajili ajue, matokeo yake ni nini? Matokeo yake atalingiza Taifa hili katika mgogoro mkubwa kwa Muungano wetu, lakini atahatarisha amani ya Taifa hili, la tatu, ataingiza Taifa hili

katika mgogoro wa kiuchumi. Mnalifurahia lakini matokeo yake mtayaona mbele tunakokwenda. Kwa kufanya haya, uchumi wetu utadorora, ndani na nje ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka haraka kuhusiana na masuala ya uchumi. Sekta za uzalishaji mara nyingi zinakuwa ni sekta za kiuchumi na kwa maana hiyo kuna nchi nyingi ambazo zimejikita katika maeneo mahsus ya kiuchumi, kwa mfano, nchi ya Afrika Kusini imejikita katika biashara, madini na utalii; Algeria mafuta na uzalishaji; Nigeria mafuta na mawasiliano, Morocco utalii, viwanda vya nguo pamoja na kilimo. Tanzania kuna msururu kabisa, *series!*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## **TAARIFA**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Nchi aliposimama hapa dakika chache zilizopita alinukuu ripoti ya Kamati kwamba Kamati...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, sasa unampa nani taarifa?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa msemaji.

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa, kaa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Ningemwomba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid, endelea.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kuna *series* za mambo ya kiuchumi, kuna kilimo, viwanda, maliasili, madini, gesi, usafirishaji *and so on and so forth*. Kilimo kinawakilishwa kwa asilimia 75 na Watanzania,

kilimo kinabeba Watanzania wengi sana, lakini awamu hii inaelekea kana kwamba kilimo siyo kipaumbele chake hasa, kina viashiria hivyo. Nasema hivyo kwa sababu mwaka 2015/2016 Serikali iliyopita ilitoa pembejeo za kiasi cha shilingi bilioni 78, lakini Serikali hii hadi kufika hapa imetoea pembejeo za shilingi bilioni 10. Kutoka shilingi bilioni 78 mpaka shilingi bilioni 10, hivi kweli Serikali hii inawaambia nini wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kusema kwamba kilimo kinaanza kushuka na kwa sababu hakuna mbolea ya kutosha ambayo imetolewa na Serikali, tutegemee upungufu mkubwa wa mazao katika kipindi kinachofuata. Hili litakuwa ni tatizo kubwa kweli kwa wananchi walio wengi wa Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Munde Tambwe. Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Chikota na Mheshimiwa Nkamia wajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa niapongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, nampongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake, Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Mavunde pamoja na Baraza zima la Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Wabunge wenzangu wa Tabora kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutatua kero ya tumbaku Mkoani Tabora. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakuombea kila la heri, Mwenyezi Mungu akuwezeshe ili

umalize kero hii ya tumbaku ambayo imetukabili kwa miaka mingi sana. Tunakuamini, tunajua utaimaliza na umedhamiria. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya, wameanzisha programu maalum ya kuhakikisha wanafutilia llani ya Chama cha Mapinduzi itekelezeke, lakini kufuatilia ahadi zote za viongozi wakuu. Nawapongeza pia kwa kuhamia Dodoma, wamefanya kazi kubwa. Tulikuwa tunasikia toka tukiwa wadogo kwamba Serikali inaenda Dodoma, lakini imeenda Dodoma leo hii. Tunaipongeza sana Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Kitengo cha Baraza la Uwezeshaji ambacho kipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Baraza la Uwezeshaji limefanya kazi kubwa ya kuwatambua, kuwabaini wajasiriamali wadogo ambao kwa Mkoa wa Tabora wameianza kazi hiyo na kuwawezesha kuwapa mitaji ili waweze kusonga mbele na huu ndiyo uchumi wa kati ambao tunautaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri tu Serikali yangu, naishauri Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba hili Baraza la Uwezeshaji lingeungana na watu wa *SIDO* likaungana na Wizara ya Viwanda ili kuwawezesha hawa wajasiriamali wadogo sasa waweze kuingia kwenye viwanda vidogo vidogo, mkiungana nadhani itakuwa vizuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee kuhusu bajeti. Nimesikia wenzangu wanasema kwamba kulikuwa na bajeti hewa, nimesikia jana kuna neno linaitwa bajeti hewa ambapo mimi kama Mbunge wa Tabora sikubaliani na hiki kitu cha bajeti hewa na sababu ninazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ukiniambia bajeti hewa, mimi nimeingia hapa Bungeni mwaka 2011, nilikuwa nahangaika kila siku kugombana kuhusu maji ya mradi wa Ziwa Victoria, leo hii mkandarasi yuko *site* toka mwaka 2016. Kwa hiyo, ukiniambia bajeti hewa, siwezi kukuelewa. Tulikuwa tunahangaika na barabara ya lami ya

Chaya – Tula ambayo inaunganisha kutoka Dar es Salaam - Tabora mpaka Urambo kwa lami, leo hii mkandarasi yuko site. Pia tulikuwa tunahangaika kwamba uwanja wetu wa ndege unatua ndege ndogo tu, leo hii mkandarasi yuko site anafanya matengeneza ya kupanua uwanja wa Tabora. Kwa hiyo, sikubaliani kabisa na kuniambia kwamba kuna bajeti hewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, punda hasifiwi kwa rangi zake, anasifiwa kwa kazi anazozifanya na mzigo anaobeba. Hii Serikali ya Hapa Kazi Tu inafanya kazi sana, Rais wangu Mheshimiwa Dkt. Magufuli anafanya kazi sana. Wamwache Mheshimiwa Rais afanye kazi! Toka nikiwa mdogo nikiwa Tabora nasikia Waheshimiwa Wabunge wa Tabora wanalamika kuhusu reli ya kisasa, lakini leo hii minara ya reli ya umeme imeanza kutengenezwa. Reli ya *standard gauge* inajengwa. Leo mtu ananiambia kuna bajeti hewa, sitakaa nikubali. Huu ni uongo na niwaombe Wabunge wenzangu, tuseme Serikali inapofanya mambo mazuri, tusinyamaze, tusiogope, tuseme. Nimetoka kifua mbele, nasema Serikali yangu imefanya mambo makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa humu Bungeni kipindi kilichopita, kaka yangu Mheshimiwa Zitto kama yupo atasema. Tulikuwa tukisimama tukiungana kulilia ndege, wanasema nchi gani hii, inashindwa hata na Rwanda, haina hata ndege moja. Leo tuna ndege, watu wanasema kwa nini tumenunua ndege? Wamwache Mheshimiwa Rais afanye kazi, waiache Serikali ifanye kazi. Tukifanya kazi, mnasema, tusipofanya kazi, mnasema. Tunajua binadamu hata ufanye nini, hawezi kukusifia kwa asilimia 100, tufanye kazi kama tulivyojipangia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea elimu bure. Kuna mtu labda ana hela watoto wake hawasomi shule hizi anaona utani. Leo hii shule zimejaa, madarasa yamejaa, watoto wanasoma, hakuna *ma-house girl* vijijini. Yote hii ni juhudhi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu na Serikali yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeona juzi, mwaka 2016 hii bajeti hewa *UDSM*, leo hii watoto 4,000 watakaa kwenye mabweni *UDSM*, yamejengwa kwa muda wa haraka sana. Leo unaniambia Serikali haijafanya chochote, sitakubali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *REA*, tumemwona Mheshimiwa Muhongo huko, umeme unawaka vijiji. Leo hii tunashindwa kusifia Serikali yetu. Nawaomba Wabunge wenzangu, tusiingie baridi, tutoke tuseme mema yaliyofanywa na Serikali yetu. Watu wanasema viwanda, viwanda gani? Vitajengwa lini? Viwanda hewa. Mpaka hapa ninapoongea, tunajenga viwanda 2,160 na hii *issue* ya viwanda tumeanza juzi mwaka 2016, Magufuli kaingia mwaka mmoja. Mimi niwaulize Wabunge wenzangu, ninyi kwenye Majimbo yenu mwaka mmoja mmeefanya mangapi? (*Makof*)

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mbona mnaisema Serikali tu! Kuna watu hapa hawajawahi kufanya chochote. Akimwona *DC* ameenda kwenye mkutano wa *DC*, naye anakwenda kama Mbunge. Lako wewe kama Mbunge liko wapi? Tuoneshe. (*Makof*)

**MBUNGE FULANI:** Sema, sema.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali yangu, nampongeze Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wake, wanafanya kazi. Hii nchi ni kubwa jamani, kazi ni ngumu. Ni rahisi sana kukosoa, lakini ukiambiwa kafanye wewe, hiki kitu ni kigumu jamani, tuwatie moyo, tuwaombee kwa Mwenyezi Mungu waweze kutekeleza walioyaahidi. Ni faida yetu sisi wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajisifu Tanzania ni kisiwa cha amani, Tanzania ina amani, Tanzania ina utulivu, nani aliyetuletea utulivu? Ni Usalama wa Taifa. Leo tumo

humu, tuna amani tu. Leo tukitoka tutaenda Club, tunaenda tunarudi hata saa 9.00 usiku, tuna amani. Kama kuna madoa madogo madogo, basi yatashughulikiwa, lakini tusiseme Usalama wote hawafanyi kazi. Hiki kitu nakataa na nitaendelea kukataa. Tuko hapa kwa sababu ya amani. Tunajisifu, tuna sifa dunia nzima, kisiwa cha amani. Amani inatengenezwa, kuna watu hawalali kwa ajili ya amani hii tuliyonayo, ni lazima tuwatie moyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuga mbwa ukiona habweki, bweka mwenyewe. Leo nimeamua kusema mwenyewe. Wenzetu hawa kama hawayaoni haya, leo nimeamua kuyasema mimi niliyeyaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongezee kidogo kuhusu Msajili wa Vyama vya Siasa (*Registrar*), amekuwa akishambuliwa sana. Nasema vyama vingi ni tatizo, ni kazi kubwa. Sheria zake anazozisimamia, ndiyo maana leo tumekaa Wabunge wa CUF, wa CCM, wa CHADEMA tunaongea kwa sababu wa usimamizi mzuri wa *Registrar*. Tulishuhudia watu walitaka kupigana viti kule Ubungo kwenye mikutano yao, lakini *Registrar* kwa kazi yake kubwa aliyoifanya, ndiyo leo CUF kuna amani na utulivu. Ndiyo leo wameweza kukaa pale wote wakiwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida sana tunapokuwa tunawashambulia wataalam, tuwatie moyo kwa kazi wanazozifanya. Pale kwenye upungufu tusiache kusema; tuseme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kusema, naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, nampongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli na sisi tumwambie tupo, tutasema. Sisi ni wanasiasa, kazi yetu ni kusema. Tutasema na tunamuunga mkono kwa asilimia mia moja kwa kazi anazozifanya. CCM oyee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngeleja. Mheshimiwa Chikota na Mheshimiwa Nkamia wajiandae.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru sana. Na mimi naungana na wenzangu kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri sana, ye ye pamoja na wasaidizi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijazungumzia mambo manne ambayo nimepanga kuyazungumzia, nina salamu za pongezi kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Sengerema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, tunaipongeza Serikali, lakini kwa hapa tunazungumza mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tufikie salamu kwa viongozi wote wakuu wa nchi yetu pamoja na wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo mnaratibu shughuli za maendeleo ya Taifa letu. Tunazungumza kama Wabunge tukiwa tumejumuika kutoka katika maeneo mbalimbali. Yapo maeneo ambayo sisi wenyewe kutoka kwenye maeneo tunayofanyia kazi ni mashahidi kwa namna ambavyo shughuli za maendeleo zinafanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa namna ambavyo imeshughulikia jambo moja kubwa ambalo lilishakuwa kidonda ndugu kwa Taifa letu nalo ni nidhamu ya kazi. Taifa lilikuwa limefikia mahali pabaya. Sisi wote ni mashahidi, tumekuwa tukifika kwenye taasisi za umma na kuona namna ambavyo huduma zimekuwa zikitolewa miaka iliyopita, lakini tuseme kweli kabisa, katika hii Awamu ya Tano, tumeshuhudia mageuzi makubwa ya uwajibikaji kwa Watendaji wetu. Kwa hilo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, lakini kiranya mkuu katika usimamizi wa Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Shukrani za pekee kwa namna ambavyo unalifuatilia hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Sengerema tuna mambo makubwa yamefanyika, moja, namshukuru sana Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummu pamoja na Mheshimiwa

Dkt. Kigwangalla kwa namna ambavyo mnatusaidia katika Jimbo la Sengerema. TAMISEMI pale, Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Waziri Simbachawene, kile Kituo cha Afya cha Ngoma A ambacho mmekitengea fedha, wananchi wa Sengerema wamenituma nifikishe salamu zenu kwa shukrani kwa namna ambavyo mnatufanyia kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa *Engineer* Lwenge na msaidizi wako Naibu Waziri, ule mradi mkubwa kabisa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ngazi ya Halmashauri na Wilaya unaofanyika Sengerema, sasa uko katika hatua za mwisho kabisa. Shukrani kwenu pamoja na Serikali nzima kwa namna ambavyo mmesimamia mradi huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene tuna kiporo. Tumezungumza miezi michache iliyopita. Kwenye hesabu za Mfuko wa Jimbo zillzofanywa hivi karibuni, yapo baadhi ya Majimbo ambayo tulipunjwa. Halmashauri ya Sengerema ni mojawapo hali iliyotokana na makosa ya kimahesabu. Mmetuahidi kwamba kufikia mwisho wa mwezi huu fedha zile zitakuwa zimeshafika, lile salio. Naomba Mheshimiwa Simbachawene na Serikali kwa ujmla, jambo la mapunjo ya Mfuko wa Jimbo mlifanyie kazi, fedha zifike mahali pake, zifanye kazi kwa ajili ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizamie kwenye mchango, la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaanzia kwenye ukurasa wa 43. Umeanzishwa mfumo wa wazi wa kielektroniki kufuatilia uwajibikaji na utendaji wa Serikali, jambo hili ni kubwa sana. Ni muhimu tuipongeze Serikali. Wamesema, kwa kupitia utaratibu huu, *wata-track* utekelezaji wa ahadi ambazo zimefanywa na Serikali kupitia llani ya Chama cha Mapinduzi, matamko, ahadi za viongozi wakuu wa Serikali akiwepo Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali katika hili ni kwamba kwa sababu hatuna mashaka yoyote kuhusu umakini na Serikali yetu, lakini pia kwa kutambua kwamba sisi Wabunge ndio daraja la wananchi na Serikali,

nilikuwa naomba uandaliwe utaratibu ambao Serikali kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, watakuwa wanatushirikisha Wabunge, tujiridhishe kujuu yale ambayo tunaya-track katika maeneo yetu ya kazi ni yapi? Miradi gani ambayo inaonekana katika ule mfumo? Mahali ambapo pamesahaulika, sisi tuwakumbushe kwa kusema hili nalo ni sehemu ya yale mambo yaliyokusudiwa, yafanyiwe kazi kupitia huu mfumo wa kielektroniki ambao utawasaidia Watanzania kufahamu shughuli ambazo zinafanywa na Serikali.

Kwa hiyo, naomba na nilikuwa naamini kwamba atakapokuwa anafanya majumuisho Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake, atatusaidia kuona umuhimu wa kutushirikisha sisi Wabunge tujue miradi ambayo uki-google ama ukibonyeza ule mfumo unakuletea miradi iliyotekelizwa katika maeneo yetu. Tusipofanya hivyo, narudia tena kusema kwamba, sina mashaka na utendaji wa Watumishi wa Serikali, lakini binadamu ni binadamu. Sisi ni jicho la pili kusaidia kufikia yale yaliyokusudiwa katika kuyasimamia yaliyotekelizwa kwa namna ambayo tunakusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia jambo moja la kufanya maendeleo katika maeneo yetu ya kazi. Tunapanga bajeti, kila mwaka tunaipitisha hapa. Tumekuwa na changamoto ambayo sijapata jibu lake, tutasaidiana kadri ambavyo siku zinaendelea. Suala la *disbursement*, kufikisha pesa ambazo tunazipitisha hapa kwenye bajeti kwenda kwenye maeneo yetu. Ninazungumzia kutotimiza jukumu hili ama wajibu huu ambao sisi tunaufanya Kikatiba, tumekuwa tukipitisha bajeti kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza hapa Sengerema kwenye OC ambazo ndizo fedha ambazo zimeidhinishwa kufutilia miradi mbalimbali ambayo tunazungumzia hapa tuna asilimia 20 tu, lakini shughuli za maendeleo tuna asilimia 30. Nafahamu Waheshimiwa Wabunge wengi wanalamika. Hilo siyo la kumnyooshea mkono mtu yejote, lakini ushauri wangu kwa Serikali,

tusaidiane kupitia chombo hiki cha uwakilishi wa wananchi tuone namna bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejifunza na mwaka 2016 tumeshauriana hapa, yapo mambo tulikubaliana kwamba yako mambo hayakunyooka sana, lakini tutumie nafasi hii katika Bunge hili tuelewane vizuri kwa mfumo huu wa bajeti tulionao, tuone namna ambavyo tunaweza kutekeleza bajeti ambazo tunazipeleka kule. Haina maana yoyote kupitisha mafungu hapa kwa kiwango fulani halafu utekelezaji wake unakuwa chini ya asilimia 50. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachozungumza, hili ni letu sote, halina itikadi ya vyama kwa sababu tunazungumzia utekelezaji wa mambo ambayo kwa pamoja tumekubaliana kuyatekeleza. Kwa hiyo, nashauri sana Kamati ya Bajeti pamoja na Serikali kwa ujumla, tushauriane namna bora ya kuhakikisha kwamba mafungu tunayoyapitisha, fedha zilizokusudiwa zinafika mahali pake palipokusudiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mweyelekiti, ukisoma Mkataba wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo sasa ziko sita, ukisoma Ibara ya 49 inayozungumzia namna ambavyo tunaweza kuimarisha mtengamano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Inazungumzia habari ya *Bunge Sports Club* ikiwa ni chombo mahsusini kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika michezo hiyo ambayo inafahamika kutokana na Mkataba wa Jumuiya ya Nchi za Afrika ya Mashariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia jambo hili kwa sababu ninaona kuna masuala yanaingiliana na hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na hasa lile Fungu la Mfuko wa Bunge. Bajeti ya *Bunge Sports Club* inatokana na huo mfuko.

Naomba Bunge pamoja na Serikali kwa ujumla tuone kwamba ushiriki wa *Bunge Sports Club* katika michezo siyo jambo la anasa ama la kwenda kutumia pesa hovyo, bali ni nyenzo ya utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Watendaji wote wa Serikali na Bunge kwa namna ambavyo mliwezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 tulikwenda kwenye mashindano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mombasa; tuliondoka katika mazingira magumu kidogo, lakini ninavyozungumza sasa hivi mambo yote yako *level seat*. Shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Spika na Naibu Spika pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo mliwezesha jambo hilo. Tunasema ahsanteni sana. na imeandikwa katika maandiko matakatifu, asiyeshukuru kwa kidogo hatashukuru kwa kikubwa. Sisi tumejata kikubwa, kwa nini tusishukuru? Ahsanteni sana. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Moto, moto, moto.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo inayoongozwa na Mheshimiwa Mtemi Chenge. Unapozungumzia fedha nydingi ambazo tunazipitisha hapa, utekelezaji wake unakwenda kutekelezwa kutokana na miongozo na sheria zilizotungwa katika Halmashauri, Taasisi zetu mbalimbali zikiwemo Wizara za Serikali. Ninachotaka kuzungumza hapa ni kwamba tunapozungumzia Sheria zinazotungwa na Halmashauri zetu, ndiyo mpango wa fedha wenye. Tumeshuhudia wote kama Taifa, wakati mwingine viongozi wakuu wa Serikali wamekuwa wakitamka matamko ambayo wakati mwingine katikati ya safari wanaamua kuondoa tozo ambazo zimeshakubalika kwa utaratibu wa kisheria kwa namna ambavyo tumekasimu madaraka kwenye Halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, silaumu katika hilo kwa sababu kama kuna kero ni lazima ishughulikiwe hapo hapo, lakini ninachosema, tuboreshe utaratibu wa namna ambavyo tunaweza kukatiza katikati ya safari, kwa sababu hizi Sheria Ndogo ndiyo zinaongoza mafungu ya kule Halmashauri na hasa mafao yale ambayo yanakwenda

kuwawezesha hata Madiwani wetu ambao sisi tulioko hapa tunawategemea na ni Madiwani wenzetu kutekeleza miradi mbalimbali ambako fedha nyingi zinakwenda. Tusiwakatishe katikati ya safari. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya bajeti hizi, kuwe na utaratibu mzuri wa kukaa pamoja tuelewane kwamba mwaka huu tutaondoa tozo hizi na hizi ili wasizifuate kwenye bajeti zao wanazoziveka. Tukikatisha katikati tutakuja kuwalaumu hawa wawakilishi wa wananchi wenzetu kwamba hawatimizi wajibu wao, lakini kwa kweli mazingira ambayo yamesababisha kumbe nasi tumeyachangia. (*Maiofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa hili narudia kusema, simlaumu mtu ye yote lakini naomba tulifanyie kazi kwa uzuri kwa namna ambavyo tutaweza kuwa... (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chikota. Mheshimiwa Nkamia na Mheshimiwa Shangazi wajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Mheshimiwa Rais alifanya ziara Mkoani Mtwara na ametufanya kazi kubwa sana, mojawapo ikiwa ni kutatua changamoto ambayo ilikuwa inakabili Kiwanda cha Dangote. Hapa jana kuna mchangiaji mmoja alitoa maelezo ambayo pengine alichokifanya Rais kule Mtwara hakukielewa, anasema Dangote amepewa eneo la mgodi kwa ajili ya kuchimba makaa na maamuzi yale yatakuwa na athari kama tutakavyofanya mchanga kutoka kwenye migodi ya almasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika Mtwara ni tofauti na hicho alichokisema mchangiaji kwa sababu Mheshimiwa Rais ametatua changamoto mbili kuu ambazo

Kiwanda cha Dangote kilikuwa kinakabiliwa nayo. Changamoto ya kwanza ilikuwa ni upatikanaji wa Makaa na alisema tunaamua hapa hapa. Mheshimiwa Muhongo na Mawaziri wengine walikuwepo na walipewa siku saba kwamba taratibu zote zifuatwe ili achimbe mkaa mwenyewe na kodi zote stahili aliye ili apeleke kwenye kiwanda chake cha Mtwara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili, Mheshimiwa Rais alitatua tatizo la muda mrefu ambalo ni upatikanaji wa gesi asilia kutoka Madimba. Tulikuwa tunalalamika hapa kwamba wawekezaji wakubwa hawasikilizwi, kwa hiyo, Mheshimiwa Rais akatoa maamuzi pale kwamba *TPDC* impe umeme Dangote bila kupitia kwa mtu mwingine wa pili. Kwa hiyo, maamuzi yale ni ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na siyo ya kumkatisha tamaa kwamba alichofanya siyo sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa niaba ya Wabunge wa Mtwara na kwa niaba ya wananchi wa Mtwara tunamshukuru sana Rais wetu kwa maamuzi mazito aliyoafanya katika ziara yake Mkoani Mtwara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nichangie hoja nyingine ukurasa wa 23 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hatua alizochukua katika kusimamia zao la korosho. Wananchi wa Mtwara na wananchi wa Kusini wanakupongeza kwa kile ulichokifanya mwaka huu. Kwanza hukusita kuvunja bodi pale uzembe ulipotokea, lakini pili, ulichukua hatua ya kusimamisha uendeshaji wa Mfuko wa Pembejeo na kazi hiyo sasa ikapelekwa kwenye Bodi ya Korosho na kusimamia kwa karibu kwa yale yanayoendelea katika tasnia ya korosho katika msimu wote. Hata pale zilipopotea tani 2,000 kwenye lile ghalia la Masasi, ulichukua hatua za haraka na wale watuhumiwa sasa hivi wamefikishwa kwenye vyombo vyaya sheria. Tunakupongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo, bado kwenye mfumo wetu wa Stakabadhi Ghalani kuna changamoto ambazo kwa usimamizi wako Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Kilimo nafikiri msimu huu mtazirekebisha ili bei ya korosho izidi kupaa, na sisi Wana-Mtwara tunategemea bei ya korosho mwaka huu itafika kilo shilingi 5,000. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo ni pamoja na wakulima kucheleweshewa malipo na hii ni kwa sababu vyombo vingi havikujandaa na ununuzi wa msimu wa mwaka huu na ule utaratibu wa mwaka huu. Tumeona pale ghala ya Benki Kuu ilikuwa inaingia Mtwara kila baada ya siku moja. Kwa hiyo, nafikiri kwa sababu sasa hivi Tawi la Benki Kuu limezinduliwa Mtwara, yale ambayo yalikuwa yanatokea mwaka huu kwamba kila baada ya siku moja zinapelekwa fedha Mtwara, nafikiri msimu ujao hayatajitokeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna changamoto ya usafirishaji. Tumeona pale zikitokea kauli mbili; Watendaji wa Bandari wanasema Bandari ya Mtwara inaweza kusafirisha korosho lakini Mkoa wa Lindi wanasema kwamba Mtwara hawana uwezo wa kupeleka korosho zote, kwa hiyo, tusafirishe kwa barabara. Yote kwa yote, kuna changamoto pale zimejitokeza. Kwa hiyo, ni matarajio yangu kwamba Mamlaka ya Bandari, Wizara husika na Wizara ya Kilimo wataishughulikia hii changamoto ili mwakani korosho zote zisafirishwe kwa Bandari yetu ya Mtwara kwa sababu korosho zinaposafirishwa kwa Bandari ya Mtwara, tunawapa vijana wetu ajira, lakini vilevile tunadhibiti ununuzi wa korosho holela ule ambao unajulikana kwa jina la kangomba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tunatakiwa tulifanye katika mfumo wetu wa Stakabadhi Ghalani, tuongeze uwazi. Sasa hivi kuna malalamiko kwa wakulima kwamba mkulima anaiza korosho yake kwenye mnada wa pili, lakini amelipwa kwa bei ya mnada wa tano. Kwa hiyo, nafikiri hili Wizara ya kilimo italicifanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani, kuna tozo moja. Kwanza tumshukuru na tumpongeze Mhesimiwa Waziri Mkuu, mwaka 2016 kwa usimamizi wake walifanikiwa kuondoa tozo tano kwenye zao la korosho. Kwa hiyo, kuna tozo moja ambayo inalalamikiwa sana na wakulima, tozo ya uchangiaji wa gunia. Ni matarajio yangu kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya kilimo na wadau watalishughulikia suala hili ili gunia zinunuliwe na Bodi ya Korosho au Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho ili wakulima wasichajiwe ile fedha ya kuchangia ununuvi wa gunia kila kilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende ukurasa wa 36 ambaao unahusu elimu na mimi nakubaliana kauli ya Waziri Mkuu kwamba uchumi wa viwanda lazima unahitaji rasilimali watu yenyewe weledi, lakini rasilimali watu yenyewe weledi inapatikana kukiwa na mfumo bora wa elimu. Lazima hapa tukubaliane kwamba tunapozungumzia mfumo bora wa elimu au tunapozungumzia elimu bora, hatuwezi kusahau mahitaji na kero za walimu.

Kwa hiyo, naomba sana Serikali yangu ya Awamu ya Tano ijikite katika kuondoa changamoto zinazowakabili Walimu. Walimu bado wana malalamiko kwamba wana madai, bado hatujaandaa *incentive package* kwa Walimu wapewe motisha; lakini Walimu vile vile wanahitaji mafunzo kazini. Kwa hiyo, naomba Serikali chini ya Mheshimiwa Profesa Ndalichako na Mheshimiwa Simbachawene, basi walishughulikie hili suala la matatizo ya walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie mchango wangu kuhusu suala la maji. Kwanza naipongeza Wizara ya Maji kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya na katika Jimbo langu kuna harakati ambazo zinaonekana, za kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kutoka asilimia 40 kwenda kwenye malengo yetu ya kufika asilimia 85, lakini bado kuna changamoto nyingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza kuna ule mradi ambaao tunatarajia kupata mkopo kutoka

Benki ya India, miradi 17 ambapo ni pamoja na mradi wa Muheza, ule mradi wa Makonde. Kwa kweli ni muda mrefu sasa hivi tunataka mradi huu uanze kutekelezwa. Kila siku mnasema kwamba tunamalizia *financial agreement*, lakini sasa hivi natarajia Wizara ya Maji itaongeza *speed* ili mradi huu uanze kutekelezwa. Mradi huu ukianza kutekelezwa kwa miradi ile 17, tuna uhakika kwamba asilimia ya watu wetu ambao wanapata maji vijijiini itaongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kwa sisi Wana-Mtwara kuna mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma na kupeleka Manispaa ya Mtwara. Mradi huu ni tegemeo kwetu na utaongeza upatikanaji wa maji katika Jimbo langu la Nanyamba. Kwa hiyo, naomba pia na utekelezaji wa mradi huu usimamiwe kwa karibu na fedha zipatikane ili utekelezaji wake uanze mara moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na yale yote ambayo yapo katika kitabu cha Waziri Mkuu yakitekelezwa, tuna uhakika kwamba nchi yetu tunakwenda kule ambako tunatarajia. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nkamia. Mheshimiwa Shangazi na Mheshimiwa Kikwete mtoto wajiandae. (*Makofii*)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nawapongeza sana wachezaji wa Simba, jana kidogo watulaze na viatu, lakini kwa kweli kazi waliyoifanya ni nzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache tu, la kwanza nachukua nafasi hii kwa dhati kabisa ya moyo wangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuleta maendeleo ya Taifa letu. Wakati mwininge maneno haya ni kwa sababu mnafanya kazi nzuri. Ukiona mtu anakushambulia hivi, ujue unafanya

kazi nzuri sana. Na mimi niwatie shime kwamba endeleeni na kazi hiyo ili Taifa letu liweze kusonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, nawapongeza watu wa TAMISEMI vilevile na Wizara ya Afya kwa kutupatia fedha kwa ajili ya Kituo cha Afya cha Hamai ambacho kwa leo ndiyo tunakitumia kama Hospitali ya Wilaya ya Chemba. Nawashukuruni sana na ninaomba kazi hiyo ya kujenga wodi, nyumba za waganga iweze kufanyika kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nizungumzie maji. Tuna Mradi wa Maji wa Ntomoko, alisimama Mbunge mmoja hapa akasema uftutwe, lakini mimi nasema ashindwe tu, kwa jina la Yesu. Ni kama amedandia gari katikati, kwa sababu hajui chanzo chake na hajui mwisho wake. Mradi huu una changamoto zake ndogo ndogo, lakini mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kukubali kwenda, kama Mungu akijaalia wiki ijayo ili na wewe ujionee kwa namna moja ama nyingine changamoto zilizopo kwenye mradi huu ili ziweze kutatuliwa na watu wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni suala la kuhamia Dodoma. Kwa namna ya kipekee kabisa sisi Wabunge wa Dodoma tulikuwa na mkakati kabla ya tamko la Mheshimiwa Rais kuleta muswada binafsi hapa Bungeni ili Serikali ihamie Dodoma, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuamua kwa dhati ya moyo wake kuhamia Dodoma, lakini suala hili halipo kisheria. Naiomba Serikali sasa iletu muswada Bungeni hapa ili iwe sheria. Anaweza kuja mtu mwingine kesho akasema Makao Makuu ya nchi anayapeleka kwingine. Kwa hiyo, niwakumbushe hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile pamoja na kuhamia Dodoma, harakisheni ujenzi wa mradi wa maji wa bwawa la Farkwa ambao pia utaongeza maji Dodoma, Chemba, Chamwino na Bahi. Leo tathmini imeanza kule Farkwa, Mombose na Bubutole, vile vijiji vinahama basi wale watu walipwe fidia zao mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, Serikali lazima iwe *active*, lakini siyo kuwa *active* kwa kukosea. Nitoe mfano, samahani sana, jana nilikuwa naangalia mukutano wa waandishi wa habari (*press conference*) na yule Bwana anaitwa sijui nani yule...

**MBUNGE FULANI:** Roma.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Roma Mkatoliki. Hivi Waziri wa Habari alikwenda kufanya nini? Unajua wakati mwingine unaweza kuambiwa ukweli ukachukia, lakini ni afadhali uambiwe ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Habari amekwenda kwenye mukutano wa Roma Mkatoliki, anampisha na kiti, anayeongoza *press conference* ile ni Zamaradi Kawawa, Afisa wa Serikali. Hivi kesho, mtu akikwambia wewe ndio ulimteka Roma, utakataaje? Ni vizuri uchukue ukweli hata kama unauma, lakini *take it. At the end of the day* unaweza ukafanya marekebisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine mnamgombanisha Mheshimiwa Rais na wananchi bila sababu ya msingi. Mimi sikuona *logic* kabisa. Mimi siyo mwanasheria, nimesoma uandishi wa habari na nimesoma uhusiano wa kimataifa, lakini *this is wrong. Is not applicable!*

Kwa hiyo, Serikali wakati mwingine mnaingia kwenye mtego wenyewe bila kujua. Hebu liangalieni hili, ilitokea wapi mpaka Mheshimiwa Waziri anakosa kiti, anahama, halafu huyu mtu binafsi anafanya *press conference*, wewe unakwenda kufanya nini? *What were you doing there?* Halafu leo akina Nkamia wakisema ukweli humu, kuna watu wanasema, aah, unajua labda kwa sababu alikosa Uwaziri. *No, we have to tell you the reality! This is a principle!* (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu suala la kuongeza maeneo ya utawala. Hapo nyuma tumeongeza sana maeneo ya utawala lakini bado tunashindwa

kuhudumia yale maeneo tuliyoyaongeza. Hebu angalieni, malizeni kwanza tatizo la yale maeneo mliyoyaongeza ya utawala ndiyo muanze kuongeza maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Jimbo ulipoletwa, idadi ya watu ilikuwa tofauti na sasa. Fanyeni *review*, Chemba ilikuwa na watu 160,000, leo tuko watu 250,000, lakini bado kiwango cha Mfuko wa Jimbo kinachotolewa ni kile kile cha wakati ule na wakati mwingine kinapunguzwa, amesema Ngeleja hapa. Hebu angalieni namna gani mnaweza kuongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo. Jana amesema hapa Mbunge wa Kiteto, kuna tatizo kubwa kati ya Wilaya ya Chemba, Kiteto, Kongwa na Gairo. Watu wa Kiteto wanafikiri kama ni Jamhuri ya Wamasai hivi ndani ya Tanzania. Baadhi ya viongozi wanaopelekwa katika maeneo haya, nao ni shida. Hebu tusaidieni, mtaniwia radhi. *RAS* wa Manyara, *DC* wa Kiteto, *DC* wa Chemba, kabilo moja na wanawasiliana vizuri sana. Matokeo yake kumekuwa na *crisis* katika Wilaya hizi kwa sababu Wagogo, Wakaguru, Warangi hawatakiwi Kiteto. Amekaa miaka 30 anaambiwa ondoka leo. Hivi leo na sisi tukaamua Mrijo tukafunga mpaka, hakuna Mmasai kuingi Chemba...

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## **TAARIFA**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kumweleza mwenzetu kwamba wakati mwingine kuna mambo magumu yanatokea ambayo viongozi tunayaona, lakini wakati mwingine unaangalia maneno ya kutumia kwa ajili ya umoja wa utaifa wetu hata kama una uchungu wa jambo fulani, cha kwanza ni kufikiria Tanzania iliyo moja na kuchagua maneno ya kutumia na kutafuta namna ya kiuongozi ya kupeleka hoja yako na ikaeleweka. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkamia, taarifa.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni ushauri, wala siyo taarifa tu. Kwanza hawa niliowasema, ni watani zangu wote, hawa Wakurya wote watani zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, tunazungumza *leadership credibility*. Wapo watu wanapewa vitu vidogo vidogo kuwaumiza baadhi ya watu. Mtu amekaa miaka 30, unamwambia ondoka leo, acha nyumba yako, wewe ni Mrangi nenda Chemba. Wewe ni Mgogo toka, nenda Kongwa, wewe ni Mkaguru toka nenda Gairo. Tukae kimya! *This is a problem.* Ni ndani ya Tanzania hii kaka yangu anayoisema pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tufike wakati sasa tuwe *serious* ili tuendelee kuishi kwa umoja na amani yetu. Namshukuru kaka yangu pale, namheshimu sana kwa ushauri wake, nimeupokea, lakini pia kwa wakati mwingine nanyi upande wa pili muwe mnaangalia maneno ya kutumia, isiwe upande mmoja tu. Kisumu kikate kote kote. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie la mwisho, mimi ni mwana michezo. Naomba sisi Wabunge tuiunge mkono timu ya *Serengeti Boys* kwa nia njema kabisa na Serikali nayo iweke mkono wake ili timu yetu ikafanye vizuri, badala ya kulaumu tu wachezaji, na sisi tuoneshe moyo wa upendo kwa timu zetu ili tupate vijana walete heshima kwa Taifa letu. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi jiandae, Mheshimiwa Kikwete na Mheshimiwa Nsanzugwanko utachukua nafasi ya Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kunipa nafasi leo hii ya kuzungumza. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Mama

Salma Kikwete kwa kuapishwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kipindi kirefu sana amekuwa anahangaika na masuala yanayohusu watoto, hasa yatima, wasio na uwezo na akina mama. Nina uhakika kabisa kwa kupata nafasi ya kuwa Mbunge, Mheshimiwa Rais amefanya jambo jema sana kwa makundi haya na sasa watapata mtetezi wa kweli ambaye anayaishi yale atakayokuwa anayaongea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, namwombea pia kwa Mwenyezi Mungu Rais wetu apewe afya njema sana aendelee kuhudumia Taifa hili ambalo linamhitaji sana kipindi hiki kuliko muda mwingine wowote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, pia namwombea heri mzee wangu, Mzee Chrisant Majiyatanga Mzindakaya ambaye anaugua pale Dar es Salaam, Mwenyezi Mungu ampe afya njema na apone mapema ili aendelee kuwa mshauri katika maisha yetu sisi vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, napenda sana pia niwape pole wananchi wenzangu wa Jimbo la Chalinze na Halmashauri ya Chalinze hasa kwa tatizo kubwa lililotupata ndani ya siku mbili au tatu, kutokana na mvua kubwa ambazo zinanyesha sasa katika maeneo yetu. Tumeshuhudia barabara zikikatika, tumeshuhudia magari yakisimamishwa, safari zinasimama lakini baya zaidi ni uharibifu mkubwa wa miundombinu na nyumba zetu ambaao umetokea katika Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa tu taarifa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hapa ninaposimama leo hii kuzungumza, zaidi ya kaya 150 hazina mahali pa kulala wala hazijui zitakula nini kutokana na tatizo kubwa la mafuriko lililokumba eneo letu lile. Ninachomwomba yeye pamoja na Serikali ni kuangalia njia za haraka zitakazofanyika hasa katika kile chakula cha msaada ili wananchi wangu wa Halmashauri yetu ya Chalinze wapate chakula kwanza

wakati tunajipanga kuona mambo mengine tunayafanya  
vipi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia kipekee kabisa, naomba sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Chalinze kwamba Mbunge wao niko pamoja nao sana na katika kipindi hiki kigumu mimi baada ya kumaliza kuchangia leo hii, nitarudi tena kukaa nao na kushauriana nao. Pia tumeomba tukutane kama Madiwani kupitia Kamati yetu ya Fedha ili tuweze kuona tunaweza kuchanga kipi au kutoa kipi katika Halmashauri yetu ili kukabiliana na hali hiyo ngumu ambayo wananchi wenzangu wanaikabili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa nirudi katika mchango wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na nitapenda nianze na eneo la maji na viwanda. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunatambua kwamba Serikali yetu imeweka msisitizo mkubwa sana katika kuhakikisha kwamba viwanda vinajengwa katika eneo hili la Tanzania na katika kipindi hiki kifupi tumeshuhudia mabadiliko makubwa sana katika ujenzi wa viwanda. Waziri Mkuu mwenyewe anaweza kuwa shahidi na Serikali inaweza kuwa shahidi juu ya jinsi wananchi wa Jimbo la Chalinze au wananchi wa Halmashauri ya Chalinze walivyotoa maeneo yao kwa ajili ya kujenga viwanda. Viwanda takriban sita vikubwa vimekwishaanza ujenzi ndani ya Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na viwanda hivyo vinavyojengwa, tatizo kubwa sana lililokuwepo ni upatikanaji wa maji. Tulizungumza na hata juzi alipokuja Waziri Mkuu kufanya ziara katika Halmashauri yetu, aliona juu ya shida kubwa ambayo wananchi wanavyokabiliana na maji lakini pili alipata taarifa ya kina juu ya viwanda vile ambavyo vinaweza vikashindwa kuanza kutokana na matatizo ya maji. Tumezungumza mengi, lakini kubwa zaidi tulimwomba Waziri Mkuu kupitia Wizara ya Maji atoe kibali kwa wale wawekezaji wanaojenga kiwanda kikubwa cha *tiles* pale Pingo ili waweze kupata *access* ya kutumia maji ya Ruvu na siyo maji ya Wami ili waweze kujenga kiwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa maji Ruvu mpaka kwenye kiwanda pale Pingo ni kilometa zisizopungua 16; lakini kutoa maji Wami mpaka Pingo ni kilometa zaidi ya 26. Tunachoangalia hapa ni upatikanaji rahisi wa maji hayo na ninashukuru kwamba Waziri Mkuu alinikubalia. Nimeona niseme hapa leo kwa sababu hii ni mikakati ambayo ikiingizwa kwenye bajeti itakaa vizuri. Tunachosubiri kutoka kwake ni kusikia neno kwamba kibali kile kimetoka na kwamba ujenzi wa miundombinu hiyo umeanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hili tu, maji haya yatasaidia pia hata wananchi wa Mji wa Chalinze kwa namna moja au nyingine kwa sababu makubaliano yetu siyo tu maji yaende kwenye kiwanda, lakini pia yaende mpaka pale Chalinze Mjini ili kupunguza tatizo la maji tunalokabiliana nalo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia, kiwanda kikubwa kingine kinachojengwa kule Mboga cha kuchakata matunda nacho kinahitaji maji. Tumezungumza na Mheshimiwa Waziri Mwijage, tunamshukuru kwa jinsi alivyo tayari kukabiliana na changamoto hiyo, lakini pia kinachohitajika zaidi ni ule Mradi wa Maji wa Wami ukamilike mapema ili maji yapate kupelekwa pale na wananchi wa Chalinze wapate kazi, wananchi wa Tanzania wapate matunda kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi hiki cha miaka mitano hii inayoanza mwaka 2015 mpaka 2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, nije katika jambo la vita ya dawa ya kulevy. Katika vita ya dawa za kulevy tunashuhudia mamlaka mbili zenyne nguvu tofauti zikifanya kazi moja. Mimi ni mwanasheria, katika utafiti wangu au ujuzi wangu wa sheria, haiwezekani kazi moja ikafanywa na vyombo viwili na ndiyo maana katika mgawanyiko wa kazi hizi, mambo yanagawanyika kutokana na mihimili na kutokana na ofisi. Leo hii tunashuhudia, wako watu wanaitwa na Bwana Siro lakini pia wako watu wanaoitwa na Bwana Sianga. Matokeo yake sasa haieleweki, kumekuwa na *double standards* katika *treatment* ya watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba kwa kuwa natambua Sheria ya Dawa za Kulevyia inayompa nguvu Bwana Sianga ya kuita, kukamata na kufanya *inspection*, hiyo sheria pia inaingiliwa na Jeshi la Polisi. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaposimama hapa awaeleze ni jinsi gani vyombo hivi viwili vinaweza vikatenganisha utendaji ili kutoharibu mlolongo mzima wa upelelezi na upatikanaji wa watuhumiwa hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja kule kwetu na akaenda katika mbuga yetu ya Saadani, ameona jinsi mambo yanavyokwenda na ameona hali ilivyo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati anakuja kufanya majumuisho ya hotuba yake azungumzie vizuri juu ya jinsi gani tunaweza ku-*promote* utalii katika mbuga yetu ya Saadani, lakini pia azungumzie ni jinsi gani Serikali imeweza kukabiliana na vile vilio vya wananchi wanaozunguka mbuga yetu ya Saadani juu ya matatizo ya migogoro ya mipaka iliyopo baina ya mbuga yetu na makazi au vijiji vilivyo jirani hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilio vimeduwa vikubwa sana, vimefika kwenye Ofisi ya Mbunge, lakini pia vimefika kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu mwenyewe ameshuhudia watu wakigaragara kumzuia asitoke katika mbuga ya Saadani kwa sababu ya taabu kubwa wanayoipata hasa wenzetu hawa wanaosimamia mbuga wanapoamua kuchukua sheria katika mikono yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia, niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua kubwa anazozifanya. Sisi tulikutana naye, niliongea naye na baada ya kuzungumza naye, siku tatu baadaye akaja Waziri Mkuu kuzungumza juu ya kero ambazo zinawakabili wananchi wa Chalinze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Chalinze, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi alivyomwepesi kukabiliana na changamoto. Katika wepesi huo, naomba niishauri Serikali

yangu, kumekuwa na malalamiko mengi sana. Tumeshuhudia malalamiko mengine ambayo yanahitaji majawabu kama siyo majibu ya haraka ili kuondoa hizi sintofahamu walizonazo wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana, hakuna sababu ya mtu kama Mheshimiwa Waziri Mwigulu kuendelea kukaa kimya wakati wananchi wanalamika juu ya hali ya kiusalama katika maisha yao. Mimi binafsi naishauri Serikali yangu kwamba unapojibu jambo lolote lile unatoa hali ya wasiwasi na wananchi wanapata... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa ni Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako. Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Riziki Said Lulida wajiandae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijasema mengi, kwanza niunge mkono hoja hii ambayo imeletwa mbele yetu toka Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na machache sana, lakini moja kubwa naomba tu kwa namna ya pekee niwapongeze wenzetu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri na watendaji wake, timu nzima ya Serikali, mmefanya kazi nzuri sana na hasa hii kazi ya kurejesha nidhamu Serikalini, hongereni sana. Hili ni jambo jema na kila mmoja anaona tofauti iliyokuwepo siku za nyuma na siku za sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niendelee kuwashauri, kama ilivyo kazi yetu Wabunge ni kuwashauri Serikali, kwamba tunaomba utaratibu huu wa nidhamu ya watumishi wa Serikali ujikite katika kulinda misingi ya sheria. Tafadhalini sana, endelezeni nidhamu ya watumishi wa umma,

tuwaheshimu watumishi wa umma kwa kuzingatia sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa namna ya pekee naipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kumaliza ligi hii ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya ya kuwaweka ndani watumishi wa umma hovyo hovyo. Kwa kweli juhudhi zimekuwa nzuri, sasa tunaona mashindano haya hayapo tena, maana huko nyuma ilikuwa Mkuu wa Mkoa akijisikia, Mkuu wa Wilaya akijisikia anaweza kumweka ndani ofisa ye yote wa Serikali bila utaratibu. Tunashukuru sana, jambo hili wenzetu wa Utumishi, TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu mmelisimamia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, Mheshimiwa Simbachawene najua amefanya vizuri katika jambo hili, na tunakupongeza sana kwa kazi nzuri anayoifanya. Lazima Wakuu wetu wa Wilaya na Mikoa wafuate sheria kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda nilisemee limeainishwa ukurasa wa 31 na 32 wa hotuba ya Waziri Mkuu ni ujenzi wa reli ya kat i kwa kiwango cha *standard gauge*. Tunaishukuru sana Serikali kwa jithada hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe, Mheshimiwa Jenista, reli ya kat i tafsiri yake ni reli inayotoka Kigoma kwenda Dar es Salaam ikiwa na matawi ya kutoka Tabora kwenda Mwanza na matawi kutoka Kaliua kwenda Mpanda, ndiyo reli ya kat i hiyo. Sasa nimeona kwenye kitabu cha Waziri Mkuu, kuna juhudhi kubwa zimefanyika katika ujenzi wa reli ya kat i na hususan kuanza kufanya *feasibility studies* katika matawi haya ya reli ya kat i.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashauri kwamba ili reli hii iweze kuwa ya kiuchumi, maadamu inaanza kujengwa kwa kiwango cha *standard gauge* ni vizuri reli hii ikatoka Dar es Salaam ikaenda Kigoma kwa sababu ya mzigo mkubwa, tani milioni nne zilizoko katika Jamhuri ya

Demokrasia ya Kongo ambayo zinahitaji njia kwenda kwenye masoko ya Kimataifa. Tusipofanya hivyo, tutajikuta mbele ya safari, hii reli haitakuwa na faida za kiuchumi mbali na kusafirisha abiria peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda niliseme ni uwiano wa maendeleo katika Mikoa yetu. Waheshimiwa Mawaziri mlioko hapa nadhani Waziri wa TAMISEMI unanisikia, nchi yetu hii ina mikoa takribani 25. Uwiano wa Mikoa hii umetofautiana katika sekta mbalimbali, ni vyema sasa Serikali yenyewe kama ambavyo mwaka wa 2016 mlitupa takwimu za hali ya umaskini katika nchi yetu tukawa na utaratibu wa kuiinua mikoa ambayo iko nyuma, mikoa hiyo iko nyuma kwa sababu za kihistoria tu. Mikoa kama Kigoma, Dodoma, Singida, Katavi, iko nyuma kwa sababu za kihistoria. Ni jukumu la Serikali kuweka uwiano sawa wa mikoa hii katika sekta mbalimbali kama elimu, maji, afya, kilimo, barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine yana nafuu kidogo na maeneo mengine yana shida kubwa sana na wananchi wote hawa ni Watanzania hawa hawa. Kwa mfano, Mkoa wetu wa Kigoma mpaka leo bado ni mkoa haujaunganishwa na Tabora kikamilifu, haujaunganishwa na Katavi, haujaunganishwa na Geita, haujaunganishwa na Kagera, haujaunganishwa na Shinyanga, hali ni mbaya sana. Sasa naomba sana TAMISEMI mko hapa, Ofisi ya Waziri Mkuu, angalieni uwiano ambao una afya katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania hawa wana haki sawa. Maeneo mengine yana unafuu na mengine yana shida kubwa. Kwa hiyo, naomba kama ushauri Serikalini kwamba ni muhimu sana kuweka uwiano wa maendeleo katika mikoa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa niishauri Serikali ni suala la kilimo. Katika nchi yetu kuna maeneo yanapata mvua, Mwenyezi Mungu ameyabariki tu, yanapata mvua za kutosha na tunalo tatizo kubwa sana hata la kuzalisha mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwa kweli kwa miaka yote hii, miaka 50 ya uhuru sasa hatuwezei kujitosheleza hata kwa mbegu za mazao ya nafaka. Nilikuwa nafikiri ni wakati muafaka wenzetu wa kilimo na Serikali, yale maeneo yanayopata mvua za kutosha kwa mwaka mzima tuyape kipaumbele ili tuweze kuzalisha mbegu za kutosha ili tujitosheleze kwa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kwamba mpaka sasa nchi yetu tunazalisha mbegu asilimia 40 ya mbegu zilizobaki zinatoka nchi jirani kama Kenya, Zimbabwe na mataifa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nizungumzie juu ya umeme wa Malagarasi. Niwapongeze wenzetu wa nishati wamefanya kazi kubwa na taarifa niliyonayo ni kwamba wenzetu wa Benki ya Dunia na *African Development Bank* wametoa fedha kwa ajili ya kuanza kujenga umeme wa Malagarasi. Huo umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya watu wa Kigoma na ni dhahiri umeme huo utaingizwa pia kwenye Gridi ya Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa nizungumzie suala la maji, maji ni uhai na ni dhahiri kwamba maeneo yenye vyanzo vya maji vingi na mikoa ambayo ina vyanzo vya maji vingi tu sasa kwa sababu ya matatizo ya tabia ya nchi, uharibifu wa mazingira, naishauri Serikali kwamba wakati umefika maeneo yenye vyanzo vya maji tuyalinde, kuwe na mkakati wa kitaifa wa kulinda vyanzo vya maji. Kwa mfano, katika Mkoa wa Kigoma, katika Wilaya ya Kasulu peke yake tuna vyanzo vya maji takribani 600 ambavyo havikatiki mwaka mzima. Vyanzo hivi vinapeleka maji yake katika Mto Malagarasi kwa kiwango kikubwa na maji hayo hatimaye yanakwenda kwenye Ziwa Tanganyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huu mpango kabambe wa kupeleka maji Malagarasi, Urambo, Kaliua na kwingineko kama hakuna mkakati endelevu wa Serikali nina hakika tutafika mahali maji ya Mto Malagarasi yatakuwa

hayatutoshi, hayataweza kuzalisha umeme na kufanya shughuli za kilimo. Kwa hiyo, nashauri *strongly* kabisa kwamba wenzetu wa Serikali hata kama ni mwakani tuleteeni *a comprehensive plan* ya kulinda vyanzo vya maji. Iko mikoa yenye vyanzo vingi, Morogoro wana vyanzo vingi, Katavi wana vyanzo vingi tuwe na mpango mkakati kabisa kitaifa wa kulinda vyanzo vya maji katika maeneo ambayo maji hayakauki mwaka mzima. Ni kweli yako maeneo yenye shida lakini tukiwa na mkakati endelevu nina hakika maji haya hatimaye yatusaidia sisi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Mheshimiwa Simbachawene ulitembelea Kigoma, ultumwa na Mheshimiwa Rais kule Kigoma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Zitto na Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Koshuma, Mheshimiwa Mgimwa, Mheshimiwa Aeshi Hilaly wajiandae.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusiana na mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali tukifahamu kwamba Waziri Mkuu kwa mujibu wa Katiba ndiyo mwenye udhibiti na usimamiaji wa ujumla wa shughuli za Serikali. Nina mambo manne kama nitapata muda wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka kulizungumzia ni hali ya uchumi. Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri Mkuu anaonesha kwamba hali ya uchumi ni nzuri, mfumuko wa bei uko chini asilimia 5.2 lakini jana tu *NBS* wametoa taarifa mpya ya mfumuko wa bei ambao umepanda kwa kasi sana. Sasa hivi hali ya wananchi kwa kweli ni ya kupoteza matumaini, bei za vyakula zimepanda, sukari imefika mpaka shilingi 2,500 kwa kilo, maharage yamefika mpaka shilingi 3,000 kwa kilo, unga kuna maeneo ya nchi umefika mpaka shilingi 2,200 kwa kilo. Kwa hiyo, kuna

haja ya kuweza kuangalia taarifa ambazo Wizara zinapeleka Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu inaonesha kwamba taarifa ambazo Waziri Mkuu amezitoa katika ibara ya 20 ya hotuba yake ni *outdated*, siyo taarifa za sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Waziri Mkuu katika ibara ya 26 ya hotuba yake ameongelea ajira na kusema kwamba tumeingiza ajira mpya 418,000 lakini naomba ifahamike kwamba kwa mwaka Tanzania watu wanaoingia kwenye soko la ajira ni milioni 1.6. Kwa hiyo, kuingiza watu 418,000 maana yake ni kwamba kuna zaidi ya watu milioni 1.2 ambao hawajapata ajira na wako nje ya shughuli za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo kuna ajira zimepotea. Ndani ya Manispaa yako Mwenyekiti, Manispaa ya llala jumla ya biashara 2,900 zimefungwa. Maana yake ni kwamba leo llala hamuwezi kupata *service levy*, leo llala hamuwezi kupata leseni za biashara, kwa sababu biashara zimefungwa kulingana na sera za Serikali ambazo siyo rafiki kwa watu kuweza kufanya biashara inavyotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia matamko kwa mfano ya viongozi yanababisha upotevu mkubwa wa mapato. Mimi nafahamu na natambua juhudhi ambazo Rais anazifanya, anataka tukusanye mapato zaidi kwenye madini, lakini Rais hafahamu na wasaidizi wa Rais pia hawafahamu kwamba tamko lake alilolitoa Mkuranga kuhusiana na mchanga limepoteza mapato ya Serikali kuliko mapato yoyote ambayo tungeweza kuyakusanya kwa miaka 20 iliyopita na nitawapa takwimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 1998 tulipoanza uchimbaji mkubwa wa dhahabu mpaka mwaka 2016 tumeuza nje dhahabu ya Dola za Kimarekani bilioni 18 na makusanyo yetu kwa miaka yote hiyo ya kodi ni dola za Kimarekani milioni 833. Tamko alilotoa Rais Mkuranga, kwa sababu kulikuwa na mazungumzo ya kuuza Kampuni ya *Acacia* ambayo ingeingiza mapato mengi sana Serikalini kuititia *capital gain tax* ambapo tulipitisha sheria hapa,

***NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)***

tumepoteza Dola za Kimarekani milioni mia nane themanini na nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Rais anazungumza kukusanya mapato, Rais huyu huyu anaipotezea nchi mapato. Haya ni mambo ambayo tunapaswa tuwe makini nayo sana na ningeomba viongozi hasa Mawaziri wajaribu kumshauri. Tunajua ana dhamira njema, lakini tuifanye kwa namna ambayo haiathiri maslahi ya Taifa kama ambavyo imefanyika sasa hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi hapa kulikuwa kuna mwongozo ambao umeombwa na *Chief Whip* wa Serikali ametoa maelekezo ambayo wewe umeyakubali. Maelekezo ambayo *Chief Whip* ameyatoa na wewe umeyakubali hayaendani na Kanuni za Bunge. Suala la Mtanzania aliyepotea Ben Sanane, ni suala ambalo linapaswa kuchukuliwa kwa uzito wa hali ya juu sana, sio suala linalopaswa kuchukuliwa kisiasa. Sio suala linalopasa Wabunge wabebe uthibitisho waulete mezani kwako kwa sababu taarifa ambazo ziko sasa hivi na zipo Jeshi la Polisi zinaonesha kwamba Novemba 15, Ben Sanane kwenye mawasiliano yake ya simu kuanzia asubuhi alikuwa maeneo ya Tabata, akaenda maeneo ya Mikocheni, akatumia muda mwingi sana maeneo ya Mwenge, akapelekwa au akaenda Mburahati, saa nne usiku tarehe 15 Novemba, simu yake ikapoteza mawasiliano na toka hapo hajawahi kuwa *traced* tena na haya maelezo yako polisi. Ukifuatilia Jeshi la Polisi wanakwambia sisi tumefikia mwisho, lakini mwelekeo wetu unaonesha kwamba waliomchukua Ben Sanane ni Usalama wa Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ume-save kwenye Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama na Mambo ya Nje, unafahamu sheria ya Usalama wa Taifa, kifungu cha 5(2) kinaipiga marufuku Usalama wa Taifa *ku-enforce laws*. Usalama wa Taifa hawana mamlaka ya kukamata, hata wakimwona mwizi hivi, sheria inawakataza, kwa sababu ya kuepuka haya mambo ambayo tunayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumekuwa na matukio hatuyapatii ufumbuzi. Ninyi mnafahamu na mnakumbuka aliyekuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, Absalom Kibanda, alikamatwa, akateswa, akaumizwa na leo jicho lake moja, halioni lakini mpaka leo hakuna hata mtu mmoja aliyekamatwa kulingana na tukio kama hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mazingira kama haya, hatuna namna na siyo kawaida ya Bunge hili ninyi wenyewe ni mashahidi ambao mmekaa Bungeni muda mrefu kujadili Usalama wa Taifa. Kwa mara ya kwanza tunaivuka hiyo *taboo* kwa sababu watu wamechoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa mujibu wa Kanuni ya 120 ya Bunge, natoa taarifa rasmi kwamba nitaleta Hoja Binafsi ndani ya Bunge ili Bunge liunde Kamati Teule ya kufanya uchunguzi wa matukio yote ya upoteaji, mauaji na matukio ambayo yanaweza kujenga taswira hasi dhidi ya Idara ya Usalama wa Taifa katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizikumbushe Kamati za Bunge, kuna masuala ambayo Kamati za Bunge hazipaswi kupelekewa na Spika, zinapaswa kufanya zenyewe, ndiyo maana Bunge lina utaratibu wa taarifa maalum.

Mimi ningetarajia Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ingetuletea taarifa maalum kuhusu mambo haya badala ya kusubiri mpaka Wabunge wazungumze, tuanze kujianika na kama nilivyoeleza *it was a taboo* kuongelea Usalama wa Taifa ndani ya Bunge lakini leo tunaongelea kwa sababu ya utendaji mbovu ambao unaendelea.

## **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba Mheshimiwa Zitto anafahamu Kanuni vizuri sana lakini nafahamu kwamba ni mtu mwenye uwezo mkubwa wa kusoma vitu vingi na anafahamu kwamba hili analolijadili haliruhusiwi kujadiliwa humu, anazungumzia suala la Usalama wa Taifa ambalo hawezи kulijadili humu. Pia Mheshimiwa Zitto anautuhumu Usalama wa Taifa kwamba umeshiriki kukamata watu, je, anaweza akalithibitishia Bunge hili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zitto anafahamu kwamba ni makosa kufanya hivyo, *it is a taboo* lakini anasema imebidi tuvuke mipaka na sasa anauingiza Usalama wa Taifa katika kuutuhumu kwa jambo ambalo sina hakika kama anao ushahidi wa kutosha. Kwa hiyo, mimi nimuombe tu kwa ruhusa ya Kiti chako Mheshimiwa Zitto alete ushahidi wa kulithibitishia Bunge hili kwamba Usalama wa Taifa ndio waliomshikilia Ben Sanane.

### **TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Waziri, Mheshimiwa Simbachawene kwamba mimi Hussein Mohamed Bashe nilikamatwa na Maafisa wa Idara ya Usalama wa Taifa, acheni unafiki, *we are all Tanzanians in this country*. Hamjawahi kunyanyaswa ninyi, acheni.

Mimi ni mwana CCM, *I don't care* mkitaka nifukuzeni Ubunge. Mimi nimekamatwa na Usalama, nimeonewa *in this country*, acheni unafiki, tunavumilia mambo mengi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bashe, umeshaelewaka.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Acheni, hamjawahi kuwa *humiliated*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe, umeshaelewaka, ahsante.

*(Hapa Mhe. Hussein M. Bashe aliendelea kuongea bila kipaza sauti)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe umeshaelewaka, ahsante. Mheshimiwa Zitto. (*Makofii*)

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, hebu kaa kidogo muda wako tutakupa. Kufuatana na mjadala wako na kuanza kuzungumzia habari ya Kiti, Kiti kilishachukua maamuzi ya kulichukua jambo hili na kulipeleka mbele likajadiliwe kwa kina kabisa ndani ya Bunge lenyewe kwenye uongozi huko. Sasa sijui unalalamika kitu gani, ultaka hapa watu muanze kuimbaimba tu bila kuwa na jambo lolote? Haya endelea.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetoa taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 120 ya kuunda Kamati Teule na ndijo taarifa ambayo inapaswa kufanyiwa kazi kwa mujibu wa Kanuni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka nimkumbushe Mheshimiwa George anafahamu, ni rafiki yangu, ni ndugu yangu yaani ndugu kabisa, waliokwenda kuvamia *Clouds Media* ni Kikosi cha Ulinzi wa Rais na ninaweza kuthibitisha, aliyemtolea bastola Mbunge wa Mtama ni Afisa Usalama wa Taifa na ninaweza kuthibitisha. Kwa hiyo, kama Bunge linaweza likaunda chombo cha kutaka nikathibitishe hayo, niko tayari kuthibitisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie, Mheshimiwa Waziri Mkuu ibara ya 31 ya hotuba yako imezungumzia kilimo na umezungumzia mavuno ambayo tumeyapata msimu uliopita wa 2014/2015. Naomba

## *NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

nikukumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, taarifa ya Benki Kuu ya *Quarterly Economic Review* inaonesha kwamba kilimo kimekua kwa asilimia 0.3 tu. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba, wananchi wetu vijijini mwaka 2016, wengi wamekuwa maskini kwa sababu ya ukuaji mdogo katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mweyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia mbolea ambayo Serikali imenunua tani 30,000. Ni kazi nzuri sana mbolea imenunuliwa lakini naomba nikufahamishe katika kila mfuko wa mbolea ambao umenunuliwa kwa shilingi bilioni 10 Serikali ilizotoa, watu wako ama ni watendaji wa Wizara ya Kilimo au *IFC* wameongeza shilingi 15,000 kinyemela. Mnunuzi wa kawaida akinunua mbolea Dar es Salaam ananunua kwa shilingi 55,000 mpaka ifike kwa mfano Rukwa, Kigoma au Katavi mbolea ile inauzwa kwa shillingi 60,000. Leo hii mbolea ambayo imenunuliwa kwa fedha za Serikali, kwa kampuni ya Serikali ikifika Sumbawanga, Mpanda, Kigoma ni shilingi 75,000. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, jana nimekuona umechukua uamuzi katika mambo kama haya ya pembejeo, nakuomba umwagize *CAG* akague...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, nakuongezea dakika mbili.

**WABUNGE FULANI:** Anakuongezea dakika mbili.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nimeweka pia kwa maandishi nitayaleta ili iweze kufanyiwa kazi kwa uzuri zaidi. Naomba Ofisi yako imwagize *CAG* akague manunuvi ya mbolea ya shilingi bilioni 10 yaliyofanywa na kusambazwa katika msimu huu na taarifa hiyo uweze kuifanya kazi, kwa sababu kuna shilingi 15,000 zimeongezwa kwenye mbolea zote zilizonunuliwa ile ya *DAP* na ile nyingine ya kukuzia. Kwa hiyo, naomba jambo hilo uweze kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu ibara ya 17 ameongea maneno mazuri sana kwamba tufanye siasa na naomba nimnukuu, ni maneno mazuri sana, anasema; "Ninatoa rai kwa wadau wa siasa kote nchini kujenga utamaduni wa masikilizano na kuendesha siasa za maendeleo badala ya siasa za malumbano; siasa za kuunganisha watu wetu badala ya kuwagawa; na siasa za uwajibikaji badala ya siasa za mazoea."

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu mmetufungia kufanya siasa. Tunafanyaje siasa za kuwaunganisha watu wakati hatufanyi mikutano ya hadhara? Tunafanyaje siasa za maendeleo wakati hatufanyi mikutano ya hadhara? Tunafanyaje siasa za uwajibikaji wakati hatufanyi mikutano ya hadhara na mnafahamu kabisa kwamba ni kinyume cha Katiba. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Waziri ambaye unahuksika na suala la vyama vya siasa umshauri Rais. (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Riziki Said Lulida ajiandae Mheshimiwa Koshuma, Mheshimiwa Mgimwa na Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia afya njema na kuwepo katika kuchangia hii hoja ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Dkt. Macha ambaye Mwenyezi Mungu amempenda zaidi. Kwa muda mfupi niliokaa na Mheshimiwa Dkt. Macha nimejifunza vitu vingi sana na nikikaa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu huwa nawaambia Mama Macha alikuwa na kipaji maalum kwa walemovu hasa. Hivyo Mwenyezi Mungu amrehemu amuweke katika njia iliyokuwa sahihi na ampe pepo.

### **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda nitoe pongezi za dhati kwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu ni mtu mnyenyekevu, huruma, na mwenye upole. Nataka nimpe usia mmoja kama ndugu yangu, tulichukua Qurani na Biblia tukasema tutatenda haki kwa Watanzania. Nina imani kwa unyenyekevu na upole wake atawatendea haki Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania sasa hivi tunasimama kutaka kutatua migogoro ya Burundi, tunaiacha Zanzibar iko katika mgogoro, Zanzibar ni mwiba. Mwiba ule kwa unyenyekevu kabisa, nakuomba Waziri Mkuu uliapa kutenda haki na kuwatetea Watanzania, basi lile unaloliona wewe litakuwa haki ulisimamie kwa vile Qurani hii itakuja kutuadhibu siku moja. Qurani na Biblia zetu hizi zitakuja kutuadhibu siku moja tutende haki kwa waislam, wakristo na wote wanaopenda haki katika Tanzania hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nataka nimshukuru tena Waziri Mkuu, nilitoa hoja ya kumuomba Waziri Mkuu ashughulikie suala la korosho kuhusiana na tozo. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu nikiwakilisha wananchi wa Mtwara, Lindi na walima korosho wote kwamba ameweza kulitatua tatizo lile kwa asilimia kubwa sana, sasa hivi tuko katika neema. Neema hii tunaomba iende katika mazao ya tumbaku, pamba na kahawa. Naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu una uwezo mkubwa, ahsante sana na Mwenyezi Mungu atakujalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka katika Mkoa wa Lindi. Mkoa wa Lindi ni wa mwisho katika maendeleo lakini ni wa kwanza kwa kuwa na *resource* nzuri, lakini bado keki ya kugawiwa Lindi inapelekwa ndogo sana. Nataka niongelee tatizo la maji Lindi na ni karibu miaka 10 tunazungumzia, leo Manispaa ya Lindi imetumia shilingi bilioni 51 lakini hakuna maji. Hata hivyo, nataka nitoe sababu ya msingi inayosababisha miradi ya maji kufeli. Tunawapa wakandarasi kutoka India na hela zinapelekwa shilingi bilioni 51, mkopo wa Watanzania, mkopo wa walipa kodi, kwa

nini zipelekwe India? Tunaagalia mradi wa maji wa Chalinze, shilingi bilioni 51 hela zote kunapelekwa katika Benki ya India sio *Bank of Tanzania*. Tujiulize, maji hakuna tayari mabilioni yanakwenda India, kwa faida ya nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu ana meno na macho ya kuangalia, nashauri akaangalie hili suala la maji Tanzania nzima. Kila ukija humu ndani watu wanalamikia maji lakini mabilioni ya pesa ya maji yamepotea kwa ajili ya wazembe wachache ambao wamefanya wanawake wanatoboka utosi kwa ajili ya kutafuta maji kisa wao wananaufaika na kuzichukua zile pesa kuzipeleka India. Inakuwaje mkopo wa *World Bank* unachukua pesa za Mtanzania, zinawekwa Benki ya India na sisi wenyewe tumenyamaza? Cha kushangaza miradi hii yote wamepewa Wahindi, kuna *syndicate* hapa. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kabla hujamaliza kuhitimisha uandae Tume ujiulize ni akaunti ngapi za maji zimepelekwa nje? Akaunti ngapi za ujenzi wa barabara zimepelekwa nje na kwa faida ya nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa Lindi mpaka leo haujafika hata shilingi bilioni mbili lakini tayari shilingi bilioni 51, nilikuwa Mjumbe wa Bodi ya Maji, alipewa *MS Jandu* shilingi bilioni 13.7 maji hayakupatikana Lindi. Akapewa tena shilingi bilioni 16 maji hayakupatikana Lindi. Amepewa shilingi bilioni 29 maji Lindi hamna. Je, hizi hela za walipa kodi tunazifanya nini? Ni madeni ambayo yangeweza kuzuilika lakini haiwezekani kutokana na watu wachache wanaifanya hii nchi isitawalike. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia uhifadhi wa wanyamapor. Mimi ni mdau wa wanyamapor, ni Mwenyekiti wa Kupambana na Ujangili. Kwa idhini yako, nataka nimuombe ahakikishe mpaka wa Gorogonja ambao unaunganisha Serengeti na Masai Mara usifunguliwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Waheshimiwa Wabunge wengi hawaelewii ni wapya, nashauri wapewe

### *NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

semina wajue kwa nini mpaka wa Gorogonja usifunguliwe. Mtalii akija Tanzania atarudi kwenda kulala Kenya, uchumi wote utapelekwa Kenya. Ni lazima tuhakikishe kuwa tunajitambua kuwa ule mpaka ni sumu kwa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mzigo muda mrefu nataka niutue, lakini leo nataka nimtulie Waziri Mkuu mzigo huu. Mjusi ameanza na Mheshimiwa Mudhihir akashindwa mahali pa kuupeleka yule mjusi. Akaja Mheshimiwa Mama Mikidadi na Mheshimiwa Riziki, *dinosaur* ambaye yuko Ujerumani nimeshindwa kulitua. Hapa simtulii Mnyamwezi wala Mndengereko mzigo huu namtulia Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yanayopatikana na *dinosaurs* yule ni makubwa sio ya kubeza ndani ya Bunge hilli. Leo watu wa Lindi hatuna mirahaba ya *TANAPA*, hatupati tozo yoyote ya Ngorongoro lakini tungepata pato la mjusi, shule za Mipingo, Matakwa, Namapwia, tungepata barabara, tunajuliza kigugumizi kiko wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema tena, sitamuuliza swalii hili Mheshimiwa Maghembe, nitauliza Ofisi ya Waziri Mkuu mpaka Mwenyezi Mungu aniondoe katika Bunge hilli, suala la mjusi limefikia wapi? Naomba suala la mjusi huyu ulipokee wewe na unijibu wewe siyo mtu mwininge tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja tena katika masuala ya uwiano wa maendeleo katika Mikoa ya Kusini, Lindi na Mtwara. Mradi ambao ni mwiba katika Mkoa wa Lindi ni huu Mradi wa *TASAF*. Bahati nzuri nilimpelekea *document* kuonesha shule zilizojengwa Lindi ziko chini ya viwango, hospitali zilizojengwa Lindi ziko chini ya viwango, vyoo vilivyojengwa Lindi viko chini ya viwango, maji yaliyopelekwa Lindi hayapatikani, yote ilikuwa ni miradi ya *TASAF*, lakini nataka nitoe sababu na yeye kwa vile yuko humu ndani akalisimamie, tuko pamoja kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya viongozi wamekuwa miungu watu ndani ya Wilaya zetu, hawa wanaitwa Makatibu na Wenyeviti. Wale wanawatisha Madiwani wasifanye kazi zao, wasikague miradi, matokeo yake nafikiri umeona. Choo cha *TASAF* kimejengwa kwa karibu shilingi milioni 100 hakuna choo. Darasa limejengwa limeshaanguka. Je, tutaendelea na *TASAF* !!! wakati *TASAF* /...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Haya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Waitara.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulitolewa mwongozo hapa juzi na Kiti kikaamua kwamba tunapochangia hapa tunam-*address* Waziri Mkuu na hii ni hotuba yake. Katibu wa CCM, Mheshimiwa Ulega amehama kwake karibu saa nzima yupo pale, Mheshimiwa Mama Riziki analazimisha Waziri Mkuu amsikilize lakini hasikilizi anampigisha *story*.

**MWENYEKITI:** Mbona mimi sioni mtu hapa?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waziri Mkuu asikilize ili aweze kujibu hoja. Ni hilo tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, mimi sioni mtu hapa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Kiti hakijaona mtu. Endelea Mheshimiwa Lulida.

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

**MWENYEKITI:** Kaa chini wewe.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniongezee muda wangu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu mjisui namhamisha kutoka kwa Mheshimiwa Riziki, Mheshimiwa Bobali, nakukabidhi tupate mapato na tozo liende Namapwiya, Mipingo na Nangaro. Wakati Mheshimiwa Rais anakuja Nangaro alisema atatuletea mapato katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nashukuru na nawapenda Watanzania wote, Mungu ibariki Tanzania na Mungu mbariki Waziri Mkuu. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Koshuma. Wajiandae Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Aeshi Hilaly na Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pia naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameweza kunijalia afya njema ili niweze kuendelea kutoa michango yangu katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kuongelea suala zima la uvezeshaji wananchi kiuchumi. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 15 ameongelea suala la uvezeshaji wanawake kiuchumi na ukisoma pale ndani ameandika kuhusiana na maendeleo ya wanawake kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake wa mwaka 2007 ambao unalenga kuwawezesha wanawake kiuchumi ili waweze kukopesheka. Lakini kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 Mfuko huu wa Maendeleo ya Wanawake haukutengewa fedha zozote. Naomba niiombe Serikali itusaidie kutenga fedha kwa ajili ya kuuwezesha huu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ili wanawake waweze kukopesheka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa nina kikao na wanawake wa Mkoa wa Mwanza, kwa kweli swali zito ambalo nilikumbana nalo ni huu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Wanauliza Mfuko huu wa Maendeleo ya Wanawake unawasaidiaje wanawake ili waweze kujishughulisha na masuala mazima ya uchumi? Ukiangalia wanawake wengi wa Mkoa wa Mwanza wanajishughulisha na shughuli mbalimbali kama vile mama lishe hata wamachinga pia wapo amba ni wanawake lakini kama Mfuko huu wa Wanawake usipotengewa fedha, ni jinsi gani wanawake wataweza kujkwamua kiuchumi? Hivyo, naomba sana katika bajeti ya Waziri Mkuu basi suala hili la wanawake liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika mataifa makubwa duniani na hata yale ya nchi jirani kama vile Zimbabwe, Malawi na Msumbiji na nchi nydingine hata Kenya tu hapo jirani, wamekuwa wakiliangalia suala zima la wanawake katika kutenga bajeti. Ukiangalia hapa Tanzania katika bajeti zote ambazo zimekuwa zikitengwa suala la mwanamke limekuwa liki-*lag behind*. Unakuta mwanamke anatajwa katika maeneo machache sana. Sisi wanawake tumeamua sasa kuiambia Serikali, lakini kuiomba kwa unyenyekevu mkubwa sana kwamba sasa ianze kuangalia suala zima linalowahuwanawake. Kwa sababu wanawake ndio amba wanachangia katika pato la Taifa na hivyo basi naomba wasiachwe nyuma. Hivyo basi, naendelea kuisihi Serikali yangu kuuangalia mfuko huu na kuweza kutenga fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Wizara hii ya Afya inayoshughulika na wanawake, huyu mama ambaye ndio ameshikilia hii Wizara, dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu, tunapomuweka kuwa yeye ndio mshika dhamana ya wanawake hapa Tanzania halafu mfuko ule haujtengewa fedha, ina maana tunamdhooifsha huyu dada katika kuisimamia hii Wizara ya wanawake. Kwa hiyo, naendelea kusisitiza na kuiomba Serikali, kwa mwaka huu wa fedha iweze kutoa fedha na kuweka kwenye mfuko ule ili kuweza kuwasaidia wanawake kwenye VICOBA ambavyo

## *NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

wamevianzisha waweze kujikopesha na kuweza kujikwamua kiuchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee suala la afya. Katika hotuba ya Waziri Mkuu ukiangalia ameongelea suala zima la afya na amesisitiza kwa kusema kwamba Serikali inaendelea kujenga vituo vya afya ili kuhakikisha wanawake nchini wanapata huduma za kiafya vizuri. Ukiangalia katika afya kuna *pillarstatu*, yaani zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali za Wilaya. Kule ndiko ambako zile *basic needs* za afya zinaanzia. Katika Mkoa wa Mwanza tunavyo vituo vya afya vya Serikali 46 tu ukiunganisha na vituo vingine vya binafsi jumla ni vituo 388.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hivi vituo 46 va Serikali ni vituo vinne tu katika mkoa wa Mwanza ndivyo ambavyo vinatoa huduma ya upasauji. Wanawake wengi wamekuwa wakipoteza maisha wakati wa kuleta watoto hapa duniani. Ukiangalia idadi ya vifo vya akina mama Mkoa wa Mwanza ni 21% na hiyo inatokana na kukosa huduma za upasauji katika vituo vyetu vya afya. Hivyo basi, naomba Serikali iweze kutusaidia katika Mkoa wa Mwanza kuwezesha kutupa vituo vya afya ambavyo vinaweza vikatoa huduma za afya ili viweze kuongezeka kutoka vituo vinne tufikie hata vituo 15 kwa kuanzia ili wanawake wasiweze kuendelea kupoteza maisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika *Sustainable Development Goals, goal* mojawapo ni kuhakikisha huduma za mama na mtoto na za wajawazito zinapatikana kwa urahisi na kuendelea kuondoa vile vifo vya mama na mtoto. Kwa hiyo, kama tumeingia mkataba huu wa kwenye *Sustainable Development Goals*, naomba Serikali iweze kutusaidia katika Mkoa wa Mwanza kutuboreshea vituo vyetu vya afya ili viweze kutoa huduma ya upasauji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka siku moja hapa nilipokuwa nikiuliza swalı langu la nyongeza niliuliza suala la wanawake wanavyopata huduma za upasauji lakini hawapati huduma za upasauji kwa kupangiwa. Nilipokuwa

naongea kile kitu nafahamu kwa sababu mama anapopata ujauzito kuna matatizo ambayo huwa yanaonekana kwenye *scan* kabla hata muda wake wa kujifungua haujafika. Kwa hiyo, kama tatizo limeshaonekana na kwenye kituo cha afya kuna huduma ya upasuaji, mama huyu anatakiwa apangiwe ni lini na siku gani atakayofanyiwa upasuaji ili kuweza kuokoa maisha yake ye ye kama mama lakini pia na maisha ya mtoto yule ambaye anamleta duniani. Kina mama wengi sana wamekuwa wakipoteza maisha yao lakini mtoto anabaki kwa sababu ya kutoa damu nyingi na matatizo mengine mbalimbali ambayo yanawakumba akina mama wakati wa kujifungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika hotuba ya Waziri Mkuu wameeleza ni namna gani bajeti ya vifaa tiba pamoja na dawa imeongezeka kutoka shilingi bilioni 31 hadi shilingi billioni 251. Katika kuongezeka kule sisi Mkoa wa Mwanza naiomba tu Serikali katika bajeti hii ya mwaka huu iweze kutusaidia *CT Scan*, Mkoa wa Mwanza hatuna *CT Scan*. Ukiangalia *CT Scan* inasaidia katika mambo mengi sana si tu wanawake. Kuna watoto wanazaliwa kule na vichwa vikubwa Mkoa wa Mwanza lakini na Kanda ya Ziwa kwa ujumla...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, ajiandae Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dkt. John Pombe Magufuli, lakini kwa namna ya

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

kipekee, naomba nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake. Pia niwapongeze ndugu yangu Waziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitauelekeza katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kuwawezesha wananchi kiuchumi. Katika kampeni yetu ya uchaguzi ya mwaka 2015, Ilani ya Chama cha Mapinduzi tuliahidi kupelea shilingi milioni 50 kwenye kila kijiji na kwenye kila Serikali ya Mtaa. Huu ni mwaka wa pili sasa toka tulipotoa ahadi ile. Ni vyema tukatekeleza ile ahadi. Tumebakia na mwaka mmoja tu wa kufanya kazi, mwaka 2018, 2019 tutaenda kwenye uchaguzi, tusipotimiza ahadi ambazo tumeziahidi wenyewe itakuwa vigumu sana mwaka 2019 kuomba kura hasa kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakuomba, kuitia kwenye Serikali yetu ya Chama chetu cha Mapinduzi tutekeleze ahadi hii muhimu kwa sababu wananchi waliokuwa wengi kule vijijini na kule kwenye Serikali zetu za mtaa walikuwa wanategemea wapate shilingi milioni 50 hizi kusudi ziweze kuwatoa kwenye *stage moja* kwenda kwenye *stage* nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka kuchangia ni suala la kilimo. Watanzania kati ya 67% mpaka 70% wameajiriwa katika eneo hili. Tumekusudia kwenda kwenye uchumi wa viwanda, lakini hawa wananchi ambaao wameajiriwa kwenye eneo hili hatuwapi *facilities* za kutosha. Ukiangalia pembejeo sasa hivi ni ghali sana kuliko siku za nyuma. Kwa hiyo, ule uchumi wa viwanda ambaao tumekusudia kwenda utakuwa mgumu sana kwa sababu malighafi ambazo tumekusudia kuzipata hatutazipata kwa sababu wakulima hawa watakuwa hawana uwezo wa kulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie sana hili eneo la

pembejeo hasa mbolea kwa wakulima wetu zisiendelee kupanda bei. Mheshimiwa Waziri Mwigulu kipindi kilichopita alituahidi kwamba mbolea itauzwa bei rahisi, itauzwa kama soda, lakini haya yaliyokuwa tumeahidiwa hayafanyiki na hatuyaoni. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iliangalie sana eneo hili. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili hili la kilimo Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna hawa wenzetu mawakala wa pembejeo ambao wanaidai Serikali takribani shilingi bilioni 68. Huu ni mwaka wa nne wanadai hela zao na hawajalipwa mpaka leo. Kuna baadhi ya watu wameshaanza kuuziwa nyumba zao na wengine wanakufa. Kwa hiyo, tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atengeneze utaratibu wa kuhakikisha hawa watu wanaodaiwa hela zao katika maeneo haya wanalipwa baada ya kuwa wamehakikiwa vizuri. Kuendelea kuwaacha na madeni, watakuwa na hali zao zitaendelea kuwa mbaya. Serikali yetu ni sikivu, nina uhakika hawa watu watalipwa hela zao haraka iwezekanavyo baada ya uhakiki. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuchangia ni suala la maji. Maji ni tatizo kubwa na kule kwenye jumbo langu kuna tatizo kubwa sana la maji. Cha kusikitisha ni kwamba tatizo hili limekuwa kubwa na linaendelea kuwa kubwa siku baada ya siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa ya Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali. Mwaka jana katika mambo mengi ambayo sisi Wabunge tulishauri Serikali kwenye bajeti iliopita hayakutekelezwa likiwepo la kuongeza tozo ya kutoka shilingi 50 kwenda shilingi 100. Tulikuwa na uhakika kama tungeweza kuongeza tozo kwenye eneo hili Mfuko wa Maji ungeendelea kuwa mkubwa na hatimaye watu wengi wangepata huduma ya maji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana kupitia Waziri Mkuu, muwe mnatusikiliza na sisi Wabunge. Hakuna Mbunge ambaye anataka kero ya maji iwepo katika maeneo yake. Kwa hiyo, tunaomba sana Waziri Mkuu kwenye

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

jambo hili atusikilize na sisi Wabunge. Sisi Wabunge wenyewe tumekubali kwamba ile shilingi 50 iende kwenye shilingi 100 na tutatolea majibu kwa wananchi kwa nini tumeamua kuongeza tozo katika eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka kuchangia katika sehemu ya maji ni kwamba katika Jimbo langu la Mufindi Kaskazini kuna vyanzo vikubwa viwili nya maji. Katika Tarafa ya Sadani kuna vyanzo nya maji nya Mto Kihata. Hili eneo linahitaji shilingi bilioni mbili tu ili eneo hili liweze kusaidia kutoa maji katika vijiji 19. Tumeshaleta maombi mara kwa mara katika Wizara ya Maji lakini mpaka leo halijashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine la pili ni Tarafa ya Ifwagi. Tuna taasisi ya *RDO* ya watu binafsi imetusaidla kutoa maji kwa kata takribani tano na wanalisha vijiji takribani 30. Serikali hajatia mkono wake wowote katika eneo hili. Ni wakati umefika sasa kwa Serikali yetu kutia mkono. Kwa masikitiko makubwa kwenye eneo hili inafika wakati hawa wanatozwa *VAT*, kwa hiyo, badala ya kuwapa moyo wanakosa moyo wa kushughulikia eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni barabara. Tuna barabara kubwa mbili katika Jimbo langu la Mufindi Kaskazini ambazo nataka mziangalie kwa macho mawili. Barabara moja ni kutoka Kinambo A – Isalavanu – Saadani - Madibila - Lujewa. Mwaka 2010 na 2015 barabara hii iliingia kwenye llani ya uchaguzi, kwa maana ya vipindi vyote vitano imeingia kwenye llani ya Uchaguzi lakini hata kilometa moja hajawahi kutengenezwa. Kwa hiyo, tunakosa majibu ya kuwajibu wananchi kwenye maeneo yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamuomba sana Waziri Mkuu kwenye jambo hili aliangalie. Nakuomba Waziri Mkuu ufanye ziara katika Wilaya ya Mufindi kwa sababu hakuna kiongozi yejote wa kitaifa ambaye amekuja katika Wilaya ya Mufindi kujiona hali halisi. Nataka nikuambie mionganoni mwa maeneo ambayo tunapata kura nyingi CCM ni Wilaya

ya Mufindi. Wananchi wa Wilaya ya Mufindi wasije wakakata tamaa kwa sababu yale mambo ambayo tumeyaahidi hayafanyiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine tulilokuwa tunaomba mtusaidie ni barabara ya kutoka *Johns Corner - Mgololo* na barabara ya kutoka *Mchili - Ifwagi - Mdabulo - Ihanu - Tazara - Mlimba*. Barabara hii inaunganisha Wilaya mbili na mikoa miwili. Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi haina uwezo wa kuitengeneza barabara hii.

Kwa hiyo, tunaomba sana ipandishwe hadhi na tumejitahidi kadri ya uwezo wetu kupeleka barua kupitia kwenye *Road Board* ya Mkao, lakini kwa bahati mbaya mpaka leo Waziri mhusika hajawahi kutujibu kwenye eneo hili. (*Makof*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Aeshi, ajandae Mheshimiwa Chumi.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi na uwajibikaji mzuri na kila Mbunge ndani Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anakuamini kwa asilimia mia kwa kazi kubwa na nzuri unayoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia maeneo machache sana katika bajeti hii na kwanza, ni suala la maji. Ndani ya Mji wa Sumbawanga Mjini tuna mradi mkubwa sana wa maji ambaao napenda sana kwa niaba ya wananchi niwashukuruni sana kwa mradi ule. Sumbawanga sio mji peke yake pale mjini, Sumbawanga imezungukwa na vijiji vingi

sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu mliangalie hili, mtusaidie kupata fedha za kuwezesha miradi ile midogo midogo ili wananchi wanaozunguka Mji wa Sumbawanga waweze kupata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni la wafanyabiashara. Nataka kuongelea sana wafanyabiashara hususan wa Jimbo la Sumbawanga Mjini wengi ni wakandarasi na wengi wamefanya kazi ndani ya Serikali, lakini ni muda mrefu sana hawajapata malipo yao. Hao watu wanaumia sana kwa sababu wanadaiwa kodi, kwenye mabenki na kwenye maeneo mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo linanishangaza Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeunda kamati kila Mkoa ya kudai madeni ya wafanyabiashara ambao hawajalipa kodi. Kamati hiyo wameandika barua sehemu mbalimbali pamoja na kuzuia fedha ambazo wakandarasi wamefanya kazi Manispaa au taasisi nyingine, wakizua fedha zile zote hawa watu wanakwama. Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu hili suala la kamati ambazo mmeziunda mikoani ziongozwe na watu wa *TRA* kwa sababu wao ni wataalam na wamesomea kazi hiyo. Nilikuwa nataka nizungumzie hili ili mliangalie kwa uzito wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pembejeo, wameongea Wabunge wengi na jana nimekusikiliza ukiongea na hawa mawakala wa pembejeo na umeahidi kwamba ifikapo tarehe 26 *at least* wachache watakuwa wameshaanza kulipwa wale ambao wamehakikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaumiza sana, watu hawa wamekopa kwenye mabenki na watu hawa kama mnakumbuka, nataka niweke kumbukumbu sawa wafanyabiashara au mawakala wakubwa walikataa kuikopesha Serikali. Wafanyabiashara wadogo wadogo hao wakaenda kukopa fedha benki wakaenda ku-supply pembejeo na bahati nzuri tukapita kwenye uchaguzi vizuri sana, lakini baada ya uchaguzi kupita hawa watu hatujawakumbuka.

Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi wana imani kubwa sana na Serikali hii, liangalieni hili kwa jicho lingine watu wanaumia sana, watu wamekufa, watu wana presha na wengine wamejinyonga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni la kusikitisha, mwaka jana kwenye bajeti wakati tunapitisha hapa masuala ya pembejeo na kutoa ruzuku kwenye mbolea tukaichagua *TFC* iwe mwakilishi wetu. *TFC* ndiyo wamekuwa walangazi wakubwa. Mheshimiwa Zitto amechangia hapa amesema umtume *CAG*, nikuombe kabla hujamtuma *CAG* msimamishe huyu Mkurugenzi wa *TFC* ana miaka 20 yupo pale, ana kampuni binafsi ya kwake. Mheshimiwa Waziri Mkuu nikuombe sana kabla hujamtuma *CAG* kwenda kuhakiki au kuchunguza, kwanza huyu Mkurugenzi wa *TFC* mumsimamishe kazi. Jana mmemsimamisha mmoja, lakini huyu ni wa pili ili akae pembeni uchunguzi ufanyike. Nikuombe sana na naamini hili unaliskia ulichukulie kwa uzito wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni uwanja wa ndege. Uwanja wa ndege tumepata bajeti, tumeshatafuta mwekezaji, uwanja wa ndege utajengwa ndani ya Mji wa Sumbawanga Mjini, shida kubwa nayoiona ni wale wananchi wanaouzunguka uwanja wa ndege. Wale wananchi wanaouzunguka uwanja ule walifanyiwa tathmini miaka sita au saba iliyopita, gharama za ujenzi zimeongezeka na gharama za viwanja zimeongezeka. Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Simbachawene yuko hapa kwa sababu wanaotakiwa kuwalipa fidia sio Idara ya Ujenzi, hapana, wanotakiwa kuwalipa fidia wananchi ni sisi TAMISEMI kuititia Manispaa. Naomba tufanye tathmini upya kulingana na wakati uliopo. Nafikiri hili Mheshimiwa utakuwa umelichukua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kuhusiana na umeme. Sumbawanga Mjini tumebahatika tuna umeme na hatuna mgao wowote lakini Sumbawanga imezungukwa na vijiji mbalimbali. Kwa bahati nzuri vijiji vingine vyote vimepata umeme tatizo kubwa ambalo naliona na nilishamwambia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na ameahidi

kunisaidia ni vijiji ambavyo vinatoka nje ya barabara kilometra tano kutoka barabarani, wale watu hawakubahatika kupata umeme. Hata hivyo, kwenye *REA* /// nimeona baadhi ya vijiji vipo na niishukuru sana Serikali katika hilo. Niombe tu Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini naye aje azindue mradi huo wa *REA* /// ndani ya Jimbo la Sumbawanga Mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka kuongelea kuhusiana na minara ya simu. Minara hii ya simu ni michache sana. Yapo baadhi ya maeneo hayana kabisa *network*. Niwaombe Wizara inayohusika na jambo hili lichukulie kwa uangalifu mkubwa na kwa nguvu kubwa kuhakikisha sasa Tanzania nzima inafikika na Tanzania nzima mawasiliano yanapatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika hili hili ni kuomba tu Serikali iwekeze *TTCL*, iache maeneo mengine iongeze nguvu *TTCL* ili na yenye we iwe kama kampuni nyingine tulizonazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mengi ya kuongea lakini mengine nimeamua kuyaacha kwa sababu maalum. Nimalizie tu na suala la *Bunge Sport Club*. Mheshimiwa Waziri Mkuu ulikua kocha wetu. Kwenye bajeti ya mwaka huu tumeona mmetujali kidogo lakini ikumbukwe sisi tuna ugeni mwaka huu kwa sababu sisi ni wenyeji wa mashindano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiki, nikuombe sana bajeti tuliyonayo japoikuwa mmetuongeza haitutoshi kulingana na ugeni mkubwa ambao tutakuwa tumeupokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama taifa tusiingie aibu. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu uliangalie hili kwa sababu wewe ulikuwa kocha wetu. Mashindano yakianza tutakuomba rasmi uombe likizo kidogo uwe kocha ili tuweze kuchukua kikombe kwa sababu kidogo tumeshuka kiwango baada ya wewe kutoka ndani ya mashindano haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba kuna mengine nimeyaacha lakini kuna kitu ambacho kinaniuma lazima nikiseme. Mimi ni mionganoni mwa watu walotishwa tena mimi sikutishwa kwa maneno nimemuona yeye mwenyewe, nimekutana naye uso kwa uso *vis a vis*, akiniambia...

**MBUNGE FULANI:** Nani?

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Nitamtaja mwisho. Akiniambia kwamba Wabunge mmezidi unafiki na baya zaidi maneno haya ameyatamka mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni. Alisema hivi; "Wabunge mmezidi unafiki na nita-deal na nyie nikianza na wewe."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo Dar es Salaam sikanyagi na nalogopa yaani nilikuwa nlmei-*miss* mno lakini baada ya kutishwa nimeogopa inabidi nikae Dodoma na Sumbawanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niliarifu Bunge na familia yangu ijue kwamba Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam mionganoni mwa watu wanaowatisha watu ikiwa ni pamoa na nini. Mengine mabaya siyasemi wala mazuri yake siyasemi nasemea hilli kwa usalama wa nafsi yangu. Najua yapo mazuri aliyoafanya na yapo mabaya aliyoafanya, lakini mimi naomba niseme hilo moja tu kwamba ni bora tukaliangalia kwa makini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo tayari kuhojiwa, nipo tayari kuja kusema na nitatoa ushahidi kwa sababu nilikuwa kwenye hoteli inaitwa Colosseum, niliitwa mbele ya Mkuu wa Wilaya na akanitisha. Sasa mimi sisemi mengi, naomba hilli niseme kulitaarifu Bunge kwamba na mimi ni mionganoni mwa watu ambao tunatafutwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi, wajiandae Mheshimiwa Benardetha Mushashu na Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa kupata nafasi na pia nipende kuwapongeza Mawaziri wanaofanya kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Jenista alifika mpaka kule Jimboni Mafinga akazungumza na wajasiriamali na akina mama kuhusu fursa mbalimbali zinazopatikana kuitia Baraza la Uwezeshaji, pia ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde hakuwa na ziara rasmi lakini alivyopita pale akasimama *stand akaongea* na vijana kuwatia moyo, kwa hiyo, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunajadili hotuba ya Waziri Mkuu ambayo ndani yake kuna Bunge, moja kwa moja nizungumzie kuhusiana na ufanisi wa ufanyaji kazi wa Bunge. Tumeshuhudia siku zilizopita badala ya kukutana wiki tatu tumekutana wiki mbili. Kwa mujibu wa Katiba, wajibu wa Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali na sehemu mojawapo ya kuisimamia ni kuitia tunavyokutana kwenye Kamati, lakini pia tunavyokagua miradi mbalimbali inayotekelizwa na Serikali. Niombe bajeti hii pamoja na jinsi ambavyo tumeambiwa imeongezwa, iliangalie Bunge katika namna ambayo italiwezesha kufanya kazi kwa ufanisi kwa mujibu wa Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aeshi amezungumza hapa kuhusu *Bunge Sports Club*, sisi tulioenda Mombasa kwenye mashindano ya Bunge tunajua kilichotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumechagua Wabunge wa *EALA* ni sehemu ya ushiriki wa Tanzania katika masuala mazima ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo suala la michezo. Tumekwenda kule kuna watu tulikuwa tunapanda kwenye karandinga, huu ni ukweli mpaka kuna watu wametuuliza ninyi ni Wabunge kweli maana *we were seen like a second citizen* wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niombe kwa nia ya kufanya kazi kwa ufanisi, tumeona hapa wakati wa kukagua miradi Wabunge wanasaifiri na *double coaster* zinaharibika njiani. Hata *security* yao, pamoja na kuwa wanakuwa na maaskari mle ndani lakini kuna *healthy security*, afya yao katika kusafiri kwenye mazingira ya magari ambayo *basically* yamejengwa kwa ajili kuwa *school bus* sio jambo jema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba ili Bunge lifanye kazi kwa ufanisi hebu kile kinachotengwa kipatikane. Kwa sababu sisi hatufanyi kwa kujipendekeza, tunafanya kazi kwa mujibu wa Katiba iliyowekwa. Naomba hilo tulitizame sana...

## **TAARIFA**

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilindie muda wangu.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mambo ya Wabunge, sisi kule kwetu Namanyere wananchi wangu wanasaifiri kwa shida sana wengine kwa mguu, wengine kwenye Noah na kwenye daladala wanasmama. Nashangaa Wabunge wanadai kuwa na hadhi kuliko watu wengine wa kawaida. Ndugu zangu tuwafikirie na wanakijiji kule kwetu majimboni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake sipokei kwa sababu naamini amepokea mkopo wa Bunge kwa ajili ya gari, hii siyo *luxury* ni ili kutuwezesha kufanya kazi kwa ufanisi, *that is my point. (Makofii)*

### **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu pembejeo. Wamezungumza Waheshimiwa hapa na kaka yangu Mgimwa amesema. Tumesikia kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amekutana na watu waliokopesha pembejeo, ni kweli matajiri wakubwa walikataa kuwahudumia wakulima wetu, wafanyabiashara wadogo wadogo wakajitokeza. Kwa hiyo, mimi niombe baada ya uhakiki watu hawa walipwe pesa zao. Kwa sababu ni kupitia kilimo watu wetu kwa mfano mimi kule Mafinga kuanzia Bumilainga mpaka Itimbo watu wale hawana shida, wewe wape mbolea tu ni wapiga kazi wazuri. Vijiji vyote Isalamanu na Kitelewasi watu wanalima mwaka mzima lakini wapete tu mbolea kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hawa ambao wamekopeshwa wapewe fedha zao kwa wakati ili kusudi wakati ujao waweze kuwa na moyo wa kushirikiana na Serikali katika kuwahudumia wananchi wetu. Kwa hiyo, niombe sana Ofisi zinazohusika, najua itakuja Wizara ya Kilimo tatalisemea, lakini suala la pembejeo ni suala linalogusa maisha ya watu. Kwanza, mbolea zifike kwa wakati kwa sababu msimu unajulikana. Sasa mbolea ya kupandia iende mwezi wa pili sio jambo zuri, wananchi wanaona kama tumewatelekeza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa nadhani wa 16 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu umezungumzia kuhusu kutenga maeneo kwa ajili ya biashara. Mimi niombe mamlaka zinazohusika, Halmashauri zetu kwa hali ilivyo baada ya kutoa ule utaratibu wa *retention* haziwezi kuwa na fedha kwa ajili ya kutenga maeneo, kwa sababu tunaposema kutenga haiishii tu kutenga ni pamoja na kuyapima maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuwa Halmashauri hazina nguvu hii tena tuje na utaratibu ambao tunaweza tukazisaidia, zikatenga maeneo yakapimwa yakajulikana haya ni maeneo ya biashara, haya ni maeneo ya wafanyabiashara wadogo wadogo na yakajengewa miundombinu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake amempongeza Alphonse Simbu, huyu ni mwana michezo. Sasa katika kutenga maeneo pia tuzisaidie Halmashauri zitenge maeneo kwa ajili ya michezo. Kwa sababu ni kupitia michezo vijana wanapata ajira na kupitia michezo tunapata akina Samatta na hawa akina Simbu. Bila kuwa na miundombinu kwa maana ya viwanja hatuwezi kufanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupitia michezo tumeona hapa utalii umeongezeka kwa asilimia 12 lakini kupitia michezo tunaweza tukafanya *promotion* kwa wepesi zaidi. Leo hii Simbu ameshinda *Mumbai Marathon* ni Wahindi wangapi India wameweza kuifahamu Tanzania? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba Halmashauri bado hazijawea kuwa na nguvu *especially* kama ya Mji wa Mafinga. Wananchi wamejita hidi wamejenga zahanati, juzi tunashukuru Ubalozi wa Japan umetusaidia tujenge *theatre*. Kwa hiyo, niombi Serikali kwenye Halmashauri kama hizi ambazo ni mpya na wananchi wamejenga maboma itie nguvu yake katika kuhakikisha kwamba zahanati zinakamilika. Vilevile kama ambavyo Serikali imefanya kwenye utaratibu wa kuwapata walimu wa sayansi na hesabu pia tuweke utaratibu na tupate vibali ili kusudi watumishi wa kada ya afya nao waweze kuongezwa katika maeneo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa haya yote tunayoyasema na kuyatekeleza na tutakayoyatekeleza yatafanikiwa tu ikiwa Serikali kwa macho mawili itaangalia *welfare* ya watumishi wa umma. Chochote tutakachofanya kama watumishi wa umma *morale* wako chini nadhani kwamba hatuwezi kufanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa tutazungumza kwenye Wizara husika lakini Serikali iangalie kama wamepata *promotion*, waweze kulipwa zile haki zao zinazoendana na *promotion* zao na *welfare* yao kwa ujumla

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

watumishi wa umma. Kwa sababu hawa pamoja na rasilimali fedha ni watu muhimu kuhakikisha kwamba tumefanikisha mipango tullyoipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mushashu, ajiandae Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri pamoja na Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Antony Mavunde kwa kazi nzuri wanayofanya katika shughuli zao za kumsaidia Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Magufuli pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kazi nzuri mnayofanya. Ni mwaka mmoja tu tangu mmeingia madarakani lakini mambo mnayofanya ni mazuri sana, uchumi wa nchi hii umeendelea kuwa mzuri hadi sasa hivi viashiria vyote vya uchumi vinaonekana kwamba tunafanya vizuri sana kwenye uchumi. Pato la Taifa limeendelea kukua hadi sasa hivi linaendelea kukua kwa asilimia saba na mmeweza kuu-*contain* mfumuko wa bei ukaendelea kukaa kwenye tarakimu moja. Vilevile ni furaha ilioje niliposikia kwamba Tanzania iko katika ya nchi sita *the best in Africa* ambao uchumi wao unakuwa kwa kiasi kikubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mengi ya kujivunia, tumeambiwa *TRA* sasa hivi makusanyo yameongezeka kutoka kwenye shilingi bilioni 850 mpaka kwenye shilingi trilioni 1.2 ndiyo maana mmeweza kuyafanya mambo makubwa kama kununua ndege. Anayependa apende, asiyetaka asitake lakini makubwa yanafanyika ndani ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Mmeweza kuwa mnapeleka shilingi bilioni 18.77 kwenye shule kwa ajili ya elimu bure kila mwezi, hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia kwamba mabenki yako salama, mitaji na ukwasi upo wa kutosha. Hapa nina wasiwasi kidogo kwa sababu tukienda kule chini, tukienda mijini na vijijini tunaona kwamba mabenki ya biashara yamepunguza kutoa mikopo. Tunahamasisha wajasiriamali wengi wajitokeze wafanye shughuli mbalimbali, wafanye shughuli za kilimo, biashara ndogo ndogo, tunahamasisha wananchi waanzishe viwanda vidogo na vikubwa, hivi kama mabenki hayatoi mikopo hawa mitaji watapata wapi? Niombe Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie ili Serikali sasa iweke mpango wa makusudi wa kuziwezesha hizi benki ili zianze kutoa mikopo kama walivyokuwa wanatoa kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wadogo waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita kwenye suala la kahawa. Kahawa ni zao la muhimu sana katika nchi yetu ya Tanzania, lakini lina umuhimu wa pekee kwa sababu tunaliuza nje linatuletea fedha za kigeni. Bei ya kahawa imeendelea kuwa chini kiasi ambacho inakatisha tamaa na ukilinganisha bei ya kahawa ya Tanzania na nchi jirani ya Uganda unakuta bei ya kahawa ya Uganda iko juu pamoja na kwamba nchi hizi zimepakanana, ndiyo kitu kinachoshawishi watu wauze kahawa ya magendo kuitoa Tanzania kuipeleka Uganda. Bei ya kahawa kuwa chini ni kwa sababu bei ya kahawa ya Tanzania imegubikwa na tozo nyngi, ada nyngi, kodi nyngi. Wataalam wanasema hizi kodi na tozo zinafikia hadi 26. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, kuna kodi na tozo za zimamoto, *OSHA, land rent, crop cess* pamoja na kwamba sheria inasema *crop cess* inaweza kuwa kati ya asilimia tatu mpaka tano, sisi halmashauri zinatoza *maximum, five percent*. Kuna *income tax, cooperate tax, VAT* kwenye *inputs* zote zinazoingaia kwenye kahawa, *research cess, Coffee Development Fund* ambapo hela zinakatwa kwenye kila kilo, lakini sijawahi kuona huu mfuko unakwenda kumuendeleza au kuendeleza kilimo cha kahawa. Kuna *labour charge, service levy, property tax, coffee bags duties, coffee industry licence et cetera* mpaka zinafika 26. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo hizi ziko kwenye ngazi mbalimbali za uzalishaji pamoja na pale wanapouza nje. Ukienda pale mkulima anapouza kahawa kwenye chama cha msingi, kwenye chama kikuu cha ushirika, kule kwenye mnada Moshi ambapo wana-export kahawa kote kuna tozo kila mahali, lakini mzigo mzima anaubeba mkulima. Tozo hizi ndio zinasababisha bei ya kahawa inakuwa chini sana. Kwa msimu huu Mheshimiwa Waziri Mkuu, bei ya kahawa kwa Mkoa wa Kagera ni shilingi 1,300, mtu anatunza ule mbuni kwa miezi tisa anapalilia, anakatia na kadhalika lakini anakuja kuishia kupata kati ya shilingi 1,100 na shilingi 1,300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijilinganisha na nchi jirani ambazo ni washindani wetu katika hili zao la kahawa kama Ethiopia wao wanakata *0.04% kama exchange rate sale price*, Uganda wanakatwa *1% export levy*, Kenya wanakata 3% tu kwa ajilli ya cess, lakini Tanzania tuna *different cess's, licence fees, taxes* na tozo mbalimbali zinazofikia zaidi ya 26 na kuifanya hiyo bei iwe chini sana na kuwafanya wakulima wa kahawa wakate tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya mambo mazuri sana kwenye korosho, tumemuona. Ameweza kuifanya bei ya korosho ikapanda kutoka kwenye kilo moja shilingi 1,200 mpaka shilingi 3,800. Tumucombe chondechonde, mimi kama mwakilishi wa wakulima wa Mkoa wa Kagera na nyuma yangu wakiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Kagera, tunamuomba hebu aangalie kwenye hili zao la kahawa, watu wamelia ni kilio cha siku nyingi. Hebu aangalie tunatoa ada, tozo na fees gani ili kumwezesha huyu mkulima na yeye mwenyewe aweze kufaidi jasho lake aweze kupata bei ya juu ili angalau kilo moja isiteremke chini ya shilingi 3,000. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati namalizia, unakumbuka kwamba watu wa Mkoa wa Kagera na Mwanza wanafanya biashara na Uganda kwa kuititia Ziwa Victoria. Meli ya Mv. Bukoba ilizama, Victoria imezeeka inakarabatiwa kila kukicha lakini wafanyabiashara wanapata matatizo kwa sababu ili waweze kupeleka mazao yale ina...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Naomba na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kupata nafasi ya kusema machache kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini pia na Kamati ambazo ziliwasilisha maoni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na kwenye hiki kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 21. Waziri Mkuu ametoa takwimu za upatikanaji wa chakula kwa mwaka uliopita na akagusia kwamba mwaka huu kuna maeneo ambapo hali ya hewa haikuwa nzuri sana. Nilichokuwa nakitegemea hapa kidogo na nitoe ushauri ni kwamba kutokana na hali hiyo kutokuwa nzuri, kwanza nillitarajia nione hapa kama kuna akiba kiasi gani sasa ya chakula lakini tunakitumia kwa namna gani ku-control bei inayoendelea kupanda kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza jana Mwanza gunia la mahindi lilikuwa shilingi 125,000 na wakati kelele za uhaba wa chakula zinaanza gunia la mahindi lilikuwa shilingi 80,000. Hii maana yake ni nini? Kadri tunavyokwenda kuja kufikia mwezi wa kumi kama hakuna *mechanism* ya Serikali ku-control bei ya mahindi yatafika shilingi 160,000. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachozungumza hapa sio njaa, hatuzungumzi njaa tunazungumzia kwamba bei ya chakula inapanda kwa sababu Serikali ni kama hajachukua *position* yake ya ku-control bei ya chakula kwenye soko. Wakati tunazungumza wakati ule bei ya mchele ilikuwa shilingi 1,200 leo ni shilingi 2,500, Mwanza ni shilingi 1,800. Maeneo yote haya ninayoyazungumzia hawakulima kwa sababu mvua hazikuwepo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ombi langu Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama tunayo *stock* ya chakula kwenye *godowns*, Wizara ichukue *position* yake, chakula kingie kwenye masoko na bei elekezi itolewe ili kisiendelee kupanda, vinginevyo *purchasing power* ya wananchi inapungua. Wananchi kipato ni kilekile, chakula kinapanda, matokeo yake watajikuta hata hiyo shilingi 2,000 ya kula kwa siku inakosekana. Hilo ndiyo lilikuwa ombi langu kwenye huu ukurasa wa 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 25 amezungumzia kuhusu hekta 38,567 za wachimbaji wa madini. Tatizo langu mimi sio utengaji wa maeneo, nilimwambia Waziri wa Nishati na Madini, alikuja Geita akazungumza takwimu kubwa za kuwapa watu maeneo ya kuchimba. Nikamwambia tatizo kubwa lilloloko hapa wanaopewa ni walewale. Ukiingia kwenye *database* utamkuta Kanyasu huyu ana-*appear* kwenye karibu kila eneo dhahabu inapotokea wale ambao wanatakiwa kabisa wapewe maeneo haya hawapewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza na wewe tuna vikundi zaidi ya 100 Geita vimejiandikisha vinasubiri maeneo ya kuchimba havipewi, lakin ukienda kwenye takwimu za Wizara atakutajia kubwa ya watu ambao kimsingi ni walewale wachimbaji wakubwa ambao wanahama toka sehemu moja kwenda sehemu nytingine.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, ni ahadi yetu kwenye llani ya CCM, tutawapa watu maeneo ya kuchimba, lini? Huu ni mwaka wa pili sasa. Kama yapo tunaomba yaanze kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 28 limeongelewa suala la umeme. Geita kila siku umeme unakatika. Hivi ninavyozungumza na wewe umeme hakuna, unakatika zaidi ya mara nne. Nimezungumza na Waziri na Naibu Waziri, wana matengenezo ya kutoka Busisi kwenda Geita karibu miaka miwili hayaishi. Nataka kufahamu hili tatizo la umeme Geita linakwisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakinii hata hivyo, kuna maeneo tumepeleka umeme wa *REA* baada ya umeme wa *REA* kufika kazi imeisha, jirani akiomba umeme *TANESCO* hakuna vifaa. Ina maana *REA* peke yake ndiyo sasa inafanya kazi ya kusambaza umeme, *TANESCO* wenyewe hawana uwezo? Naomba sana eneo hili lifanyiwe kazi vizuri kwa sababu linakatisha tamaa, kama umeme umefika kijijini, kuna watu wanne wamepewa umeme, jirani hapewi umeme kwa sababu *TANESCO* hana vifaa, nadhani hapa kuna mipango mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la fao la kujitoa. Mimi natoka Geita na naomba Waheshimiwa Wabunge wote wanisikilize vizuri sana. Geita pale karibu nusu ya watu wanaofanya kazi pale Geita Mjini ni watumishi wa mgodi. Kinachotokea kwenye mgodi pale ni kwamba hakuna mwenye ajira ya kudumu. Kuna watu pale wanafanya kazi kwa mikataba ya miezi sita, miaka miwili, miaka mitatu. Anapofukuzwa kazi hawezi kupata kazi ya aina ile tena katika nchi hii, kuna wengi ni vibarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu wanafukuzwa kazi, kwa sababu kandarasi iliyokuwa imempa kazi mkataba wake umekwisha, imeondoka imekwenda *South Africa*. Akienda kufuata pesa zake *NSSF* anaambiwa hizo pesa hawezi kupewa mpaka afike umri uliolezwa. Mtu leo ana miaka 25 au 30 asubiri pesa hizi mpaka afikishe miaka 55 ndiyo aweze kulipwa na hana kazi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja ametoa hoja kwamba wapewe asilimia 25, hapana. Ziko kada ambazo wanaweza wakasubiri, ukimwambia mwalimu, polisi, daktari asubiri sawa. Pale mgodini kuna tabia *supervisor* akikuchukia anakу-blacklist, akiku-blacklist huwezi kuajiriwa mgodi wowote duniani. Sasa unakaa unasubiri hiyo pesa mpaka utakapofikisha miaka 60 unaendelea kuwa maskini kwa misingi gani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri, sekta ya madini iangaliwe kwa jicho tofauti. Kuna watu pale

wanaacha kazi kwa sababu ni wagonjwa. Mgodi ule hauchukui watu wagonjwa, ukitibiwa mara mbili unaumwa kifua wanakufukuza, Mheshimiwa Jenista unafahamu nilikuletea watu wanaumwa, walipokuwa vilema walifukuzwa kwenye kazi, wana miaka 25, 30 halafu wananyimwa zile pesa wanaambiwa wasubiri mpaka watakapozeeka, anazeeka hizo pesa aje atumie nani? Ushauri wangu ni kwamba sekta ya madini ichukuliwe kwa namna tofauti, hatuwezi kuwa na jibu moja kwenye maswali yote magumu, lazima tuliangalie hili suala tofauti. Kama tuna nia ya kuwekeza *NSSF* wana mitaji mikubwa waangalie sehemu nyngine, lakini haya maisha ya watu kwa pale Geita tutawafanya kuwa maskini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna gereza pale Geita Mjini, uwezo wake ni kuchukua watu 100 na zaidi, hivi sasa lina watu 800, sababu kubwa ni wachimbaji wadogo wadogo ambao wanatafuta pesa ndogo ndogo ya kula, akikamatwa anarundikwa pale. Kuna tatizo sasa hivi kwenye Jeshi la Polisi na watu wa Idara ya Sheria, kesi ya madai inageuzwa inakuwa jinai wanarundikwa mle, matokeo yake watu wanalala wamesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu Mheshimiwa Waziri Mkuu na nafikiri nilizungumza na wewe, pale kuna tatizo tuna *OC-CID* hafanyi kazi yake vizuri, kazi yake ni kukusanya pesa, anachokifanya yeye ni kuhakikisha kwamba kila anayetuhumiwa pale, iwe ni jinai, iwe ni *civil* lazima abambikwe kesi ambayo itamuweka magereza zaidi ya miezi mitatu, gereza limejaa. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe alikuja aliona, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ulikuja uliona, tunaomba mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna hizi kesi ndogo ndogo za kupita tu mgodini anakamatwa mtu anawekwa ndani miezi sita. Unapita tu na baiskeli unakamatwa unawekwa ndani miezi sita. Serikali ina pesa za kuchezea, kwa nini hizi pesa ambazo zinakwenda kulisha watu humo wasipewe hawa wanasheria wakapeleka hizi kesi haraka? Mimi nadhani kuna haja ya kuisaidia Wilaya ya Geita. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni uwepo wa migodi mingi sana kwenye Mkoa wa Geita na tatizo la huduma za afya. Wilaya ya Geita peke yake ina watu 800,000 kwa sensa ya mwaka 2012, lakini hospitali yetu iliyokuwa ya Wilaya tulii geuza kuwa ya Mkoa, matokeo yake hatuna tena Hospitali ya Wilaya. Sasa ufikirie *population* ya watu 800,000 wa Wilaya moja na ile hospitali imegeuka kuwa ya mkoa, watu milioni mbili matokeo yake ile hospitali imezidiwa kabisa uwezo. Tuna vituo viwili vya afya tumeanza kuvitengeneza, tunaomba *support* yako Mheshimiwa Waziri wa Afya, tunakushukuru ulitupa gari lakini hatuna madaktari. Daktari aliye po pale kuna *specialist* mmoja ambaye ni *surgeon* waliobaki wote ni *AMO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru sana Serikali, tulitaka kuleta muswada hapa wa kuwaondoa Madaktari Wasaidizi kwenye mfumo wa madaktari, lili kuwa ni kosa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule vijiji ni madaktari wetu ni ma-*AMO* na ndiyo wanaofanya kazi usiku na mchana. Ukiwaondoa wale kwenye mfumo wa madaktari waliobaki wengine wote ni mabosi wakienda kwenye wilaya kazi yao ni *research*, hawakai kwenye ofisi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi namuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu mtusaidie sana Hospitali yetu ya Mkoa wa Geita ianze ili Hospitali ya Wilaya irudishwe Wilayani ili gharama za matibabu ziweze kupungua. Hivi sasa navyozungumza na wewe gharama za matibabu ziko juu sana kwa sababu tunalipa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na wachangiaji waliopangwa muda huu wa mchana wametimia kwa uhakika.

Waheshimiwa Wabunge, tuna utaratibu wa mambo mahsusini yanayojadiliwa humu kwenda kwenye Kamati ya Bajeti. Naelekeza Kamati ya Bajeti kushughulikia suala la *TTCL* na wakae na Serikali, Wizara ya Mawasiliano, *TCRA* na wenyewe *TTCL*.

Waheshimiwa Wabunge, Ethiopia chombo cha simu kinakusanya *almost 1.7 billion dollars* kwa mwaka. Njia ya kuondokana na matatizo haya ya maji, barabara ni chombo chetu kipewe nafasi kubwa nchini kiweze kufanya kazi. Kwa maana hiyo, tutaiomba Kamati ya Bajeti baadaye na Wabunge wote wawe mabalozi wa *TTCL*. Sidhani kama Waheshimiwa Wabunge hapa wana kadi za *TTCL*. Lazima wote tuingie *TTCL* na tuhakikishe *by december subscribers* wa *TTCL* wako milioni 30 na Serikali iwekeze ili minara na umeme upatikane maeneo yote na *TTCL* iwe *number one Tanzania*.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo dogo, Wabunge wote wa CCM leo wanatakiwa kwenye *caucus* saa mbili baada tu ya Bunge kuahirishwa. Tangazo lingine, Waheshimiwa Wabunge wote wanatangaziwa kuhudhuria ibada katika *chapel* ili yopo Jengo la Pius Msekwa, ghorofa ya pili leo, leo siku ya Jumanne, tarehe 11 Aprili, 2017 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana. Aidha, wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma watahudhuria ibada hiyo. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, jioni mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Zubeda Sakuru, wa pili Mheshimiwa Joyce Mukya na wa tatu Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Mchangiaji wetu wa mwanzo jioni hii ni Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, jiandae Mheshimiwa Joyce Mukya na Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcemba ajiandae. Mheshimiwa Zubeda.

**MHE. ZUBEDA H. SAKURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii kujadili hotuba ya Waziri Mkuu katika kuitia mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka huu wa fedha wa 2017/2018. Pia nitoe pole kwa familia ya Mbunge mwenzetu Dkt. Elly Macha aliyesariki nchini Uingereza na naungana na wana CHADEMA wote kufikisha salamu hizi kwa familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuweka wazi kuwa naunga mkono kwa asilimia mia moja maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe na naamini kwamba Serikali itaenda kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa alipata kusema maneno yafuatayo naomba niyanukuu: "tunataka kuona katika Taifa hili vijana jeuri na wenye kujiamini siyo vijana waoga akina ndiyo Bwana Mkubwa, vijana wenye ujasiri wa kuhoji na kupiga vita mfumo wa jamii isiyoshabihiana na matakwa na matarajio ya jamii ya Kitanzania na tunataka kuona vijana waasi dhidi ya mfumo kandamizi, ubwana na ujisadi katika Taifa". (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kijana nauliza swalii ambalo vijana wenzangu wa Tanzania wanaauliza *where is Ben Saanane?* Tunapozungumza leo hii kijana aliyezaliwa na mwanamke na Watanzania tunajua usemi wa Kiswahili unaosema "uchungu wa mwana aujuae mzazi" kijana wa

watu Ben Saanane ana takribani miezi sita haonekani, hajulikani alipo, itakuwa ni kosa kubwa kama Bunge tukinyamaza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa mbalimbali zimeletwa mbele yetu, katika mijadala hii kunaonekana kwamba kulikuwa kuna namba 0768-797982 iliyosajiliwa kwa jina la Emmanuel Joseph, ndio iliyotuma ujumbe wa vitisho kwa Ben Saanane. Wasiwasi wangu kama kijana ambaye leo hii nipo katika siasa lakini siasa za upinzani na wasiwasi alionao Mama yangu Doris Harold Mboni alipo ni kwamba je, nini hatma yangu kesho? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza mwezi Oktoba, 2016 kulitokea uvumi wa aliyekuwa Mkuu wa Majeshi Nchini Devis Mwamunyange kwamba amelishwa sumu. Uvumi huu ulianza tarehe 2 Oktoba, 2016 lakini ukaja kufupishwa kwa kumpata kijana aliyetuma na kuanzisha ujumbe huu kupitia *TCRA* na Jeshi la Polisi, tunachouliza ni kitu gani kifanyike, ni aina gani ya hasira na maumivu ya wazazi wa Ben Saanane waliyonayo wayafanye ili *TCRA* na Jeshi la Polisi liseme huyo aliyetuma ujumbe ni nani? yuko wapi na wamechukua hatua gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu wana CCM pamoa na wana CHADEMA na wana *CUF* hakuna dhambi kubwa duniani kama dhambi ya uoga, uoga huanza kumtafuna mmoja baada ya mwingine. Tumeimbiwa juzi hapa na kijana mwenzangu Diamond anasema tupige kimya, mimi kama tunda la aliloliacha Baba wa Taifa sitokaa kimya nikiwa kijana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Waziri Mkuu kwa sababu tunapozungumzia hali ya kisiasa nchini ni lazima tuzungumzie *tension* iliyosambaa. Mimi kama Mbunge naweza nikajihakikishia usalama wangu lakini kwa wanaonipenda, familia yangu, jamaa zangu nawahakikishia nini? Tunapokaa hapa sasa hivi tunaongelea hali ya kisiasa kuwa nzuri nchini lakini kuna video zinatapakaa za Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaama akivamia kituo cha Television

(*Clouds Media*) Waziri Mkuu hajazungumzia kitu chochote. Pamoja na kwamba hawa ni wateule wa Rais lakini ipo haja Waziri Mkuu kuzungumza haya kama Msimamizi Mkuu wa shughuli za Serikali hapa Bungeni na tulitegemea kwamba hili litaonekana hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linasikitisha sana ni kuhusu *pension* ya Wazee ambayo iko chini ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mwaka 2010 hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kwa kuwa ilikuwa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi, wazee waliahidiwa *pensheni*, leo miaka 15 baadaye hakuna anayezungumzia *pension* ya wazee ambayo ilisemwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Mwaka 2005 na 2010 ni dhahiri kuwa, waliokuwa wapigaji kura wakubwa walikuwa ni wazee, sasa leo tunawaachaje? Itakuwa dhambi kubwa sana kuhitimisha mjadala huu bila kuhakikisha Serikali inatekeleza ahadi yake ya kuhakikisha wazee wote nchini wanapata *pension*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia kuhusu watu wenye ulemavu. Ni haki na wajibu wa walemvu kupata huduma zote za kijamii kama ambavyo tunapata sisi wengi lakini hali ikoje? Tukijiangalia na kufanya tathmini katika sekta mbalimbali za huduma za jamii, je, walemvu wamewekewa mazingira rafiki, kuwawezesha kupata haki zao za msingi kama tunavyopata wengine? Ukienda hospitalini, hakuna hata kitu kimoja kinachoonesha kwamba haya mazingira ni rafiki kwa walemvu, ukienda katika sekta ya elimu huwezi kukuta mazingira rafiki kwa ajili ya walemvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna mikakati imewekwa ambayo Serikali inasema kwamba imejaribu kuyajibu haya lakini kwa kiwango kikubwa mtu mlemavu anayezaliwa katika familia ya kimaskini anakuwa ameachwa kama alivyo. Sasa ni wajibu wetu kama Wabunge kuendelea kuikumbusha Serikali kuhakikisha inajenga mazingira wezeshi kwa watu wenye ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira rafiki au mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara; tarehe 2 Februari, 2017, Waziri Mkuu alitoa katazo la uuzaaji wa viroba. Hakuna asiyepinga matumizi ya viroba nchini, lakini je, hili katazo liliuja kwa wakati na je, liliuja rafiki kwa wafanyabiashara? Mfanyabiashara wa Dodoma tulioneshwa hapa amejipiga risasi shambani kwake kwa sababu alichukua mkopo. Tunasemaje kwamba tunajenga mazingira wezeshi wakati Serikali inatoa matamko bila kufikiria athari zake mbadala zinazojengwa kwa wafanyabiashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kwa ubaya gani kwa Waziri Mkuu kuzuia uzalishaji wa viroba nchini halafu wawape muda au *grace period* hawa wafanyabiashara warudishe viroba viwandani vifanyiwe *packaging* inayotakiwa ili kuhakikisha kwamba hawa watu wanaweza kurejesha mikopo yao. Leo hii mtu amejlua kwa hasara ya karibu bilioni mbili, bilioni tatu, Waziri Mkuu anasemaje kuhusu hicho kitu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu ambaye anapenda matumizi ya viroba hapa, kwa sababu mwisho wa siku hivi viroba mnavyokataza vinaenda kutengenezwa upya katika ujazo mwingine na mnasema kwamba matumizi yake wanatumia vijana, hapana. Leo ukienda kwenye maduka ya reja reja mtoto wa miaka saba, nane anatumwa kwenda kununua sigara, kuna mtu anayezungumzia hiki kitu au kwa sababu sigara imeandikwa ni hatari kwa maisha yako? Ni lazima tuhakikishe kwamba, tunawawezesha wawekezaji na wafanyabiashara nchini kwetu mazingira ya kubadilisha maisha kwa kupitia matamko yatakayowajenga na siyo kuwabomoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumeona kwamba kuna baadhi ya makampuni nchini ambayo yanawafanyisha watu kazi bila ya kuwa na mikataba ya ajira. Je, Serikali inalionia hili? Kamati ya Miundombinu tulipita katika makampuni mengi ya simu na tukaona kwamba kuna wafanyakazi ambao wanafanya kazi nchini lakini hawapewi mikataba ya ajira na hii mwisho wake inasababisha wao

kushindwa kupata stahiki zao za kazi. Naamini kwamba Serikali inaweka mkakati wa kuhakikisha kwamba mikataba ya kazi katika sehemu za ajira inapewa kipaumbele na Watanzania hasa wazawa wanapata stahiki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye jambo moja la msingi; Tanzania ni yetu sote, Tanzania haitojengwa na CHADEMA peke yake, haitojengwa na CCM peke yake, ndio maana leo hii fedha za miradi ya maendeleo hazitoki Lumumba, mnakusanya kwa Watanzania waliowachagua na wasiowachagua, mnakusanya kutoka kwa wana CHADEMA na wasio wana CHADEMA, sasa tunapokuja tunajinasibu kwamba hii ni mikakati ya Serikali, hata *TLP* ingepewa dhamana ya Serikali, ingesimamia kwa sababu ni wajibu wa kila Chama kusimamia....(*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sakuru. Mheshimiwa Joyce Mukya.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee alipoishia mwenzangu Mheshimiwa Zubeda kuhusu wale mavu. Wale mavu wamekuwa wakidhalilishwa sana, wale mavu wamekuwa hawasaidiwi kimatendo. Kwenye hotuba ya Waziri Mkuu katika ukurasa wa 47 amezungumzia suala la wale mavu lakini hakuna mkakati wowote unaooonesha kwamba wale mavu watasaidiwa kimatendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kama ambavyo tunatoa asilimia 10 kwenye Halmashauri zetu kutoka kwenye *own source*, naomba kwenye asilimia hizo hizo 10 iwe ni lazima kwa wanawake asilimia tano wawepo wale mavu *at least* watano au 10 kwenye watu 30 na

walemavu wengine watano kwenye watu 30 ambao ni vijana. Naomba sana kwa sababu walemavu hawa wanaonekana kwa macho tofauti na wanawake na vijana ambao mara nydingi wamekuwa wakitumika kisiasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanasiasa mara nydingi wamekuwa wakiwatumia wanawake na vijana kwa ajili ya kuwatafutia kura kwa vipindi vyta uchaguzi vijavyo lakini naomba sana suala la walemavu wamekuwa hawana msaada dhahiri unaoonekana. Naomba sana suala la walemavu, aliliongelea sana Marehemu Dkt. Elly Macha, naomba tumuenzi marehemu Mheshimiwa Macha kwa kuwasaidia walemavu wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hela za maendeleo; ni dhahiri kwamba Serikali yetu imeshindwa kabisa kuisaidia nchi hii kwa hela za maendeleo. Asilimia 34 tu mpaka bajeti inakwisha ya mwaka 2017, hakuna hela za maendeleo ambazo zimeenda kwenye Halmashauri zetu ambazo zinaenda kuwasaidia moja kwa moja wananchi kule chini. Ingekuwa hakuna *own source* katika Halmashauri zetu, mfano, Arusha Mjini tunaendesha Halmashauri kutokana na *own source* zetu wenye. Mpaka Februari mwaka 2017 imeenda shilingi milioni 320 kati ya bilioni tatu ambayo ni asilimia 11 tu iliyopendekezwa mwaka 2016. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tunavyoendelea hivi tunaenda kuua zile Halmashauri zetu, wananchi hawatapa maendeleo na kwa Halmashauri ambazo ziko vijijini hawana *own source* za maana, wanashindwa kuendesha vikao, wanashindwa kulipana hela za vikao, wanashindwa kufika kwenye vikao kutokana na umbali ama *distance* kulipana mafuta na gharama za usafiri kwa sababu tu Serikali haipeleki hela za maendeleo kule chini. Naomba sana hili mliangalie kwa jicho la pekee sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongele suala la utawala bora; kumekuwa na tabia mbaya sana Viongozi wa Serikali wanachukua madaraka mikononi na kuanza

kutumia hela za Halmashauri au hela za Mikoa na Wilaya walizopangiwa kuanza kutumia bila kuwashirikisha Kamati za Fedha na Uchumi za Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limetokea mwaka jana Septemba. Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mheshimiwa Mrisho Gambo aliita Walimu wa AICC pale Simba Hall akaongea nao, wakahojiana, Walimu 701 wakampa madai yao akamuamuru Mkurugenzi wa Jiji, Ndugu Athuman J. Kihamia awalipe wale Walimu shilingi 169.8 milioni, hii siyo sawa. Hata kama Walimu wale walikuwa wanatakiwa walipwe zile pesa lazima ilitakiwa vikae vikao vya Kamati ya Fedha na Uchumi, lazima vikae vikao lakini siyo Mkuu wa Mkoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mkuu wa Mkoa alikuwa anaumia sana na wale Walimu angeingia kwenye Mfuko wake wa Mkoa na kutoa hela kwa ajili ya kuwalipa wale walimu. Hilo alilofanya siyo sawa, alipoambiwa akasema nawakomesha na hapa nimeanza tu lakini mtakoma. Pesa zile zilikuwa kwa ajili ya kuwalipa Madiwani, ilikuwa ni stahiki za Madiwani kwa ajili ya vikao, kwa ajili ya vocha, kwa ajili ya usafiri lakini Madiwani ambao wanaongozwa na Chama cha CHADEMA walivumilia yote na leo wanaenda kwenye vikao wanalipwa sh. 40,000 mpaka sh. 60,000 mbali walivyokuwa wanalipwa sh.120,000 kwa kikao kimoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la Faru Fausta; Serikali hii imejitanabaisha kuwa inapunguza matumizi na mpaka sasa hakuna mtu ye yeyote ambaye analipwa milioni 17 kwa mwezi, lakini Faru Fausta analipwa milioni 64 kwa mwezi hiyo ni mara tatu. Gharama za Faru Fausta huyo ambaye ni Mzee ana miaka 54 ni kwa ajili ya gari lake ambalo linabeba chakula chake, kwa ajili ya chakula kinachotoka nchini Kenya aina ya LASEMI, kwa ajili ya kulipa Walinzi 15 ambao wanamlinda kwa masaa 24 na nguvu za Kijeshi. Faru Fausta huyu ni Mzee lakini ukiongea na Wizara ya Maliasili wanakwambia eti kwamba anaingiza fedha nyingi za kigeni sawa na bilioni 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini kama Wazungu au Watalii wanakuja Tanzania kumuangalia Faru Fausta peke yake. Naamini Watalii wanakuja Tanzania kuangalia utalii, kujifunza kutalii Tanzania lakini wakifika Tanzania wanakutana na Faru Fausta. Naomba sana Serikali kwa sababu inajidai kwamba inapunguza gharama na kutumbua majipu, ianze kumtumbua Faru Fausta ambaye ni Mzee sana sasa hivi na wanasema kwamba nyumba yake ikishakamilika atatumia milioni 20.4 tu sawa sawa na milioni 244 kwa mwaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado gharama hizi ni kubwa sana. Kule chini Ngorongoro wale Wamasai na wale wakazi wa Ngorongoro wanahangaika, hawana mahali pa kulisha mifugo yao, Serikali imeshindwa hata kuwajengea majosho kule juu kwa ajili ya kulisha mifugo yao, Faru Fausta ambaye ni Mzee anahudumiwa kwa milioni 64 kwa mwezi, hii siyo haki na siyo sawa kwa wananchi wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie katika suala la elimu bure; elimu bure ni kwenye makaratsi tu, ukienda kule chini elimu bure hakuna cha elimu bure zaidi ya kulipa ile *UPE*. Walimu wamekuwa kwanza wanahangaika, hakuna walimu wa sayansi, hakuna walimu wa hisabati, imefikia wazazi wakae vikao na walimu na wanafunzi kutafuta walimu wa hisabati na walimu wa sayansi. Inabidi walimu wakae vikao na wanafunzi na wazazi kulipa walinzi, kulipa maji kwa ajili ya wanafunzi wao waweze kusoma, hii siyo sawa kabisa hapa hakuna elimu bure. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Ma-*DC* na Ma-*RC* badala ya kupigana na Wapinzani kwenye Wilaya zenu na Mikoa yenu, tafuteni njia mbadala ya kusaidia a elimu bure ambayo ni sera ya Serikali yenu. Kama mnawenza kuchangisha hela za Mwenge, Mheshimiwa Gambo Arusha alinunua pikipiki 200 kwa kusaidiana na wadau wa Mkoa wa Arusha sasa Mheshimiwa Gambo fanya hili la elimu bure kwa watoto ambao wanakua sasa hivi. Naomba sana hili mliangalie kwa jicho la pekee kabisa, hakuna elimu bure hapa ni utapeli tu wa makaratsasi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika suala la utalii; suala la utalii tangu kodi na tozo za utalii zipande limekuwa halina faida kwa nchi yetu. Kama mnavyofahamu nchi ya Kenya ndiyo imekuwa mpinzani mkubwa sana kwetu kwa suala la utalii. Nchi ya Kenya imeondoa kodi ya VAT, nchi ya Tanzania imeweka kodi ya VAT, nchi ya Kenya imeondoa kodi kwenye magari ya utalii wakati wa matengenezo, nchi ya Kenya imeondoa Visa kwa watoto na kuwafanya watalii ambao wana familia waende Kenya na siyo Tanzania. Nchi ya Kenya imeondoa Park fees Tanzania vyote hivyo mmeviweka, Tanzania mnataka utalii wa aina gani ninyi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Tanzania, naomba sana nchi yetu, naomba sana Waziri Mkuu anavyokuja kujibu utalii Tanzania umeshuka katika ukurasa wa 20 amesema kwamba utalii umepanda kwa asillimia 1.2 siyo kweli. Wageni hawa ambao wanaingia nchini ni wageni ambao wanakuja kwenye mambo ya kibiashara na mikutano lakini takwimu za utalii zinasema wageni wote wanaokuja Tanzania ni watalii siyo kweli, siyo watalii wa vivutio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wageni wengi wanatokea Rwanda, wanatokea Burundi, wanatokea *South Africa* na hii ni kwa sababu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu anapopewa takwimu zipitie na watu wako, anapokuja hapa kwenye Bunge ziletwe takwimu ambazo ni sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee mimea vamizi katika *crater* ya Ngorongoro. Kumekuwa na mimea vamizi sana katika *crater* ya Ngorongoro. *crater* ya Ngorongoro kuna uoto wa asili. Mimea vamizi imeharibu *craterya* Ngorongoro, Waziri January Makamba alienda lakini hali ni mbaya na mbaya zaidi mimea hii inakua kwa kasi sana. Sehemu ambako mimea hii inakua, wanyama hawawezi kwenda kula. Sasa inaharibu uoto wa asili kule. Naomba sana Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Waziri Mkuu ashirikiane... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanne Mcemba, ajiandae Mheshimiwa Profesa Maji Marefu na Mheshimiwa Joram Hongoli ajiandae.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami pia kwa kunipa nafasi nichangie hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza nianze na pongezi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anayoifanya, asirudi nyuma, ana uhakika na kitu anachokifanya nasi tunamuunga mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu kazi allyoifanya katika nchi hii ni kubwa sana, siyo hilo tu uamuzi wake wa kuhamia Dodoma inataka ujasiri, ametekeleza jinsi Mheshimiwa Rais alivyosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze tena ndugu yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, amesimamia vizuri sana uanzishwaji wa Makao Makuu na Serikali kwa ujumla akiambatana na Naibu wake Mheshimiwa Antony Mavunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitatenda haki kama sitatoa pongezi kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, wewe Mwenyekiti na Viongozi wote ambao wameweza kufanya kazi ya Bunge hadi sasa tuko vizuri ingawa Bunge lilikuwa katika hali ngumu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah amefanya kazi nzuri, tumetembea, tumefanya kazi kwenye miradi na Kamati zimekwenda vizuri, niwapongeze sana kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kuisimamia Bunge. Pia nimpongeze tena AG kwa kazi nzuri ya kuisimamia sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, niwapongeze Mawaziri wote, wamezunguka Tanzania hii kuhakikisha llani ya Uchaguzi ya CCM inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie hoja sasa ya kuchangia Bajeti hii. Mimi nichangie moja kwa moja kuhusu viwanda, bahati nzuri au mbaya Waziri wa Viwanda hayupo. Tabora tuna matatizo makubwa sana ya viwanda, tulikuwa na kiwanda cha nyazi hakipo, nimpongeze Waziri wa Viwanda amesema kwamba wako njiani na yule Mwekezaji anakuja kuzindua kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hicho kinasikitisha, kina historia kubwa sana katika Mkoa wa Tabora, kiliwezesha kuwapa ajira vijana wetu lakini sasa tumerudi kwenye umaskini. Tuna kiwanda kingine cha Manonga, kila siku nazungumza na sitachoka kuzungumza. Kiwanda cha Manonga cha Rajan mpaka sasa kina matatizo ambacho kiko Wilaya ya Igunga. Naomba katika uwekezaji sasa iangalie suala zima la viwanda katika Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunasindika asali, tunarina asali nyingi sana katika Mkoa wa Tabora na zamani tulikuwa na kiwanda cha Kipalapala ambacho kilikuwa kinasindika mpaka tunauza nchi za nje lakini kimekufa, kwa hiyo natangaza soko na ombi la wawekezaji kama watakuja kuwekeza ardhi ipo na ipo ya kutosha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo suala zima la afya. Tuna tatizo sana la hospitali za Wilaya, Manispaa ya Tabora, Kaliua, Uyui mpaka sasa Hospitali za Wilaya hazipo. Niombe Serikali iangalie kwa jicho la huruma kwa sababu tabu wanayopata wananchi wa maeneo hayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aiangalie. Wilaya ya Kaliua haina Hospitali ya Wilaya, wanakwenda Urambo kutibiwa lakini wazingatie pia kwamba kuna huduma ambayo inatakiwa akinamama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Igunga kuna kituo cha Afya ambacho ni cha Jimbo la Manonga. Kimekamilika, kilikuwa kimefadhliliwa na *ADB* mpaka sasa hakifanyi kazi, hakuna vifaa vya kufanya kazi, hakuna gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la maendeleo kwenye maeneo yetu. Serikali imefanya kazi kubwa sana kuondoa umaskini kwenye kaya maskini hususan TASAF, imefanya kazi nzuri sana. Imezunguka na imesaидia miradi ya awamu ya kwanza na ya pili ambayo haijakamilika tungeomba sasa awamu ya tatu Serikali iangalie na ikamilishe miradi yote hususan vituo vyatya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali kusimamia na kuhakikisha mradi wa MKURABITA unakwenda vizuri na wanapewa pesa za kutosha ili angalau wapunguze umaskini kwenye kaya ambazo ziko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie asilimia 10 ya Wanawake na Vijana, Serikali imefanya vizuri. Niwapongeze Wakuu wa Mikoa, niwapongeze Halmashauri na Majiji nchi nzima, kwa sababu naomba nichangie kama Makamu Mwenyekiti, nina uhakika na ninachokizungumza kwa sababu wamekuja kwenye Kamati yetu, tumeona bajeti waliyopanga na mafanikio yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu Halmashauri zote zimetenga asilimia 10 kwa sababu mwaka 2016/2017 tuliwapa masharti kama Kamati, wamefanya kazi nzuri, nawapongeza na kwenye bajeti wameonesha. Kwa hiyo, kazi wanalfanya, hatuwezi kusema hawafanyi, asilimia 10 ipo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna baadhi ya Halmashauri imeweza kutenga katika asilimia 10 imesaيدia makundi maalum. Kwa mfano, Tanga tumekuta wale wenzetu kwenye makundi maalum wasiosikia wametengewa fedha. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie jinsi gani ya kutenga asilimia 10 angalau asilimia mbili wawewe kupata wenyewe makundi maalum. Ukurasa wa kumi na sita Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema, naungana naye na ni kweli hii fedha imetolewa, tuombe tu Serikali iangalie ni jinsi gani sasa ya kusaidia kuhakikisha fedha zile zinaongezeka. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni barabara nipongeze sana Serikali, barabara ya kutoka Itigi kwenda Tabora imetengewa fedha, lakini bado kazi ile inasusua. Kwa hiyo niombe barabara ya kutoka Chaya kwenda Tabora ipewe kipaumbele. Niombe tena barabara ya kutoka Puge kwenda Ndala, Nkinga hatimaye Manonga, hii barabara tumeiombea sana iweze kutengenezwa, Nkinga kuna hospitali kubwa sana ambayo inasaidia wananchi wa Mkoa wa Tabora kwa ujumla. (*Makofi*)

Kwa hiyo, niombe sana Serikali iangalie...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maji Marefu, ajiandae Mheshimiwa Hongoli na Mheshimiwa Kakosa ajiandae.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Bajeti ya Waziri Mkuu, vilevile nitoe pole sana kwa familia ya Dkt. Macha kwa msiba mkubwa ambao umewapata. Nawapa pole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendelee kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuilinda nchi hii. Wote sasa tumekuwa kitu kimoja na wote tumekuwa sawa. Vilevile nisiache kumshukuru Waziri Mkuu, Spika, Naibu Spika, Katibu wa Bunge pamoja na Wizara ya Afya pamoja na Wabunge wote bila kujali Vyama vyao kwa msaada mkubwa walionipitia wakati naumwa pale, hawakujali vyama wala itikadi za vyama vyao, walikuja wakaniona na walinipa faraja sana. Nawashukuru sana ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, haya mambo msiyafanye kwangu tu, myafanye kwa kila Mbunge msijali vyama vyao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nianze kwanza kwa kuongelea Mfuko wa Jimbo. Mfuko wa Jimbo toka tumeanza kuupata Mfuko huu wa Jimbo toka mwaka 2009 haujafanyiwa marekebisho ya aina yejote. Mfuko wa Jimbo umekuwa ni kichocheo cha Wabunge katika kila Wilaya na kila Jimbo ili pale wananchi wanapojitolea sisi tunaongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu umekuwa hauwasaidii sana Wabunge kwa sababu unakuwa na mlolongo mrefu kiasi ambacho Mbunge hana uwezo nao, yeje kazi yake ni Mwenyekiti tu, lakini inapofika kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia maendeleo yaliyoanzishwa na wananchi, Mfuko huu unakuwa ni mgumu sana kama vile ni mfuko ambao tumepewaa kama mtego. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, huu Mfuko wa Jimbo usiishie tu kwa Wabunge wenye Majimbo. Hata hawa Wabunge wa Viti Maalum wangekuwa wanapewaa kiwango kiasi kwa sababu wengi wa Viti Maalum hawakai katika Majimbo peke yake, wanazunguka katika mikoa yote. Wanapozunguka katika mikoa wanafika mahali akinamama wanawaambia tuna shida, utatoa wapi hela? Hela yenjewe ndiyo hii ya kuchanganya changanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba nao hawa Wabunge wa Viti Maalum watengewe kiwango kidogo kisilingane na cha kwetu lakini kiwasaidie kuzunguka katika mikoa yao ili itusaidie Wabunge wa Majimbo ili iwe inatupa nguvu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua Mheshimiwa Waziri Mkuu akija atuambie sisi sasa hivi tuko wapi, kwa sababu mara nyingi tulikuwa tunaambiwa vifaa vyaa Wabunge katika Majimbo hasa zile *furniture* tunapewaa na Ofisi ya Bunge, jambo la kushangaza hii taarifa kwa Waraka wa mwaka 2010 inaonesha kabisa kwamba Mfuko huu uko chini ya Mkuu wa Mkoa, toka Wakuu wa Mikoa wamepewaa

huu mfuko kwa ajili ya kuwasaidia Wabunge, hakuna hata Mbunge mmoja ambaye amejengewa ofisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kwenye Ofisi ya Bunge tunaomba vitendea kazi lakini tunaambiwa viko kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Mikoa hawatuelezi ukweli. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kutoa hitimisho lake atuelekeze vizuri Wabunge tuisumbue Bunge. Tukisumbua Bunge wakati kitu hiki kishatengwa kwamba kwenye Waraka wa Rais wa mwaka 2010 unaonesha kwamba Mfuko huu uko chini ya Mkuu wa Mikoa na sisi tukija hapa tunaendelea kuwasumbua wenzetu ili tuonekane kwamba tunafanya kazi nzuri lakini kule vijijini watu hawajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tusijitetee sisi tu. Hapa tuko katika mazingira mazuri kufuatana na utendaji mzuri wa Rais wetu, lakini kuna Watendaji ndani ya Bunge hili wanafika wakati wao wenzetu ambao wanatusaidia kwa kila kitu hata mishahara wakati mwingine wanakaa miezi mitatu hawapati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge hakuna Mbunge ana mazingira magumu. Tulizoea raha sana ndiyo leo tunaona kwamba kuna ukata. Watu wanakwenda kwenye vyombo vyaya habari kusema kwamba kuna mazingira magumu, mazingira magumu hakuna. Ukiangalia bajeti yetu ni ile ile, ila siku za nyuma Wabunge tuli-relaxsana tukajisahau ndiyo maana inafika mahali mtu anakimbilia kwenye Vyombo vyaya Habari kusema Bunge baya, Bunge gumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mazingira ya mwaka 2010 hakuna kilichopungua ila utendaji wetu, raha zetu, maisha yetu, ndiyo tunakimbilia kusema kwamba maisha magumu. Hela tunapata kwa wakati, hela ni ile ile. Tulikuwa tunapata sh. 80,000, lakini sasa hivi tunapata karibu sh. 120,000 na tunapata sh. 200,000. Sasa tukianza kuyasema haya hatutendi haki. Naomba tuwe wawazi..

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana! Niacheni niseme, kila mtu anasema kwa wakati wake, kila mtu yuko huru kusema. Tusiwe tu watu wa kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niyaseme haya mapema kwa sababu inafika mahali tunakimbilia vyombo vya habari, tukae wenyewe, tuna uongozi wetu, tukae chini, tuangalie upungufu uko wapi, turekebishe kuliko kukimbilia kulalamika, kama sisi tunalalamika na wapiga kura nao watamlalamikia nani? Nimekosea eeh?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Kumbe imefika mahali pake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu matibabu ya Wabunge.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS , TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Ngonyani mzungumzaji anayezungumza sasa kwamba, kwa taarifa tunazozijua sisi ni kwamba hakuna Mbunge ye yote anayedai, anayedai posho, anayedai *sitting allowance*. Kwa hiyo, unavyosema ni sawa kabisa kwamba hapa mambo ni safi isipokuwa mazoea ya watu ndiyo tatizo. (*Kicheko*)

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri nimeipokea taarifa yako na naendelea kuongea ..

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kwenye suala la matibabu ya Wabunge. Tungeomba ikiwezekana Waziri Mkuu amshauri Rais, matibabu ya Wabunge yarudi kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu yalikuwa....

**MBUNGE FULANI:** Taarifa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngonyani, ngoja kidogo taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimpe taarifa mzungumzaji kwamba tunavyozungumza maslahi ya Bunge, tunazungumza Bunge kama Taasisi ili Wabunge wafanye kazi zao katika mazingira ambayo ni rafiki ikiwemo na Kamati. Hatuzungumzi habari ya maslahi ya Mbunge mmoja mmoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake siipokei, kama ye ye aliкуja kufuata maslahi...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa siopokei taarifa kutoka upande wowote.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachojua kilichotuleta hapa siyo maslahi ya Wabunge ni maslahi ya wapiga kura walio tuchagua kuja kutetea Bunge hili. Kama watu walifuata maslahi basi wakabadilishe kazi ambayo itakuwa na maslahi juu yao lakini ninachokumbuka kilichotuleta hapa ni kutetea wanyonge walio tuchagua ili tuwape maslahi mazuri waendelee kutuchagua kwa namna yoyote ile. Kwa hiyo, taarifa yake siipokei akatafute sehemu nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la matibabu ya Wabunge, naomba mzigo mkubwa...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. ALLY K MOHAMED:** Bima ya Afya inatosha..

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ester Bulaya, tuwe na *order* ndani ya Bunge.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu, naona kuna mahali nimewagonga kidogo ndugu zangu. Kama kuna mahali nimewakosea ndugu zangu Wabunge basi kawaida ya mtu huwa tunasameheana basi tugange yanayokuja, ahsanteni. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea na suala la matibabu. Siku za nyuma suala la matibabu yalikuwa yanapitia Ofisi ya Spika na ye ye alikuwa anajua huyu anaumwa au huyu haumwi, inategemea sasa hivi tumeona kwamba Rais anafanya kazi nzuri sana lakini baadhi ya watumishi wake wanaweza kuchelewesha kitu kwa makusudi na kumfanya mgonjwa azidiwe. Hapa ningeomba Mheshimiwa Rais ambakishie madaraka Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili aendelee kutusaidia katika kututibu au kwenda kuzungumzia suala la aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nizungumzie mambo machache naona taarifa zinakuwa nyingi kwa sababu nimegusa maslahi ya Wabunge, nilichokuwa nataka kujali ni kwamba kauli aliyosema Mheshimiwa Simbachawene kwamba hakuna tunachokidai mambo yote yako sawa, kwa hiyo naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hoja zangu zote alinisaidia kunisafirisha India kwa kunilipia watu zaidi ya wawili. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa msaada wako mkubwa, usifanye kwangu tu, fanya na kwa hawa wengine ambao maslahi yao wanaona kama yamebanwa banwa, Mungu awasaidie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
*(Makof)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hongoli, Mheshimiwa Kakoso nafikiri hayupo, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Kafumu na Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa hii nafasi. Kwa namna ya pekee naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi anazofanya hasa za kuiongoza nchi yetu Tanzania. Niwashukuru Mawaziri wote kwa namna ya pekee nimshukuru Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anazozifanya na Mheshimiwa Jenister Mhagama na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa wanazofanya usiku na mchana kuhakikisha kwamba Watanzania tunapata maendeleo. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa walioifanya kwa kuimarisha viashiria vya kukua kwa uchumi, hasa kwenye upande wa ujenzi wa barabara. Lengo la Serikali ilikuwa ni kujenga na kukarabati barabara kilomita 692, lakini tumefanikiwa kukarabati na kujenga barabara kilomita 430 ambayo ni sawa na asilimia 62. Naipongeza sana Serikali yangu inayosimamiwa na John Pombe Magufuli na inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kidogo kidogo juu ya barabara yetu, hasa barabara yetu ya Lupembe. Barabara ya Kibena, Lupembe, Madeke ni mionganoni mwa barabara zilizopangwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami, mwaka jana kwenye Bunge la Bajeti tulipitisha shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, mpaka sasa bado tenda ya ujenzi wa barabara hii haijatangazwa, nimwombe Waziri mwenye dhamana na Waziri Mkuu mwenyewe aliona ile barabara jinsi ilivyo angalau tuweze kutangaza *tender* na ianze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana, ile barabara ya Lupembe kwanza inatuunganisha watu wa Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro kupitia Jimbo la Mlimba. Barabara hii imekuwa ni barabara muhimu ambayo wananchi wetu wa Lupembe wanasafirisha mazao yao. Lupembe tunalima chai, Lupembe tunazalisha mbao, tunazalisha nguzo za umeme, tunazalisha maharage, mahindi, viazi na kila aina ya matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea barabara ile kutokana na mvua zinazoendelea sasa hivi haipitiki tena, imekuwa-*blocked*, kuna eneo kubwa gari zimekuwa zikikwama na hivyo wananchi kupoteza uchumi mkubwa sana kwa mazao yao kuozea barabarani kwa kutoweza kusafirisha au kupitisha kupitia ile njia, kwa mtindo huo maana yake tunakwamisha uchumi wa wananchi wa Lupembe. Naiomba Serikali yangu sikilu itenye hizi fedha ili tuweze kupata uchumi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojuu Mkoa wetu wa Njombe ni moja ya mikoa ambayo tunaitegemea sana katika uzalishaji wa mazao ya chakula, pia nguzo kama nilivyosema na zao hili la chai. Sasa kama tutakuwa bado hatuna barabara nzuri, itakuwa ni vigumu wananchi wanazalisha kwa wingi, lakini hawatoweza kuuza au mazao haya hayataweza kufikia soko kwa sababu barabara yetu siyo nzuri na haipitiki wakati wa kifuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba atakavyokuja kusimama baadaye niweze kujua ni lini sasa Serikali itatangaza *tender* illi barabara hii ianze kujengwa kwa kiwango cha lami kadri ilivyokuwa tumekubaliana katika llani yetu ya Chama cha Mapinduzi pia katika bajeti ya mwaka jana, kwa hizo fedha tulizotenga bilioni nane. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa kilimo, Mkoa wetu wa Njombe ni moja ya mikoa ambayo inategemewa sana katika uzalishaji. Mikoa mingine inapopata njaa sisi ndiyo watu tunaohusika katika kutoa chakula au wananchi wa Njombe ndiyo wanaosambaza chakula katika mikoa

mingine tukishirikiana na Mikoa ya Ruvuma, Mbeya na Rukwa. Mikoa hii pia iweze kupewa *consideration* maalum katika kuhakikisha kwamba tunaipatia kipaumbele hasa kwenye upande wa pembejeo. Mara nyingi pembejeo zimekuwa zikija kwa kuchelewa, zinafika wakati tumepanda, sasa bei yenyewe iko juu, wananchi wetu hawawezi kununua kwa bei hiyo kwa sababu kipato chao ni kidogo, tunaomba bei ya mbolea ipungue, pia iwahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Njombe huwa tunalima mara mbili, tunalima mwezi wa Sita kwenye bustani baadaye mwezi wa Kumi tunalima sehemu za milimani ambako kunazalisha magunia ya kutosha au mazao ya kutosha. Kwa hiyo, tuombe mbolea zije mapema na ikiwezekana zianze kuja mapema mwezi wa Sita ili wananchi wetu waweze kutumia mbolea vizuri na hatimaye waweze kupata mazao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee zao moja la chai ambalo tunalima hasa maeneo ya Lupembe na maeneo ya Luponde. Zao hili limekuwa likiuzwa kwa bei ndogo sana ukilinganisha na gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukipiga hesabu ya mbolea inayotumika shambani, kuhudumia ule mmea mpaka unapofikia kuanza kutoa chai, kilo moja ya chai inagharimu takribani shilingi 450 na zaidi, lakini bado tunauza kwa shilingi 250, sielewi ni kwa nini zao hili limekuwa likiachwa tofauti na mazao mengine kwa hiyo tuombe wananchi wetu ili wasiendelee kuzalisha kwa hasara, angalau tupunguze baadhi ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali mmeshapunguza tozo la moto na uokoaji, nipongeze sana Serikali kwa jitihada hizo lakini bado bei ya kuuzia wananchi haijapanda, pamoja na kwamba baadhi ya kodi imepungua, bado bei imebaki palepale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama kuna kodi nyingine ambazo zinafanya hili zao liuzwe kwa bei ndogo

basi nazo tuziondoe ili waweze kunufaika na kilimo cha chai. Wote tunajua chai tunaitegemea sana hakuna mtu ambaye hatumii chai hapa ndani na ni zao ambalo kila mmoja linamgusa hasa kwenye matumizi ya majani ya chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali kwenye upande wa elimu, kwa kutoa elimu bure hasa kupeleka fedha kwenye shule zetu za sekondari na msingi kwa ajili ya kugharamia elimu bure. Ni kweli kabisa baada ya kuanza kutoa fedha hizi idadi ya wanafunzi wanaoingia darasa la kwanza imeongezeka, hata watoto wa sekondari wanaoacha yaani *drop out* zimepungua baada ya kuanza kupeleka hizi fedha. Wazazi wengi walikuwa wakashindwa kutoa...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge upande huu, tuko Bungeni Waheshimiwa. Mtu anacheka kama yuko nyumbani kwake. Endelea!

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi wengi walikuwa wanashindwa kulipa hizi ada na hatimaye kuwaondoa watoto shulenii na kuwarudisha nyumbani, hasa watoto wa sekondari na shule za msingi, baada ya hii elimu bure tumeona shule nyingi zinakuwa na watoto wengi pia shule za msingi wanaoingia darasa la kwanza wameongezeka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo lipo kwenye walimu wa sayansi, pamoja na kwamba tumeajiri walimu elfu mbili na kitu, tuombe basi hao walimu wasambazwe kwenye hizi shule za sekondari ili tuwe na mkakati na ni lazima tuwe na mkakati wa kudumu wa kuhakikisha kwamba tunawapata walimu wa sayansi wa kutosha, mkakati huu lazima tuanze mapema, tuwe na mkakati wa muda mrefu na wa muda mfupi. Tulichofanya sasa hivi ni kama muda mfupi, ni lazima tuanze kuandaa watu wetu hasa kuanzia shule za msingi kupenda masomo ya sayansi na wakienda sekondari wachukue masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutawezaje kufanya hivi, ni lazima sasa kule sekondari tusiweke *option*, tunapowaambia watoto wachague kuchukua *combination* za sayansi au kutosoma hasa *chemistry na physics*, tunafanya hawa watoto sasa waanze kukata tamaa mapema. Hivi sasa ukienda kwenye shule hizi za msingi, ukiuliza mtoto wa darasa la tano, utapenda kusoma masomo gani sekondari, atakwambia mimi nitasoma *art*. Nataka kuwa Mwanasiasa nataka kuwa Mwanasheria, ni lazima tutengeneze mazingira, tuwa-*motivate* kwa kuhakikisha kwamba watoto wote wanapokwenda kidato cha kwanza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso hayupo, Dkt. Kafumu yupo?

**MBUNGE FULANI:** Yupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii tena ya kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Namshukuru sana Waziri Mkuu kwa *speech* yake nzuri yenye maelekezo mazuri. Naipongeza Serikali kwa kazi nzuri mnazofanya, kazi zenyе changamoto nydingi sasa hivi, kwa kweli mna changamoto nydingi lakini endeleeni kuzifanya, endeleeni kulisaidia Taifa hili tuweze kufika mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa mchango wangu, naomba nitoe ushauri mdogo, ushauri unaotuhusu baadhi yetu sisi. Tuna bahati nzuri sana katika nchi yetu katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano, tumepata Rais mwenye sifa kubwa tatu, hizi sifa tulizihitaji muda mrefu. Sifa ya kwanza ana nia thabiti ya kuleta maendeleo kwa wanyonge. Sifa ya

pili, anaamua papo kwa papo, hacheleweshi na sifa ya tatu anataka watu wafanye kazi, ndiyo maana ya msemo wa Hapa Kazi Tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa hizi baadhi yetu tumezitumia vibaya, tumeshindwa kuzitumia kuzi-harness ili nchi yetu isonge mbele. Nasema hivyo kwa sababu baadhi yetu Wabunge wa Upinzani, Chama cha Mapinduzi, baadhi yetu Mawaziri siyo wote na baadhi yetu Wasaidizi wa Rais tumeshindwa kusema kweli. Tumeshindwa kushauri kwa ukweli, tumekuwa wanafiki, hili jambo litatuua sana, badala ya kutengeneza ushauri uliokamilika, unatengeneza ushauri nusu nusu, unampelekea Rais anaamua palepale unafikiri kitatokea nini? Tunahitaji uchambue ushauri wako uupime, uutengeneze uende umekamilika na Rais wetu huyu anayefanya papo kwa papo akiamua nchi inasonga mbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi haya yote tunayoyaona ni kwa sababu unafiki umezidi mionganii mwetu, nasema kweli. Mimi ni mwathirika wa mambo haya, mtu anaenda kusema anasema Dkt. Kafumu, Kafumu, Kafumu, jambo hili siyo zuri sana. Tumsaidie Rais kusonga mbele tutafika, tukifanya vinginevyo kwa kweli tatarudi nyuma. Ushauri wangu jamani tumsaidie Rais, tumshauri tumshike mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa aliamini katika ujamaa lakini waliomzunguka hawakuamini, tumeufikisha ujamaa wapi, Mzee amekufa ameondoka anaamini peke yake na sasa tuna bahati hii, hebu tuitumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, naomba nitoe mchango wangu sasa. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama ilivyo kwa Wabunge wa Tabora nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala la tumbaku lilikuwa linatusumbua kweli lakini

umelimaliza ahsante sana. Tunakushukuru sana endelea kuja Tabora kwa watani zako utusaidie na mambo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kifungu cha 46 kinazungumzia miundombinu, haya ninayoyasema nayaleta kwa Waziri Mkuu ili anisaidie kumwambia Waziri wa Miundombinu, Wilaya ya Igunga na Jimbo la Igunga, tuweze kupata miundombinu, tuweze kupata barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu sina barabara kabisa, unajua ni kwa sababu za kijiolojia. Miaka 60,000 Kabla ya Kristo Igunga asilimia 80 ilikuwa ni ziwa na ziwa hilo lilipokauka limeacha tope, ukifika Igunga ni mbuga ambayo ukitaka kujenga barabara ni lazima uweke tuta zito kubwa la juu. Halmashauri haina uwezo, tunajikuta hatuvezi kujenga barabara. Ukikwangua hiyo barabara ni ya kiangazi tu, wakati wa masika barabara hakuna kabisa na hasa Jimbo la Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igunga halina barabara ya *TANROADS*, kuna kipande cha kilomita nadhani kumi kutoka Itunduru kwenda Igurubi. Hakuna barabara ya *TANROADS* kwenye Jimbo la Igunga, wakati wa masika lile Jimbo halipitiki kabisa. Naleta hili kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, uwatume wataalam wakaangalie na hasa wakati wa masika wakienda, hatuvezi kabisa. Mimi huwa sifanyi kazi wakati wa masika, nasubiri kiangazi ndiyo niweze kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia barabara Jimbo la Igunga tunazungumzia, Kata 16 za Wilaya ya Igunga ambazo hakuna barabara ya *TANROADS* na wakati wa masika hakuna barabara. Nataka nizungumze habari za barabara Wilaya ya Igunga na nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, anisaidie kabisa ikiwezekana atume wataalam wakatembee sasa Igunga. Kwa kweli hakuna barabara na wale waliofika Igunga waliofanya kampeni wanajua hakuna barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa tunatumia 'mapanda ya ng'ombe', ni njia za ng'ombe hatuna barabara kabisa. Wakati wote nimeomba kuna barabara ya kutoka Shinyanga, kupitia Igurubi mpaka Igunga, na inapita inaenda mpaka Loya kwa ndugu yangu Mbunge wa Igalula. Hiyo barabara tumeomba ipandishwe hadhi mpaka leo angalau tupate barabara moja ambayo itatusaidia kwa ajili ya wananchi wa Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaongelea kitu kingine chochote, nataka niongelee barabara tu, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukimaliza Bunge hili, atume wataalam wakaangalie barabara Wilaya ya Igunga hususan Jimbo la Igunga. Kwa kweli kuna shida kubwa sana na nitaomba akiwa hapo akimaliza hii nitaenda hapo pembeni labda kesho kutwa niende kumwonesha vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba sana sitaki kusema mambo mengine nasema barabara. Barabara Igunga ni mbaya, barabara Igunga hakuna, barabara Jimbo la Igunga hakuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlionfanya kampeni Upinzani huku na huku CCM, mliona barabara hamna *mapanda du* wanasema Wasukuma, kwa hiyo ni kazi kubwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudie tena, ningeweza kusema mambo mengi, mambo ya maji lakini naomba barabara, hiki ni kilio cha wananchi na najua wanasiliza, tuna shida kubwa kweli tusaidieni. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naona majirani zangu wananiambia nizungumzie Ziwa Victoria lakini sitaki, naomba barabara, barabara, barabara, barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba barabara Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mipata jiandae Mheshimiwa Ugando.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu na nakushukuru wewe kunipa nafasi. Naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Spika, Waziri Mkuu, Wabunge wenzangu, kwa salamu za faraja mlizotupatia tulipompoteza Mama yetu mwezi wa Pili. Tulipokea msaada mkubwa sana tunashukuru sana, hasa ule mfuko wa faraja Mungu awabariki na tunamwombea mama yetu apate mapumziko ya milele. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kabisa kuunga mkono hoja na nina sababu; kwanza natambua kazi nzuri zinazofanywa na Serikali hii ambazo ni kushughulika na mambo mengi ambayo yalisuasua zamani. Tumeona wahenga wanasema kila zama na kitabu chake, ni hakika kitabu cha Awamu ya Tano kitakuwa cha pekee kidogo na upekee wake ni namna Serikali ilivyojipanga kushughulikia matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona suala la madawati lilikuwa sugu mashulenii limatepata ufumbuzi wa haraka kabisa. Tumeona ubadhirifu Serikalini umepata ufumbuzi wa haraka kabisa ingawaje unaendelea, Utumishi wa Serikali umekuwa na nidhamu, uamuzi wa kuhamia Dodoma wa haraka kabisa, umesuasua miaka mingi. Tumeona dawa za kulevyia zikishughulikiwa kwa haraka. Kwa hakika wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini wameniambia niunge mkono juhudzi zote zinazofanywa na Serikali hii kama mabosi wangu walionileta hapa kuwawakilisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajenda yetu sasa ni viwanda na katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 19, Ibara ya 28, imezungumza suala la uchumi wa viwanda. Katika uchumi huu wa viwanda, historia inatuambia mahali ambapo viwanda vilianzia kulikuwa na maandalizi muhimu sana kwanza na mojawapo ni elimu. Elimu lazima iwe na msisitizo wa sayansi na teknolojia, masomo ya kisayansi lazima yawekewe msisitizo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninavyozungumza hapa Wilaya yangu ya Nkasi, Walimu wa Sayansi wako 14 tu katika shule 22, kati ya hizo nyingine zina kidato cha kwanza mpaka cha sita. Kwa hiyo, hatuwezi kufanikiwa kama walimu wa sayansi hatuwapati, walimu wa ufundu hatuwapati, hatuwezi. Kwa hiyo, naomba tuleteeni walimu ili tushiriki katika uchumi ambayo ni ajenda yetu ya sasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hatutaweza kufanya vizuri katika kilimo. Kilimo kinahitaji elimu, kilimo kinahitaji sayansi na jinsi kilimo kinavyosukumwa katika nchi hii, niko miaka sita sasa Bungeni, sijaridhika. Naona kilimo kama kinasuasua kila siku, kinaenda ili mradi kiende, wakati kilimo mchango wake kwa pato la Taifa ni mkubwa, mchango wake kwa ajira ya Watanzania ni mkubwa na kilimo ndicho kitakachoendeleza ajenda hii ya viwanda. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uanzishwaji wa viwanda Ulaya, kitu cha kwanza ilikuwa mapinduzi katika kilimo ili kutengeneza *ready market*. Maana watu wakilima vizuri watakula chakula, watazaliana, watakuwa sasa wanunua chakula hicho, bidhaa mtakazozalisha kwenye viwanda, watakuwa na afya na nguvukazi itakuwepo. Sasa kwa nini kilimo kinasuasua miaka yote na kinabeba watu wote wanyonge? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri watu wanaopelekwa kwenye kilimo kusimamia wawe wakakamavu na hatua zichukuliwe. Kwa nini mkulima apate mbolea kwa kuchelewa? Sababu zinakuwa zinatolewa lakini zote hazitoshi zote. Naomba ufile wakati tuchukue hatua kakamavu, hasa katika suala la ucheleweshaji wa pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchezo pia katika utoaji wa pembejeo zinakuwa *fake*, wenzangu wamesema. Mwaka huu mimi ni mmojawapo wa watu walioathirika, nilinunua madawa *fake* ya kupalilia, ya magugu, jambo hili si jema sana na wasimamizi mpo, vitu hivi vinarudisha wakulima nyuma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya utafiti wa mambo ya kilimo, ukurasa wa 21; Wilaya ya Nkasi tuna Kituo cha Utafiti Mirundikwa, hakijasaidiwa vya kutosha, hakina pesa ya kutosha. Naomba tusaidiwe ili tuweze kujitahidi kupata mbegu kwa karibu, sasa hivi mbegu tunaagiza nje bila sababu za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilikuja hapa nikatoa kilio changu juu ya kunyang'anywa Shule ya Mirundikwa! Leo hii nipende kuishukuru Serikali, nimepata pesa zaidi ya milioni 259 kwa ajili ya kujenga bweni na kuendeleza madarasa. Niikumbushe Serikali, nilisema wakati ule kwamba, miundombinu iliyokuwepo wakati ule ilikuwa na zaidi ya thamani ya milioni 871 kwa mujibu wa Mthamini wa Serikali kwa hiyo, bado kuna safari ya kutosha ingawa si haba, lazima tushukuru. Ninaposema Serikali hii ikiambiwa jambo inatekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nililia hapa kila mtu aliniona, sauti yangu niliipaza, nikapata nafasi ya kumwona Mheshimiwa Rais na kumweleza kwa nafasi mbalimbali, lakini sasa napata matokeo chanya. Sasa kwa nini niseme hafanyi kazi? Kwa nini niseme hashughulikii matatizo ya wananchi? Nitakuwa mtu wa ajabu sana. Kwa hiyo, anafanya kazi vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa katika maeneo niliyoyasema waangalie, Mawaziri watusaidie. Waziri wa Elimu upungufu wa walimu kwangu ni 647, hatuna walimu 647. Upungufu wa nyumba na vyumba vya madarasa ni 1,100. Upungufu wa nyumba za walimu 900, ni mkoa na wilaya iliyo pembezoni kabisa! Mtutupie macho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho Mji wa Namanyere umeshakua vya kutosha, tunaomba uwe ni Halmashauri ya Mji. Mheshimiwa Malocha amekuwa akizungumza upande wake na wenywewe huko. Hiyo inatakiwa iwe wilaya ni sehemu kubwa. Mwisho zaidi tunaidai *NFRA* zaidi ya milioni 200 kwenye Halmashauri yetu. Halmashauri yetu sasa haiwezi kufanya kazi kwa sababu, mapato hayatoshelezi. Kwa hiyo,

kama mtatusaidia mtusukumie hili jambo liwezekane ili Halmashauri ipate nguvu na uwezo wa kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu wote waliozungumzia juu ya asilimia 10 kwamba, hazitoki. Kama kuna mtu aliziona basi labda ni kwa sababu kwetu hazitoki. Tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba asilimia 10 zinatoka ili ziende kwa vijana na akinamama kwa mwaka huu. Kwenye bajeti ya mwaka huu zimeingizwa, lakini sasa tulikuwa hatuzipati na hatuzipati kwa sababu ya mapato machache ya Halmashauri, wanaona vipaumbele wanavyokuanavyo vinawafanya wasizitumie pesa hizi kupeleka kwa vijana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia wanamsifu sana Mheshimiwa Mavunde. Hiyo habari yako ya mikopo kwa vijana kuwezesha vikundi mbalimbali kwetu haijafika. Tusaidie au tupe namna ambavyo tutaweza kushiriki twende kwa pamoja na wenzetu ambaao wanasifia kwamba unafanya vizuri katika eneo hili. Binafsi, kwangu mimi bado elimu haijafika na vijana wangu wote ni wachapa kazi wanahitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niongelee suala zima la uchapaji kazi, kama ilivyo Serikalini muangalie na kwenye kilimo. Kilimo, kuna watu wanajita wakulima, lakini ni wazururaji tu na hakuna mtu anayewaangalia! Hili haiwezi kutuletea tija! Wasimamizi, hasa watawala, tujitahidi kuhakikisha kwamba, kila mtu katika eneo lake awe anafanya kazi inayotambulika na kufanya kazi kwa bidii kwa masaa mengi. Isiwe kama ni ajenda ambayo haina msimamizi; tutakuwa tunazungumza kila wakati kwamba tunaondoka hapa tulipo kiuchumi, kumbe tunafuga watu ambaao...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ugando, jiandae Mheshimiwa Yusuf Kaizer Makame.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi leo nichangie hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote itabidi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili nichangie hotuba hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja; sababu, hotuba hii imejali maslahi ya wananchi wa vipato vya aina zote. Pili, niweze kumshukuru kwa kazi nzuri anayofanya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Baraza lake kwa ujumla. Hii kauli ya Hapa Kazi kwa kweli inaonekana kwa vitendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yangu ya Kibiti takriban Mawaziri watano wamefika ndani ya mwezi mmoja. Hata wananchi wa Rufiji kwa ujumla wamesema kwa kweli Serikali hii ya Awamu ya Tano inakwenda na wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa katika afya. Nashukuru kwamba Idara ya Afya imetugawia kila kituo shilingi milioni 10 ambazo tumekarabati, kila penye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto. Tuna upungufu mkubwa wa watumishi katika Idara ya Afya. Kuna baadhi ya zahanati ina watumishi mmoja-mmoja ikiwemo Kiomboni, Kechuru, Msalale...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hebu badilisha hiyo *microphone* nenda sehemu nyingine.

**MBUNGE FULANI:** Mwambie ndivyo nilivyo.

**MWENYEKITI:** Aah *ok*, basi endelea.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndivyo nilivyo. Nikupe taarifa tu nina kigugumizi, nina kilema ambacho amenipa Mwenyezi Mungu, hata hii *mic* ukii badilisha hutaweza kunibadilisha, haya ni maumbile aliyonipa Mwenyezi Mungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee suala la kilimo. Wananchi wangu wa Jimbo la Kibiti bado wanalima kilimo cha *Nungu abile*, yaani ina maana Mungu yupo, watu wanalima ili kusubiria mvua wakati sasa hali ya hewa imebadilika. Ninachoomba Waziri anayehusika atuletee miundombinu ya umwagiliaji Kibiti ili wananchi walime kilimo chenye tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unavyozungumzia kilimo chenye tija kwa sisi wananchi wa Kibiti lazima tuzungumzie masuala ya korosho. Korosho bado Chama Kikuu cha Msingi kina matatizo, kwa sababu wananchi wanalima korosho zao, wanapopeleka katika hayo masoko bado makato yao yanachukua muda mrefu katika kulipwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala zima la elimu. Tunafahamu Serikali yetu imeweka mfumo wa elimu bure, lakini kila penye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto, katika Wilaya yangu ya Kibiti kuna upungufu mkubwa hasa wa watumishi, majengo na nyumba za walimu. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu huu ni upungufu iliangalie Kibiti kwa jicho la huruma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Benki ya Maendeleo ya Akinamama; sote tunafahamu bila ya akinamama hatuwezi tukasonga mbele. Hawa akinamama lazima tuwaboreshee mazingira yao kwa sababu muda mwingu wa nyumbani akinamama ndio wanalea familia. Tuna kila sababu ya kuangalia kwa jicho la huruma ili katika vile vikundi vyao wapewe mikopo ya bei nafuu. Jambo la kushangaza ni kwamba benki hizi zimekaa mijini tu, je, kule vijijini watafika lini ili na kule akinamama wetu wa vijijini nao wakafaidike? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie na suala la miundombinu kwa sababu, barabara yetu ya Bungulu kwenda Nyamisati haipitiki. Tunaomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aiangalie barabara hii kwa sababu

barabara hii inafaidisha wananchi wa Kibiti na wananchi wa Mafia kwa ujumla. Mbali ya barabara upo ujenzi wa Gati – Nyamisati, ujenzi huo wa Gati Nyamisati likirekebishwa naamini kwamba wananchi wa Mafia na wananchi wa Kibiti watafaidika na gati hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie kwamba, Wilaya ya Kibiti ina Kata 16, lakini ziko baadhi ya Kata ziko *Delta*. Kwa hiyo, *Delta* iangaliwe kwa jicho la huruma kwa sababu miundombinu ya *Delta* siyo rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga hoja asilimia mia kwa mia. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Yussuf Kaizer Machame na Mheshimiwa Mbarouk Salim Ally.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, pili nakushukuru wewe kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Kabla ya kusema chochote naomba kwanza niunge mkono Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Ofisi hii ya Waziri Mkuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda kwenye maeneo matatu mpaka manne. Suala la kwanza nitazungumzia masuala ya *general/ya Bunge*, nitazungumzia *unit* ya *Bunge Sports*, nitazungumzia masuala ya misaada ya Wahisani kwa Serikali ya Tanzania, nitazungumzia Ofisi ya Msajili kwa sababu hii haiwezekani kutokuizungumza kwa yejote anayesimama upande huu kwa sasa inavyotekeleza majukumu yake, lakini na nne kama nitapata muda nitazungumza suala la uanzishwaji wa Baraza la Vijana la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye *issue* ya Bunge. Mimi ni Mbunge wa awamu ya kwanza hii 2015/2020,

wakati tunakuja hapa kwenye *briefing* ya kuapishwa mwezi wa Novemba, 2015 nilidhani kwamba Bunge linaloyasema linayasimamia. Tuliambiwa kwamba *issue* ya vitabu itakuwa mwisho kwenye meza zetu Mkutano ujao kwenye Bunge hili tuliloanza. Mwezi Novemba, tuliambiwa maneno hayo na Spika wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio yangu ni kwamba, sasa hivi sisi tungekuwa tunatumia zile *computer* mpakato. Hizi siyo kwa mantiki ya kujonesha sisi tunatumia ni kwa usiri wa siri za Serikali, nyaraka hizi ni muhimu na kila kitu, lakini mpaka leo tunaenda mwaka wa pili, lile neno baada ya kulisikia kwenye *Briefing* ya Bunge halijawahi kuzungumzwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kuhitimisha haya makabrasha yanajaa humu, hebu tujitahidi basi, kwenye hili atakapokuja kuhitimisha atuambie Bunge letu linaenda *electronically technological whatever!* Atambie tunaenda kwenye *computer* mpakato au tunaendelea na hili mpaka tumalize Bunge hili la 11? Hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka kuzungumza kwenye maslahi ya Wabunge. Wabunge kituo chao cha kazi ni Dodoma na ndiyo mmeamua kwamba, kituo cha kazi kiwe Dodoma. Wabunge wanapotoka Majimboni wanakuja Dodoma asilimia kubwa ya Wabunge ni watu wanaoishi katika hoteli ama *Guest* hapa Dodoma.

Tunapotoka kuja hapa tunapanga kwenye vyumba vyetu vya hoteli, sasa tukitoka kwenda kukagua miradi ya maendeleo ya Serikali tunakuwa tayari tumeponga kwenye vyumba vya hoteli, lakini bajeti tunayotengewa ni ile ya kukaa Dodoma. Kwa hiyo, kimsingi kwenye hili tuache itikadi zetu za vyama na mambo mengine, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunahitaji stahiki za mtu anayetoka kituo chake cha kazi kwenda sehemu nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu tu kwa sababu tukienda Geita, huku tuna chumba, kule tuna chumba, *cost zinaongezeka, otherwise mliangalie kwa namna nyingine suala hili kwa ajili ya Wabunge.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Bunge Sports Club*, limeongelewa sana. Tataliongelea kwa umuhimu wake, hasa mwaka huu ambao tutapokea ugeni. Ninayeongea ni mchezaji wa *Bunge Sports Club* wa kutegemewa tena. Sasa tuliyoyapata hatutarajii tuyaoone tena. Tunakushukuru Waziri Mkuu kwamba mambo yetu yamekua vizuri Kurwa ametoka kama Doto alivytoka, lakini ilikuwa ni kusuguana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni stahiki zetu kama Wabunge hatuombi. Tunapotoka nje ya nchi ni stahiki zetu tunazopaswa kulipwa siyo kwamba ni maombi au ni huruma ya Bunge kutufanyia hivi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba sasa tunapanga bajeti hapa, mara nyingi tukiongea na Spika anasema bajeti mliipitisha ninyi na nini. Tuliangalie kwa kina suala la *Bunge Sports Club* hasa tukitilia umuhimu kwamba mwaka huu tutakuwa na ugeni wa *East Africa* kwenye mashindano hayo ya *East Africa*, pia Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye Mwenyekiti wa *East Africa*. Kwa hiyo, itakuwa aibu kuja kuyapata yale tuliyoyakuta Mombasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine, walisema akina Mheshimiwa Cosato Chumi hapa kwamba tulikuwa tunaingia kwenye magari ya Askari! Wabunge! Wanatushangaa Wakenya, eeh! Wewe Mbunge kweli? Kwa hiyo, tunataraja mambo haya myarekebishe yakae vizuri, kwa sababu tukipata aibu Wabunge wa michezo linapata aibu Bunge na linapata aibu Taifa kimsingi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilisema nitazungumzia ni suala la misaada. Wakati Serikali hii inaingia madarakani mlikuwa mnazungumza kwa kina kwamba tutaenda kwenye kujitegemea na suala la misaada halitakuwa muhimu sana kwa Serikali hii. Tumemaliza mwaka huu wa bajeti asilimia 30 ya bajeti ya maendeleo ndio iliopatikana na sababu zilizoandikwa kwenye mpango ni mbili tu; kubwa kwamba kuchelewa kwa mazungumzo ya wahisani ambayo kwa kumwambia Mbunge mwenye akili kama mimi hiyo haiingii akilini ndio iliyoandikwa kwenye mpango wa bajeti 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwamba miradi ya maendeleo iliyoandikwa haikukidhi vigezo. Kwa hiyo, ilikuwa haina maana kwangu, sio hoja za kimantiki zinazoingia kwa Mbunge; tuangalie kwa kina kwa nini Serikali yetu ilikosa misaada na fedha za bure kama za *MCC*, za bure kabisa. Tuangalie kwa kina tusitoe hoja dhaifu kama hizi kwenye vitabu vyetu vya maandishi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Msajili; suala la Msajili limezungumzwa vizuri kwenye hiki kitabu cha Bunge cha Kamati ya Katiba na Sheria. Hii ni taarifa ya Bunge imeiagiza Ofisi ya Msajili ukurasa wa 30 imeiagiza Ofisi ya Msajili kwamba ifuate sheria, taratibu na kanuni. Kwa maana ya kwamba Bunge limeona kwamba Ofisi ya Msajili inakiuka sheria na taratibu hasa kwenye mgogoro wa Chama cha Wananchi *CUF* na suala la kutolewa kwa ruzuku isiyofuata utaratibu wa kiserikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala hili limeleta mjadala; msidhani kwamba hapa tukijadili tunafurahishana, Watanzania wanaona *what is going on* kwenye *CUF*. Huu mgogoro wanaujuwa *what is going on*, nini kilichopandikizwa na nini kinachofanywa. Lipumba humu ana genge lake la watu wawili tu *and we are forty MPs from CUF*. Hatuungi mkono kwa Lipumba, *why tunafanya hivi vitu?* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili suala ni la kuangaliwa kwa kina na Ofisi ya Msajili siyo Ofisi ya kutoa

haki kama mtu amefukuzwa anaenda mahakamani na huko  
ndio kwenye kutoa haki wala hawezi ku... (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Yussuf.  
Mheshimiwa Mbarouk Salim Ally.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
nashukuru...

**MWENYEKITI:** Jiandae Mheshimiwa Pascal Haonga

**MHE. MABROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
nashukuru kwa fursa hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru  
Mwenyezi Mungu kunijalia fursa hii ya kuweza kuchangia  
katika hoja hii ya bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze  
kiongozi wangu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (*CUF*)  
kwa ziara ambazo anaendelea kuzifanya za kuimarisha  
chama katika visiwa vya Unguja na Pemba na Tanzania kwa  
ujumla. Lakini pia nimpongeze kwa hotuba yake ya tarehe  
tisa pale Lamada *hotel* Dar es Salaam kwa kweli ilikuwa  
hotuba nzuri sana, nampongeza sana Mwenyezi Mungu  
amjalie na amfanyie wepesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema  
kwamba *Inna-Lillahi Wainna-lhayhi Rajiun* na nasema hivyo  
kwa sababu mwelekeo wa nchi yetu kwa kweli unasikitisha  
sana. Unasikitisha kwa sababu inawezekana tunacheza na  
Mungu; binadamu hatakiwi kucheza na Mungu, tunacheza  
na Mungu na kwa sababu mwanzoni katika kipindi cha  
kampeni tulikuwa tunaomba sana dua tunawaomba  
Watanzania watuombee dua na Watanzania wamefanya  
hivyo na viongozi wa dini wote wamefanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapomwombwa  
Mwenyezi Mungu akusaidie na akakusaidia, lakini badala  
yake ukarudi sasa ukafanya mambo ya kimaajabu ajabu ya  
kutesa watu, kunyanyasa watu na kudhulumu watu kwa kweli

hapo Mwenyezi Mungu anakuwa hayupo. Kwa hiyo, hili jambo la kucheza na Mungu ni baya sana na hili halitotupeleka pazuri Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana kwamba hakuna linalokwenda, hali ya uchumi ni mbaya, hakuna ajira, kila linalopangwa halienda na hapa tulifanya fanya tu kidogo kwa sababu kulikuwa na pesa za kuokota za madawati ndio ikaonekana kwamba tulijitahidi tukafanya kidogo lakini hakuna lolote ambalo linafanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye *issue* ya Muungano; Waziri Mkuu katika hotuba yake amesifu sana vikao vinavyofanyika baina ya SMT na SMZ kuhusu kero za Muungano. Niseme tu kwamba kwa kweli tumechoka na kuona idadi ya vikao; wananchi wameona idadi ya vikao vinavyofanyika baina ya SMT na SMZ lakini hatuoni matokeo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Muungano sio wa viongozi, sio wa Mawaziri; waasisi wa Muungano walikusudia kwamba Muungano ni wa watu wa Zanzibar na watu wa Tanganyika. Sasa inapotokea kwamba kuna vikao vinakaa lakini haijulikani linalotatuliwa wala linalozungumzwa hilo ni tatizo na hatuwezi tukaenda hivyo kwa sababu kero zipo pale pale. Kila siku vikao 13, 16, 20 lakini huoni jambo ambalo linatatuliwa, kwa hiyo hili ni tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha zaidi ni kwamba hata zile mamlaka ambazo zinahusika na zile kero ukienda wanakwambia sisi hatujui, kama wametatua, wametatua wao juu. Sasa wanasiasa tunatatua kero lakini watendaji hawajui; kwa hiyo kero zinabaki zipo pale pale. Kwa hiyo, hili kwa kweli halitendeki vizuri hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni kuhusu Msajili. Kwa kweli hatuwezi kuidhinisha pesa kwa ajili ya kwenda kufanya au kutumia mtu anavyotaka. Kama hatukupata maelezo mazuri ya Ofisi ya Waziri Mkoo ya pesa milioni 369 zilivyotumika kwa kweli hapa

patachimbika, hatuwezi kuruhusu hiyo kitu, kwa sababu tunakaa hapa tunaiddhinisha pesa kwa matumizi ambayo tunakubaliana halafu anatokea mtu tu wakati yeye mwenyewe ameshaandika barua kumpelekeea Katibu Mkuu wa CUF kwamba Chama cha Wananchi CUF kwa sababu ya mgogoro tunakizua ruzuku. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa iweje tena urudi uipitishe ruzuku kwa mtu ambaye ameshafukuzwa, sio mwanachama lakini pia ruzuku hiyo hiyo ikatembea mpaka kwenye akaunti za watu binafsi, hatuwezi kufanya upumbavu wa aina hiyo. Kwa kweli hatukubali; hii ni lazima tupate maelezo ya kutosha na vinginevyo hatuwezi kupitisha hii bajeti, lazima pachimbi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo llingine ambalo nataka nizungumzie ni kuhusu Mfuko wa Jimbo hususan kwa sisi Wazanzibari. Pamoja na kwamba Mfuko wa Jimbo bado pesa ni ndogo sana yaani pesa ambazo zilikuwa zinatolewa kwa idadi ya watu kidogo sana ndio zile zile mpaka leo haubadilili; naifikiri kuna mjumbe mwenzangu aliwahi kusema hilo. Lakini tatizo kubwa la Zanzibar hizi pesa zinachelewa sana; ile Serikali yenu ya Zanzibar inazikopa pesa kwa sherehe za Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila zikitolewa Disemba wanazichelewesha mpaka Juni ndio pesa tunazipata. Tunashindwa kufanya mambo ambayo tumeahidi kufanya sasa naomba patafutwe utatuzi wa tatizo hilo, sio mara moja mara mbili wala mara tatu, kila siku pesa hizi zinachelewa. Wenzetu huku wanatumia pesa wanamaliza sisi bado kule tunaulizia kila siku; tumechoka kuja kuulizia pesa hii. Hili jambo hebu litafutiwe ufumbuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nataka nizungumzie kidogo kuhusu Bandari ya Wete. Bandari ya Wete pana kaofisi kidogo kabanda tu; hicho hicho wanatumia wavuvi na hilo hilo wanatumia wasafiri na hilo hilo wanatumia Ofisi ya Uhamiaji. Kwa kifupi ni kwamba pale pana *movement* kubwa sana ya wasafiri baina ya Pemba na Mombasa Kenya

lakini kuna tatizo kubwa hakuna Ofisi ya Uhamiaji, forodha wala Ofisi yoyote. Kwa hivyo, inawezekana kuna upotevu mkubwa wa mapato. Namwomba Waziri Mkuu hili jambo tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika awamu iliyopita ilisemekana kwamba pesa za ujenzi wa Ofisi pale tayari zilishatoka kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini la kusikitisha mpaka leo hatujaona lolote ambalo limetendeka. Hili Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba tulipatie majibu sijui limefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Pascal Haonga, ajiandae Mheshimiwa Sokombi.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuchangia hii hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote niweze kwanza kumpongeza Rais mpya wa *TLS* ndugu yangu Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu kwa kuchaguliwa kwa kura nydingi sana. Kwa hiyo, pungezi sana japo kuuwa mchakato huu ndugu yangu Mwakyembe alitaka kuingilia, bahati mbaya akawa amelemewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naomba sasa niweze kujikita kwenye hotuba ya Waziri Mkuu na naomba nianze na suala moja la wakulima wa zao la kahawa. Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati yupo kule kusini alifanya mambo mazuri sana kwenye suala la watu wa korosho akapunguza tozo kwenye korosho na mambo mengi sana, lakini kiukweli kabisa amewasahau wakulima wa zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Mbozi pamoja na Mkoa wa Songwe na Mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wanaolima kahawa wana maeneo mengine wanasema kwamba kama Waziri Mkuu hatapunguza tozo na kodi kwenye zao la kahawa maana yake Waziri Mkuu atakuwa ameonesha upendeleo wa hali ya juu sana na

atakuwa amefanya ubaguzi ambao kwa kweli hatutegemei kuuona. Wao pia wanasema kwamba amefanya hivyo kwa sababu kule ni nyumbani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakulima wa zao la kahawa wanasema kwamba wanategemea kusikia atakapokuwa anahitimisha na hapa nimepokea meseji kama 200 hivi kutoka Jimboni kwangu; wanategemea kusikia anapunguza kodi na tozo mbalimbali kwenye zao la kahawa. Zipo tozo nyingi sana; kuna ushuru Bodi ya Kahawa, iko tozo kwenye *TaCRI* na iko tozo kwenye Halmashauri kule asilimia 0.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wanaomba tafadhali suala hili Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kulichukulia kwa umakini sana maana kule kwake nadhani ameshamaliza sijui ndio alikuwa anatengeneza mazingira lakini kwa kusema ule ukweli kwenye mazao mengine kama kahawa nahitaji kuona anapunguza tozo na kodi mbalimbali kwenye zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwetu Mbozi kahawa ndio dhahabu yetu; kahawa ndio kila kitu, mtoto anapokwenda shule lazima unaangalia kwenye kahawa na mtoto anapotaka kuoa unaangalia kwenye shamba la kahawa, kila kitu kahawa. Kwa hiyo, tafadhali suala hili ajaribu kuliangalia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu wakulima wetu wa kahawa sasa wamefika mahali wamekata tamaa na wameanza kung'oa Miche ya kahawa kwa sababu bei kwanza ni ndogo na hizo tozo na kodi zimekuwa nyingi hivyo wanategemea atatoa majibu mazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu kama hatozungumza lolote kuhusu kahawa mimi na Wabunge wengine tunaotoka kwenye Majimbo na maeneo wanayolima kahawa tutahamasishana kuwaleta wote hapa Dodoma ili waje kupewa majibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kuzungumzia kidogo suala la maafa amegusa kwenye

ukurasa wa 48. Suala la maafa tunajua ndugu zetu wa pale Bukoba tetemeko lilitokea wakapata matatizo makubwa sana. Cha kusikitisha Rais wa nchi hii amechukua muda mrefu kwenda pale kuwafariji wananchi wale. Kibaya zaidi zipo fedha ambazo zilichangwa bilioni sita kutoka EU na lakini ziko pesa ambazo tulikatwa hapa Bungeni kwa ajili ya ndugu zetu wa Bukoba, hizi pesa zimeliwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujui hatujaambiwa hadi leo lakini inaonekana fedha hizi zimepigwa. Tulifanya mechii pale Dar es Salaam uwanja wa Taifa; Wabunge tumecheza mechii hadi miguu imeuma, tumepata zaidi ya milioni mia mbili na kitu pesa hizi zinaonekana kama mmeshazipiga. Sasa hatujui kwa nini watu wanapata matatizo badala ya Serikali kuchukua fedha zile kuwasaidia, mnaamua kuzitumia kinyume na matarajio, kinyume na ile kazi ambayo tulikuwa tunategemea zifanye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kabisa kwamba pale wananchi wanapopata matatizo, Rais wa nchi, Serikali iweze kutoa lugha nzuri. Leo kama Rais wa nchi anasema mimi sikuleta tetemeko, hatutawasaidia chakula ina maana kwamba Taifa hili tumekosa Rais. Nadhani suala hili tujaribu kuliangalia sana. Naomba niwe muwazi kabisa kwamba Rais wetu lugha anazozitoa watu wanapopata matatizo...

## KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** utaratibu

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Hujaruhusiwa naomba ukae Simbachawene kwa sababu hujaruhusiwa. (*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ameruhusiwa, Mheshimiwa Pascal kaa chini.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Simbachawene tumeambiwa tusiingiliane, naomba ukae basi hujaruhusiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pascal kaa chini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba Mbunge anaeongea ni Mbunge mgeni na kwa hivyo anaweza akawa hazifahamu vizuri kanuni. Kanuni inasema haturuhusiwi humu ndani na naomba niinukuu haturuhusiwi humu ndani kuzungumzia mwenendo wa watu fulani fulani. Sasa naomba nisome ile kanuni aliyoivunja katika kifungu cha 64 cha kanuni zetu inasema

"Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100, ibara inayolinda na kuhifadhi uhuru na mawazo au majadiliano katika Bunge:-

(e) Mbunge hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwengine yeoyote anayeshughulikia utoaji wa haki isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahsusii kuhusu jambo husika." (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hii iko very *clear*: tukitaka tuzungumzie *personality* huruma ya mtu, tukitaka tuzungumzie namna mtu anavyofanya mambo, tunakuwa tunaingilia uhuru wa watu wengine pia na kanuni hii inakukataza hivyo hata kwa Mbunge mwenzio. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Kwa sababu hiyo basi namwomba Mheshimiwa...

**MWENYEKITI:** Amekuelewa ahsante.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Bado sijamazilia na kwa sababu hiyo basi namwomba Mheshimiwa Mbunge aondoe maneno hayo katika kauli yake.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anatumalizia muda wetu naomba akae tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimwa Pascal kama ni Mbunge mgeni hujui kanuni...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Nimeshakuwa mwenyeji tayari maana yake ni muda mrefu sasa...

**MWENYEKITI:** Nimeshaelewa sasa hiyo ni kadi ya njano umepewa, tuendelee.

**MHE.PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba, mara ya kwanza ulisema kuwa hutatoa taarifa yoyote ila nasikitika umetoa taarifa kwa huyo bwana. Labda inawezekana ilikuwa kasoro kwa Simbachawene tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo nililokuwa nalizungumza hapa ni kwamba watu wanapopata matatizo wananchi wakipata maafa, Serikali inatakiwa ikae karibu na wananchi. Sasa kama Serikali fedha zinachangwa inafika mahali fedha zile zinatumika kinyume ni lazima tuhoji, lazima tuulize. Sasa leo hii tusipouliza unategemea nani atauliza suala hili sisi ndio tunaowakilisha wananchi; tumekaa hapa huu ni mukutano wa hadhara wa wananchi nchi nzima hawawezi kukusanyika wote hapa. (*Makof*)

## **TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Mbunge, mimi ni Waziri ambaye nasimamia masuala ya maafa nchini. Si kweli kwamba fedha tulizopokea kutoka Ubalozi wa Uingereza fedha zile zimeliwa na Serikali, hiyo sio kweli na fedha zile zimetumika kujenga Shule ya Sekondari ya Ihungo na akienda leo na nitakapokuwa nahitimisha hoja hii Mheshimiwa Waziri Mkuu na Ofisi yake tutawaeleza Wabunge kazi nzuri iliyofanywa na Serikali katika kurudisha miundombinu ya Serikali katika Mkoa wa Kagera. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge kama hana taarifa za matumizi ya fedha hizo asifanye *generalization* kwamba fedha hizo zimeliwa na Serikali, taarifa hiyo sio sahihi na Serikali haijala fedha hizo na kazi iliyofanyika kule imefanyika na inaonekana. Kwa hiyo naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge asipotoshe umma wa Watanzania kwamba fedha hizo zimeliwa na Serikali. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, *no research, no right to speak.*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa!

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Simbachawene amesoma Ibara ya 64 kuhusu suala la kujadili mwenendo wa Rais, lakini kama wote tunavyoja, kipengele alichokisoma kinazungumza kwamba bila kuathiri Ibara husika ya uhuru wa mawazo, Katiba iko juu inayompa uhuru mwananchi wa Tanzania kuzungumza bila kubugudhiwa na mtu yejote. Kipengele anachokisema kinaeleza wazi, bila kuathiri Katiba mama, uhuru wa mawazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo anachozungumza huyu haathiri uhuru wake wa kujadili mawazo, kwa hiyo kipengele alichosema Mheshimiwa Simbachawene kinatufunga kwenye Katiba mama ambayo inaturuhusu kujadili na anachokijadili ni kujadili maendeleo ya nchi na sisi ndio wawakilishi wa wananchi. Kama kiongozi hafanyi vizuri, tuna haki ya kujadili na ndio uhuru tunaopewa. Kwa hiyo naona anapotosha Bunge kwa kusema kile kipengele kinatuzuia... (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kaa chini, Mheshimiwa Simbachawene kaa chini, Mheshimiwa Pascal endelea. (*Makof*)

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uweze kulinda muda wangu na najua bado nina dakika kama saba hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kuzungumzia suala lingine, suala ambalo Waziri Mkuu amelizungumzia kwenye ukurasa ule wa 11 kuhusu kufanya siasa za kutuunganisha badala ya kufanya siasa za kutugawa. Naomba sitanukuu sana kile alichokisoma pale Waziri Mkuu, naomba niseme tu kwamba nchi yetu ilipofikia siasa za kuwagawa Watanzania zimeasisiwa na Mwenyekiti wa CCM Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siasa hizi zimeasisiwa juzijuzi hapa kwenye vyombo veya habari, imeripotiwa tu Mwenyekiti wa CCM Taifa anasema kwamba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ni marufuku kwenda kumwona Mbunge mwenzao Mheshimiwa Godbless Lema aliyekuwa amewekwa ndani. Siasa hizi za kutugawa Watanzania...

### **TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** ...Ni siasa ambazo kwa kweli tukiziangalia hazitufikishi popote pale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pascal, kaa chini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Mbunge, anachotaka kufanya hapa ni kucheza na lugha za kisiasa kuwapotosha tu Watanzania kwenye maneno anayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge; Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi anayo nafasi yake ya kukaa na Wabunge wake wa Chama cha Mapinduzi wakati wowote lakini atakayetoea taarifa za mjadala wa kikao cha Mwenyekiti wa Chama na Wabunge wake wa chama ni mamlaka zinazohusika ndani ya *caucus* ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na sio mtu mwininge ye yeyote. Sasa naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa Mbunge hayo aliyoyachukua huko sisi hatuyajui na asituletee humu ndani... (*Makofî*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Kama ni

mambo ambayo yalijadiliwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo naomba kumpa Taarifa, tunaendelea kuwa na vikao vyetu...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** ...lakini vikao vyetu vya kikanuni ambavyo vinakidhi maslahi ya Wabunge wa chama na maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania ya kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pascal...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya, kaa kwanza. Kaa Mheshimiwa Bulaya. Mheshimiwa Bulaya unadharau mamlaka ya Kiti?

Mheshimiwa Haonga, kuna hoja muhimu sana mbele yetu ya maendeleo ya wananchi ambayo yanafanywa vizuri sana na Serikali hii. Wewe ni wajibu wako kuhoji maji, barabara, shule kwenye kambi yako...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** ...unapotaka kuleta mambo ambayo huyajui, unapotaka kuleta mambo ya vyama vingine ambavyo wewe si mjambe wa vyama hivyo na unapotaka kuleta mambo ya mitaani ambayo humu ndani hamna utajitia katika matatizo makubwa sana. Nakuomba, umesamehewa mara ya kwanza kwa sababu ni Mbunge mgeni, wakilisha wananchi wako kwa hoja za msingi za maendeleo ya jimbo lako. Mambo ambayo hayakuhusu yaache hukohuko yalipo. (*Makofii*)

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ulinde muda wangu na naomba niseme kwamba ninachochangia hapa sichangii kitu ambacho hakipo, nachangia Hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wale ambaao labda hawajasoma hotuba hii vizuri wangepata muda waweze kusoma vizuri, hapa kwenye ukurasa wa 11 amezungumza vizuri sana Waziri Mkuu, kwamba tufanye siasa za katuunganisha badala ya kufanya siasa za kutugawa na nilichokizungumza mimi, siku ambayo Mwenyekiti wa CCM Taifa amewaasa baadhi ya Wabunge wasiende kumtembelea Mbunge mwenzao vyombo vya habari vilitangaza, magazeti yaliandika, Kituo cha Utangazaji cha TBC kilitangaza, *ITV* walitangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa nashangaa sana, labda inawezekana kuna wengine ambaao inawezekana hawafuatilii vyombo vya habari, labda hawajasoma na Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, naomba tafadhali usiingie kwenye mtego, hii Hotuba ya Waziri Mkuu naichangia vizuri sana, hii ninayo hapa, ni ukurasa ule wa 11. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba nizungumze; wapo ndugu zetu wengi ambaao walifukuzwa siku za hivi karibuni Msumbiji, Mheshimiwa Waziri Mkuu nadhani anakumbuka na Wabunge wote mnakumbuka kwenye Bunge hili. Wale Watanzania wamefukuzwa Msumbiji wamepelekwa mpakani pale wengine wamepoteza maisha, wengine wamebakwa. Rais wa nchi, naomba niseme tu kwamba kiongozi mkuu wa nchi, maana yake mmesema tusimtajetaje, sijajua tatizo ni nini, anasema kwamba walikwenda kwa njia za panya warudi kwa njia za panya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea viongozi wetu, watu wetu wanapopata matatizo tuwe wa kwanza kwenda kuwasaidia, tuwe wa kwanza kwenda kuwatia

moyo. Watanzania wengi wanaoondoka nchini hawaendi nchi za huko mbali kwa ajili ya kwenda kutalii, wanatafuta maisha, wanatafuta fursa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkuu wa mkoa alipojaribu kupeleka hata gari lile la jeshi kwenda kuwabeba wale watu alikatazwa akaambiwa kwamba usiwabebe, waache kama walivyo, walikwenda kwa njia za panya warudi kwa njia za panya. Suala hili kwa kweli linasikitisha sana na kwa jinsi hali ilivyo kwenye nchi yetu kama tutaendelea kwenda hivi, mimi naamini kabisa kwamba tutakuwa hatuwatendei haki Watanzania ambao wametuchagua sisi Wabunge na ambao wamemchagua Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na ambao wametuchagua sisi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba tu kwamba ifike mahali sisi viongozi ambao ndio tumaini la Watanzania tufanye kazi ya kuwawakilisha wananchi wetu vizuri na tufanye kazi ya kuwatetea, tufanye kazi ya kuwasemea, lakini inapofika mahali unasema kwamba sikuwatuma mimi kwa kweli hatuwatendei haki hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze suala lingine ambalo linapatikana ukurasa ule wa 21 wa Hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu ziada ya chakula ambayo amelzungumza kwenye hotuba hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu anafahamu yeye na Wabunge wote wanafahamu kwamba takribani halmashauri 55 zina tatizo la njaa japokuwa sasa hatujaambiwa, hatujaletewa taarifa rasmi Bungeni kwamba kwa sasa tumefikia wapi, lakini taarifa iliyokuwepo siku za nyuma ni kwamba halmashauri 55 zina njaa. Imefika mahali tunaambiwa kwamba chakula hakitapelekwa, sasa watu waliotuchagua leo tu...

**MWENYEKITI:** Nakuongeza dakika moja!

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, dakika zangu nadhani umenipunja kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nizungumze tu kwamba sasa tuulize, wakati Watanzania wanapata njaa kipindi cha Nyerere alikipata wapi chakula cha kuwapelekea, wakati Watanzania wamepata njaa kipindi cha Mkapa, kipindi cha Mwinyi, kipindi cha Kikwete, chakula kilitoka wapi na hii Serikali leo kwa nini inashindwa kuwapelekea Watanzania chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la njaa halina baunsa, mtu yejote anaweza akapata njaa kutokana na kwamba inaweza kuwa mvua labda haijanyesha, kumetokea ukame, kumetokea matatizo mbalimbali, sasa leo Serikali inasema kwamba sisi hatutapeleka chakula kwenye maeneo ya njaa, hii ni fedheha kubwa sana kwa Taifa letu na nina...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sokombi, jiandae Mheshimiwa Chegeni, Mheshimiwa Mayenga, Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Bashungwa.

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, *please* kaa chini.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigwangalla, *please* kaa chini.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu, pili nipende kumshukuru pia Mwenyekiti wangu wa Chama cha CHADEMA na nipende kumpongeza kwa hotuba yake nzuri iliyoletwa hapa Bungeni yenye kuonesha dira na m dororo wa uchumi wa Tanzania juu ya bajeti yetu iliyoletwa hapa Bungeni. Bajeti iliyoletwa hapa Bungeni ni bajeti hewa, na nitaendelea kusema kwamba ni bajeti hewa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu moja. Ukiangalia Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ukurasa wa 35, kwenye Wizara ya Kilimo, zimetengwa asilimia 2.22, Wizara ya Viwanda na Biashara imetengwa asilimia nane, Wizara ya Afya asilimia 25. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hii asilimia 25 unazipenda kweli afya za Watanzania, maana hii asilimia 25 ndiyo imebeba maisha ya afya zote za Watanzania juu ya matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kwa kuchangia juu ya hii Wizara ya Afya; Serikali ya CCM iliahidi kujenga zahanati kwenye kila kijiji na kata na vituo vya afya. Swalii la kuijuliza; kwa bajeti hii ya asilimia 25 fedha hizi zitakidhi kweli vigezo vya afya katika Tanzania yetu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika Mkoa wangu wa Mara, Hospitali ya Mkoa wa Mara ni jambo la kusikitisha na ni aibu, tena mahali ambapo anatoka Baba wa Taifa, hospitali haina hadhi kwamba ni hospitali ya mkoa. Mfano mdogo, *CT scan*, ile hospitali haina *CT scan* na mtu akitaka kufanyiwa hicho kipimo ni mpaka wampe rufaa kwenda Bugando, Mwanza na Bugando hiki kipimo hakipo, hakipo Bugando wala Sekou Toure, ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipimo cha *CT scan* kipo kwenye hospitali moja tu tena ni *dispensary* ya mtu binafsi, inakuwaje mtu binafsi anaweza kununua hii mashine lakini Serikali inashindwa, ni jambo la kuijuliza na ni jambo la kusikitisha. Pia wanapokwenda kufanya hicho kipimo kwenye hiyo *dispensary* gharama yake ni kuanzia 290,000 kuendelea, je, mwananchi mwenye kipato cha chini hiyo 290,000 ataitoa wapi? Moja kwa moja inaonesha kwamba Serikali haina nia nzuri juu ya afya ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda katika Hospitali ya Wilaya ya Bunda. Hospitali hii ni hospitali inayohudumia wilaya tatu, lakini ile hospitali imeandikwa Hospitali ya Wilaya ya Bunda lakini yale madawa yanayopelekwa pale ni ya kituo cha afya. Hakuna madaktari bingwa kisa tu hakuna *mortuary*. Ndugu zangu tambueni zile wilaya tatu ni wilaya zenye

wananchi wengi na hakikisheni kwamba msipoiweka katika hadhi nzuri ile Hospitali ya Bunda mnahatarisha maisha ya watu wa Mwibara, Musoma Vijiji na Bunda yenyewe na uzuri Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, Mheshimiwa Bulaya ameshalisemea sana suala la Hospitali ya Wilaya ya Bunda. Kwa hiyo basi, ninachoomba, Serikali iseme kwamba ni lini itaipa hadhi Hospitali hiyo ya Wilaya ya Bunda ili wananchi wa Wilaya ya Bunda na wao wawe na hali nzuri kwa kuona kwamba wilaya yao ina hospitali ya wilaya, inaleta sifa pia kwa wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusiana na suala la maji Bunda; sasa hivi ni takribani miaka 10 Wilaya ya Bunda kila siku wanasema maji yataletwa matokeo yake mpaka sasa maji bado hayajaletwa. Kila siku mnasema chujio, hilo chujio litatengenezwa lini ili wananchi wa Bunda wapate maji salama. Tunaomba mradi wa maji Bunda ukamilike ili wananchi wale na hasa upande wa akinamama, akinamama wanateseka sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenda kuhangaika kutafuta maji na wakati maji yapo shida ni chujio. Kwa hiyo, tunachohitaji Wilaya ya Bunda inahitaji ipate maji salama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda upande wa elimu bure. Naomba tu niseme ukweli, mshaurini tu Mheshimiwa Mtukufu kwamba hili suala tayari sasa hivi limeshashindikana ili liwe wazi kwa wananchi na ikiwezekana pia aombe tu msamaha kwa wananchi kwamba hili suala limeshashindikana ili wananchi wenyewe waweze kuchangia kusomesha watoto wao. (*Makofî*)

## **TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOÀ NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOÀ NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasimama

kutoa Taarifa kwa sababu ya aina ya maneno yanayotumika. Naomba tu nimuarifu mzungumzaji kwamba Serikali inatenga shilingi bilioni 22.5 kila mwezi kwa ajili ya kulipia mitihani, kwa ajili ya kulipia uendeshaji wa shule, kwa ajili ya kulipia mambo madogomadogo yanayotumika pale katika shule kwa ajili ya uendeshaji.

Pia Serikali kupitia makubaliano iliyofanya na Chama cha Walimu Tanzania na mapendekezo yakawa tutoe posho ya madaraka, tunatoa shilingi 200,000 kwa kila mratibu wa elimu kata, mwalimu mkuu na wakuu wa shule, shilingi 200,000. Hata hivyo, kupitia uandikishaji ambao sasa hivi wazazi hawatoi gherama yoyote katika kuandikisha watoto, tumeweza kuandikisha watoto wengi mara mbili ya wale tuliokuwa tumewatarajia, matarajio ilikuwa tuandikisha 750,000 tumeandikisha 1,849,000... (*Makofi*)

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** ...idadi hii inatokana na utaratibu wa elimu...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Hebu kaa chini kwanza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** ...hakuna Taarifa juu ya Taarifa mzee...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Hapana, kaa chini, hebu kaa chini kwanza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo

nataka tu tuwe wakweli, dhana na kufikiri kwamba elimu bure basi wazazi wasifanye chochote hata watoto wao wasiwanunulie *uniform*, watoto wao watakula hukohuko shuleni, watapata kila kitu shuleni inakuzwa na wenzetu wasio na nia njema na jambo hili, lakini suala la elimu bila malipo limesaidia sana nchi hii na watoto wengi wamekwenda shule na wazazi wengi wamepata nafuu hiyo. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Hapana! Waheshimiwa...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Hapana, hebu kaeni chini, subirini. Hebu kaa chini...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anapotosha.

**MWENYEKITI:** Kaa chini, na wewe kaa chini. Niliyemsimamisha ndiye mwenye *instrument* ya elimu. Mheshimiwa Matiko kaa chini! Nimemsimamisha Waziri mwenye *instrument*, mnatakiwa mjenge hoja, Serikali inalipa zaidi ya mabilioni *every month* na pesa zinakwenda shuleni zinafika na kama una mchango wa ziada changia kwa maandishi na utajibowiwa na sekta inayohusika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Sokombi, endelea.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru lakini sitaipokea kwa sababu najua Waziri Mkuu atakuja kujibu hoja, tuseme tu ukweli elimu sio bure, Mheshimiwa Simbachawene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda upande wa hili suala lililopo Tanzania sasa hivi, ni hali ya kutisha hili suala la utekaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli...

**MWENYEKITI:** Vipi umeishiwa? (*Kicheko*)

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Siwezi kuishiwa na bado naendelea.

**MWENYEKITI:** Tuendeleel!

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utekaji kwa kweli ni suala ambalo linatisha juu ya maisha yetu na juu ya maisha ya Watanzania. Kila mtu anasimama hapa anaongelea juu ya utekaji, naomba wewe kama Mwenyekiti uliyekalia hiki kiti hapo mjiulize ni kwa nini kila mtu anasimama na kuongelea suala la utekaji? Halafu Waziri mwenye dhamana, Waziri Mkuu hajatamka kitu chochote mpaka dakika hii, kusema ukweli inasikitisha na ni jambo la aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba, Ben Saanane amepotea ni muda mrefu sasa umeaita, Serikali imekaa kimya. Msanii Roma alitekwa lakini cha ajabu yule mtu kapatikana kwenda kujieleza matokeo yake Waziri wa Michezo eti anamsindikiza, unategemea yule msanii ataongea kitu gani cha ukweli? Ina maana Serikali inajua ni kitu gani kilicho nyuma yake.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chegeni, Mheshimiwa Mayenga, Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami napenda kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu jinsi ambavyo ameweza kuiwasilisha nikiangalia inakidhi kwa kiwango kikubwa mahitaji ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rahisi sana kukosoa lakini naomba niwarejeshe Watanzania na Waheshimiwa

Wabunge wenzangu kwamba ukiangalia Serikali ya Awamu ya Tano, kwa muda mfupi imefanya mambo mengi na makubwa kwa Watanzania. Tukikumbuka kwamba Serikali ya Awamu ya tano imeingia ikirithi madeni ya awamu iliyopita kitu ambacho ukikiangalia na hata katika maelezo ya mpango wa Waziri wa fedha, sasa hivi tunalipia karibu trilioni moja, deni la Taifa kwa kila mwezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia kwamba Mheshimiwa Rais pamoja na ubinadamu wake hebu tumpe sifa kwa kile anachokifanya kwa ajili ya Watanzania na tumuunge mkono kama Watanzania na kama Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge hili. Nchi hii tunaiongoza sisi sote, sitegemei kwamba kwa vile uko upande mmoja wewe ni kusema mabaya siku zote. Hebu tuwajenge Watanzania wajue kwamba chombo hiki kinafanya kazi kama mhimili mmojawapo wa utawala hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa ku-*register* kidogo kwamba kwa kipindi ambacho tumeanza kipindi cha bajeti kuna dosari zimejitokeza lazima tuzikubali. Mhimili huu una heshima yake na heshima yake hii lazima ilindwe na Mhimili wenyewe. Vile vile kwa mujibu wa kanuni za Mabunge ya Jumuiya ya Madola, mimi kama Mwenyekiti wa CPA kwa tawi la Tanzania ningemba sana Mheshimiwa Spika na kiti chake walinde maslahi ya Bunge hili na mustakabali wa Bunge hili kwa sababu haiwezekani tukawa kila siku tunatupa lawama kwa Serikali, tujilize sisi Kama mhimili tumefanya nini? Haiwezekani kila siku tunasema Serikali, Serikali, Serikali. Bajeti ya Bunge inawezesha Bunge hili lifanye kazi zake kuisimamia Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za Mbunge ni tatu; ya kwanza ni kutunga Sheria, ya pili ni kuwawakilisha watu waliomchagua kwenye chombo hiki na tatu ni kusimamia na kuishauri Serikali, haya ndiyo majukumu ya msingi ya Mbunge ndani ya Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumejitokeza maneno yanazungumza hayatii afya kwa Bunge hili. Tunahitaji kauli

za Serikali zitoke zikieleza bayana kama kuna tatizo liainishwe. Sitarajii kwamba yamezungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mbili lakini kuna Mawaziri wenye dhamana wamekaa kimya. Huku ni kutokuwajibika ndani ya chombo hiki lazima watoe kauli wawaondolee hofu Watanzania ili wajue kwamba Serikali yao wanachofanya ndicho hicho Watanzania wanachokitaka lakini tunapokaa kimya tunaleta *a lot of speculations*, watu wanakuwa hawaelewi sisi kama Wabunge tunafanya nini. Wananchi wanalamika, Wabunge wanalamika, Serikali inalamika tunakwenda wapi? Kwa hiyo ningeomba sana hii sintofahamu hii, njiombe Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali ndani ya Bunge ni vyema ukatusaidia kuondoa sintofahamu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nikiangalla kwamba Serikali ya Awamu ya Tano imefanya mambo mazuri sana na lazima tujenge msingi wa uchumi ili tuweze kuendelea. Huku nyuma ukiangalia watu wanalamika uchumi umebadilika, m dororo wa uchumi siyo kwa Tanzania peke yake, dunia nzima sasa iko kwenye m dororo wa kiuchumi. Tusipofikiria nje ya *box nadhani* sisi Watanzania ni kama kisiwa ndani ya dunia haiwezekani lakini yanayofanyika tuyapongeze na tuyape jithada kubwa zaidi ya kuya-*support*, angalia miundombinu inayofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi, ndani ya muda mfupi tumeona uanzishwaji wa ujenzi wa reli ya kati kwa *standard gauge*, historia, miradi ya maji inayoendelea ni historia. Upande wa elimu nawasikitikia ambao wanabeza kwamba eti hakuna elimu bure, jamani nawasikitikia sana, labda hawajui wanachosema. Hajatokea katika historia ya nchi hii kwamba kila mwezi zaidi ya bilioni 18.7 zinatengwa kwa ajili ya elimu bure kwa mtoto wa Kitanzania. Haya tunapaswa kuyapongeza na Mheshimiwa Rais ukiangalia anachokifanya na naomba Watanzania tujue kwamba dhamira yake ni nyeupe, dhamira yake ni kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania, tumpeni *support* hii tusim-*discourage*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona kiongozi, mimi ni mgeni ndani ya Bunge lakini ni mwenyeji kidogo. Kazi inayofanya sasa hivi ni kazi nzuri sana lakini kuna vitu vya kushauriana. Mfano; katika suala zima la kiuchumi, kweli fedha ndani ya uchumi imepungua, ni suala la Waziri wa Fedha. Hii ni issue ya *Micro-economics*, mambo ya *Monetary Policy* na mambo ya *Fiscal Policy* atusaidie namna gani ya kurudisha fedha katika mzunguko na leo nimesikia kwamba Benki Kuu wameamua kushusha riba ile ya kuwekeza unajua kuna *Central Mineral Reserves* ambayo ni asilimia 10 ya Mabenki kuwekeza na Benki Kuu wameshusha mpaka asilimia nane. Hii italeta msukumo wa fedha ndani ya mzunguko wa uchumi, nakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuchukua *Monetary Policy* ya namna hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukumbuke kwamba jamani tunasafiri kwenye ngalawa moja. Sisi Wabunge bila kujali vyama vyetu nchi hii ni ya kwetu sote, uchumi huu ni wa kwetu wote tufanye kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia, naipongeza Serikali. Huko Busega mimi nasema kwamba nina mradi wa maji mkubwa umeshaanza kutekelezwa, sasa niseme nini zaidi ya hili jamani. Umeme wa *REA* keshokutwa tunaenda kuzindua, mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa nini niikosoe kwa kitu ambacho naona kuna faida kwa Watanzania? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi leo hii watoto wameongezeka katika kusajiliwa darasa la kwanza ni historia katika nchi hii. Hivi wewe unayelalamika kwamba Serikali hajifanya kitu unataka ikufanyie nini? Ikuletee Kitanda nyumbani kwako?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mayenga, wajiandae Mheshimiwa Ally Keissy na Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu. Nianze kwa kutoa shukrani zangu nydingi sana kwa Waheshimiwa Wabunge wote walioko katika Bunge hili kwa *support* kubwa walionipa na hatimaye sasa nimekuwa Mrs. Jamal, ahsanteni sana. Haya makofi naomba yaendelee mpaka mwisho najua kuna sehemu yatagoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe pongezi za dhati sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu wake Mheshimiwa Mavunde, wanafanya kazi nzuri sana na kazi kubwa sana. Leo nimesimama hapa, kwanza kwa kweli nina hasira kwa sababu kuna baadhi ya vitu ambavyo havijanifurahisha hata kidogo na kuna baadhi ya vitu ambavyo nikiviangalia unamwangalia mtu halafu unasema; hivi huyu anategemea nini? Unakosa majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa nafasi ya kipekee nimpe pongezi zangu za dhati sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya ye ye pamoja na Baraza lake la Mawaziri, wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi ambayo asilimia 32 ya mapato ya ndani yanakwenda kulipa madeni, katika nchi ambayo malimbikizo ya madeni yapo asilimia sita, katika nchi ambayo Mheshimiwa Rais anapozunguka au Waziri Mkuu au Mawaziri wanapozunguka Rais anaanza kuombwa kuanzia vidonge kwenye hospitali mpaka kwenye ndege watu wanalamika, Rais huyu kwa kazi hizi anazozifanya kwa kipindi hiki kifupi alichofanya kazi, anastahili pongezi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukakaa hapa kukaanza kuongea kirahisi rahisi kwamba Rais huyu amefanya hivi, Rais huyu hafai, Rais huyu sijui amefanya hivi ni rahisi sana kuongea namna hiyo, lakini Wabunge baadhi wamezungumza; hivi sisi Waheshimiwa Wabunge maana

nianze hata na mimi mwenyewe kwa sababu nipo humu ndani; katika kipindi hiki cha 2016 mpaka sasa hivi mmefanya nini kwenye Majimbo yenu? Hivi kila mtu akisema acae hapa aanze kuulizwa orodhesha ulichokifanya atasema amefanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema makofi yaendelee najua yatagoma; mimi nimekaa hapa Bungeni kwa kipindi cha miaka 12 kuanzia mwaka 2005 mpaka leo hii niliingia hapa Bungeni nikiwa mdogo sana. Naomba kutoa tahadhari kubwa sana kwa Wabunge ambao ni wapya na hasa Waheshimiwa Wabunge ambao ni vijana. Wako watu ambao ni *Genuine* kabisa kutoka pande zote mbili; kutoka upinzani na pia na huku. Kuna watu ambao wakiongea unajua kabisa huyu anaongea ni kwa kutoka kwenye dhamira yake lakini kwa *experience* yangu kuna watu nimeshuhudia tangu nimeingia hapa Bungeni miaka 12 hii kuna watu wanununuliwa na ni Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wana *interest* za nyuma, mambo yao yameharibika, wanakuja hapa wanataka kutuvuruga. Kuna mtu anakuja hapa anasimama kwa sababu mume wake alikuwa fisadi ameondolewa kwenye madaraka anasimama hapa anataka kutuvuruga. Kuna mtu anakuja anasimama hapa kwa sababu alikuwa anapewa pesa na mafisadi, mambo yamekuwa magumu anakuja hapa anataka kutuvuruga, kila saa Serikali mbaya, Rais mbaya, sijui vitu gani vibaya; tunaomba samahanini sana hayo maneno yenu mnyamaze mkaongee huko barabarani. Hapa tunataka tukae tuongee masuala ya maana, masuala ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeishi Rwanda kwa kipindi cha miaka kadhaa siwezi kusema ni miaka mingapi na kule walikuwa wanajua mimi ni Mnyarwanda. Nimeishi uswahilini ya Rwanda na nimeishi Masaki ya Rwanda; watu ambao ni viongozi wanakuwa wazalendo, kuna mambo ambayo ni ya msingi, mtu anakaa nazungumza kwa ajili ya nchi yao. Watu wanakaa wana-*discuss issues* ambazo ni za maana leo hii

tumekuwa viongozi ni mambo ya *Twitter*, sijui *Whatsapp*, meseji za kipumbavu pumbavu ni aibu kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa tutumie muda ambao huu tunao kukaa, kufanya mambo ambayo ni ya maana. Kwa nini hatukai tukashauriana kwamba jamani hebu tufundishane ujasiriamali tunafanyaje, hebu jamani twende tukamfuate Mheshimiwa Waziri wa Fedha, jamani Mheshimiwa hebu tusaidie, tunataka tujunge Wabunge 20 tufungue kiwanda, Mheshimiwa Waziri wa viwanda hebu tusaidie Wabunge 50 tunataka tukae tuweke mitaji yetu, tunataka tufanye biashara ya maana, matokeo yake watu mnakaa mnaanza kuchanganyikiwa, mnakuwa hamna hela mkitoka hapa maisha magumu, mmekaa wengine hapa mnapiga makelele, mnapata hizo nguvu kwa sababu mpo ndani ya vyama vyenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatakiwa watu muweze kukaa kila mtu amekuja hapa kwa nguvu yake na kila mtu amekuja hapa kwa moyo wake na anajua yeye mwenyewe nini kilichomleta. Sasa msikae hapa mnaanza ku-*insight other Members of Parliament to turn against the Government* hii ni adabu mbaya, mbaya, mbaya kupita kiasi. Kama mna mambo yenu huko pemberi nendeni mkayamalize, kama mna jambo lenu huko pemberi nendeni mkakae mkaongee huko, lakini siyo mnakuja hapa eti Bunge zima likae liongee mambo ya ajabu ajabu...

**MHE. SAID A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti..

**MHE. SAID A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MHE. SAID A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Naomba kuzungumza haya yafuatayo.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Taarifa

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** ....naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu upo hapa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mayenga hebu subiri.

**MHE. SAID A. KUBNEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa. Nimesimama kwa kanuni ya 64 ambayo inamta ka Mbunge asizungumze lugha ya kuudhi ndani ya Bunge, asizungumze lugha ya matusi ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti Mbunge anayezungumza sasa ametumia lugha ya maudhi ndani ya Bunge, amesema kuna watu ndani ya Bunge hili wamenunuliwa na kwamba waume zao au wake zao walikuwa ni mafisadi na wapumbavu na haya maneno siyo maneno ya Bunge, ni maneno ya kuudhi na Mbunge hawesi kuyathibitisha. Kwa hiyo, tunaomba kwa mwongozo wako ayafute au athibitishe kwamba kuna Wabunge humu ndani wamenunuliwa na aseme wamenunuliwa na nani na wamelipwa kiasi gani na lini. Hao mafisadi anaowataja ni akina nani, wako wapi na leo wako wapi na walimnunua nani. Ahsante (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, nitaagizia *Hansard* baadaye nihakikishe hayo maneno endelea Mheshimiwa.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokisema nilisema kwamba, katika kipindi ambacho nimekaa hapa Bungeni nimeshuhudia Wabunge wa aina hiyo wapo.

*(Hapa kuna Mheshimiwa alikuwa akiongea na mzungumzaji bila kufuata utaratibu)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Usitake kunipigia makelele na wewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afikishe salamu zetu kwa Mheshimiwa Rais aende akamwambie kwamba tuko nyuma yake, tunajua kazi kubwa ambazo anazifanya, tunajua Serikali hii kazi kubwa ambayo inaifanya na tuko nyuma yake kwa njia yoyote ile. Hatuwezi kunyaamazishwa lakini ninachoweza kuwaambia, hawa ambaao wanaweza kupambana naye, yupo mpaka 2025 ambaao wanadhani kwamba 2020 ni mwisho, *they are very wrong* na wanajidanganya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwaambia hata baadhi ya Wabunge ambaao tuko huku kwenye Chama chetu, kila siku nasema na kuna mtu mmoja nimeshawahi kumwambia; *You cannot win the fight with your Boss, you are messing up with the very wrong person* katika Awamu hii ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo hapa Bungeni, kipindi cha uchaguzi uliopita, wote tulikuwepo hapa labda hawa wengine wageni ambaao hawakuwepo lakini walikuwa wanafuatilia. Baadhi ya Wabunge tulikuwa tunaona tabia za ajabu ajabu walizozifanya ukiwa humu ndani, watu na heshima zao. Mimi nimeingia hapa kwa mara ya kwanza ulikuwa unamwona Mheshimiwa Mbunge unadhani kwa sababu ya umri wake ni mtu mzima, 'shikamoo Mheshimiwa' baadaye unakuja kukaa baada ya mwaka mmoja, baada ya miaka miwili, unasema kumbe hata 'mambo' hastahili kwa sababu ya jinsi vitu anavyovifanya vyatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua na wala siyo siri, tulikuwa tumekaa hapa, watu wakati wa uchaguzi, makundi yaliyokuwepo, sasa mimi nasema hivi; kama yale makundi yalikuwepo, kama ni masuala ya *interest* nyingine ambazo tunazo tuachane na hizo biashara sasa hivi tukae

tujenge nchi yetu. Tukae tufanye kazi, tukae tuanze kuangalia maendeleo ya nchi yetu yanakwendaje, wengine hapa kwanza hata muda wenyewe wa kuuliza maswali hatuna kwa sababu unawaza biashara tu sasa unamshangaa mtu mwingine kila saa amekaa 'Serikali hii sijui imefanya hizi' mimi nasemaga hivi hawa watu wanatoa wapi muda? Mwisho mtakosa Ubunge mrudi nyumbani kule maisha yaanze kuwa magumu, shauri zenu. Ndiyo ukweli wenyewe si nyie mnajjua? Niliwaambieni haya makofi yatafika mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata siku moja Simba Wazungu wana msemo kwamba; "*The lion does not turn around when a small Dog barks*" Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wala msihangaike na hawa watu ambao wanapiga makelele ya ajabu ajabu, maneno ya ajabu ajabu, wanasema vitu vya ajabu ajabu, ninyi kaeni, fanyeni kazi mwendelee kuwepo kwenye mstari na tuko pamoja, tunaowaunga mkono ndani ya hili Bunge ni wengi zaidi kuliko hawa wachache ambao wanapiga makelele. Tuwaache waendelee kupiga makelele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme; watakuja siku moja kula matapishi yao, wapo watu ambao tumewashuhudia leo mtu anasema hivi kesho anakuja unamshangaa huyo huyo anasimama Serikali hii nzuri sana. Unashangaa haya maneno ametolea wapi, watakuja kurudi kula matapishi yao lakini wakati huo tutakuwa tayari tumeshawajua.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nina hasira sana. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ally Keissy. Jiandae Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nichangie kidogo kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa muda mfupi aliokuwa Waziri Mkuu alikuja Namanyere akafanya ziara katika Jimbo langu la Wilaya ya

Nkasi akatembelea mpaka vyanzo vya maji ambavyo nilikuwa napiga kelele hapa kila mwaka habari ya shida ya maji Namanyere. Sasa mwaka huu tatizo la maji Namanyere litakuwa historia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile namshukuru Waziri wa Maji, alifika Namanyere mpaka kwenye vyanzo vya maji na akaahidi kusaidia mitambo ya kusukumia maji. Namshukuru vile vile Waziri wa Mambo ya Ndani alifika Namanyere, pia Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Makamba alitembelea Namanyere. Mawaziri wote walitembelea Namanyere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa namshukuru Mheshimiwa Magufuli. Mimi nilikuwa Bunge la Nne hapa ndugu zangu, nilikuwa msumari nazungumza ukweli kuhusu mafisadi, wezi wa mali ya umma, nilizungumza mpaka makaburi yao yafukuliwe wafungwe minyonyoro kwenye makaburi. Nilizungumza vile vile safari za Wabunge kwenda nje hazina manufaa, tunapishana *airport* kama wakimbizi. Nilizungumza hapa kabra Mheshimiwa Magufuli hajawa Rais, nilisema hizi safari hazifai! Hebu niambieni Mbunge hata mmoja aliyelewenda nje alete tija hapa kama sio ubadhirifu wa hela humu. Wengine walikuwa wanarudia *airport*, nimezungumza hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ushahidi wakamate hata *passport* zao waangalie, kama walipewa hela wakaenda, *passport* zitaonesha. Wengine wanapewa siku kumi wanakaa siku mbili wanarudi. Ndugu zangu tumsifu Magufuli amedhibiti nchi! Nilimwambia Rais Magufuli Kinyerezi kwenye kuzindua mtambo wa umeme nikasema; spidi yako bado sijaiona, bado spidi ni ndogo. Nchi hii bado mafisadi wengi, wanatuibia! Juzi juzi tu *tender* ya *EWURA* wanataka kutuingiza kutuobia bilioni sita kwa mwaka, shilingi bilioni kumi na tatu za Kitanzania kwa miaka mitatu mkataba huo tutaibiwa bilioni 40 wakati hatuna zahanati, hatuna madawati, hatuna kila kitu. Ndugu zangu bado watu hawaogopi Serikali, wapo! Hao wanataka wabanwe ikiwezekana kunyongwa! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Jimbo. Nimezungumza, Mfuko wa Jimbo kwanza usimame. Wapitie upya majimbo sio sahihi. Uchaguzi uliopita safari hii tumezidishiwa Kata kutoka Kusini kwenda Kaskazini, majimbo yameongezeka. Jimbo langu kata nzima imehamia kwangu lakini Napata mfuko wa jimbo ule ule, nitahudumiae kata ile nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwambia Mheshimiwa Simbachawene nikampelekea na taarifa kwamba kata nzima imekuja kwangu. Haiwezekani niendelee kupata mfuko wa jimbo ule ule. Simamisha kwanza nchi nzima, fanya mchakato upya. Wabunge wengi wamelalamika hapa. Halmashauri ya Mji wa Namanyere ina vigezo vyote cha ajabu wamekwenda kutoa halmashauri zingine hazina vigezo! Ushahidi tunao, upendeleo wa hali ya juu na ugawaji wa majimbo vile vile kwa upendeleo. Haiwezekani! Nchi ni moja hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna majimbo kama kwa ndugu yangu huyu hapa, Sikonge *square kilometers* 27,000, kwa Malocha, 15,000, kuna majimbo mengine *square metre* 1,000 humu, kuna mengine 200! Haiwezekani! Hatuwezi kwenda hivyo. Lazima twende sambamba, haiwezekani Mbunge yule yule anapata pesa ile ile, gari ile ile, mafuta yale yale, jimbo lake linakuwa kubwa kama Rwanda, kama Burundi, haiwezekani! Hii ni kuoneana. Lazima Namanyere sisi tupate halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mikoa imeanza juzi juzi halmashauri tano, sita. Cheki Mkao wa Rukwa, Mkao mkubwa kabisa halmashauri zile zile nne, haiwezekani! Ni maonezi hatuwezi kwenda. Ahadi ya Rais alituahidi alipokuja, barabara ya lami kilometra tatu tunaitaka Namanyere, alituahidi kilometra tatu za lami, tunazitaka!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali Namanyere. Tuna miaka 40 Wilaya ya Namanyere haina hospitali ya wilaya, miaka 40! Watu wanasema miaka 20, miaka mitano mpewe

hospitali. Kuna wilaya zimeanzishwa juzi zina hospitali ya wilaya, sisi miaka 40 hamna hospitali ya wilaya. Haiwezekani, haya maonezi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *DC* wetu wa Nkasi. Tangu ameanza hana gari, hana usafiri. Anahudumia wilaya *square kilometers* 13,500 hana gari! Leo kasimamia shule 105 kujenga madarasa matatu shule ya msingi katika kila shule kuhamasisha wananchi na anajenga, anasimamiaje? Hana gari *DC*, anaombaomba magari. Polisi Namanyere hawana hata matairii. Ndugu zangu tuoneane huruma, kuna wilaya zingine zinapewa magari matatu, manne hata hadhi ya wilaya hazina, ziko humu humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Wabunge hata ukubwa wa Kata kama Kata yangu hakuna! Wanapewa kila kitu. Lazima tufanye mchakato upya. Ikiwezekana Rais Magufuli aangalie, kama majimbo mengine ayafute! Ayavunje majimbo na halmashauri zingine. Hatutaki mambo ya kuoneana. Kupanua halmashauri ambazo hazina hata uwezo, hazikusanyi chochote! Mzigo kwa Serikali. Tuambizane ukweli hata kama unauma. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa ziwa Tanganyika; Awamu ya Nne tumeahidiwa meli mbili katika ziwa Tanganyika lakini nakuja kusoma tena ni utengenezaji wa Liemba ina miaka 113. Ndugu zangu, tunataka usafiri wa ziwa Tanganyika, meli mpya! Liemba itengenezwe maana bado inafaa, bado ni nzuri ikarabatiwe, lakini meli mpya tunaitaka katika Ziwa Tanganyika, wananchi wanapata matatizo sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pembejeo. Hao wanaogawa ruzuku ya pembejeo, ndugu zangu haiwezekani mtu anasema ana deni milioni 360 wakati tukipiga hesabu ni mbolea bilioni 1.8 alipeleka katika jimbo langu. Wanachakachua, lazima wafuatiliwe. Nimemwambia hata Waziri wa Kilimo, Waziri Mkuu nimemwambia, katika Jimbo langu la Nkasi kuna kata kadhaa, hakuna kuwapa pesa wamechakachuka, ni wezi wa hali ya juu. Ndiyo hawa Rais

Magufuli anawatafuta awafunge mara moja hao. Hawa hawafai katika nchi yetu, haiwezekani anakuja mtu na *briefcase* anapewa kuleta mbolea, analeta gari moja la mbolea anataka milioni 360, huu ni wizi wa hali ya juu. Hawa ni watu wabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya mbolea ndugu zangu bora iuzwe bei chini, mambo ya pembejeo hakuna tena ruzuku waache ruzuku, kila mtu anunue kama vile ananunua vocha ya simu, mambo yaishe! Wametajirika watu kwa hela za vocha hizi, nchi hii ni wezi wa hali ya juu. Waaminifu ni wachache! Kwa hiyo, *agenda* zangu ni hizi hizi; nataka Namanyere kuwa Halmashauri ya Mji. Mheshimiwa Waziri Mkuu uliona Namanyere ilivyokuwa, kuna halmashauri zingine ukitembelea hakuna lolote, mnawapa halmashauri, ni uonezi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri Ziwa Tanganyika; namwomba Rais Mheshimiwa Magufuli aendeleze, azidishe mara mbili. Asioneer huruma mtu yejote anayeiba hela za walipa kodi. Wananchi wetu, ndugu zangu majimboni kwangu kuna matatizo. Nazungumza habari ya usafiri kutoka Kilado kwenda Kazovu miaka 50, tangu uhuru hatujaona gari! Nashukuru Ofisi ya Rais imenipatia pesa, mwaka huu wananchi wa Kazovu wataona gari! Niseme nini sasa? Nikose kumshukuru? Nilikuwa napiga kelele hapa wananchi hawajona gari, hawajaona bajaji lakini mwaka huu wananchi wataona gari. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba na Waziri wa Ujenzi aniongezee tena hela nipasue ile barabara Kazovu kwenda Korongwe, wananchi wafurahie uhuru katika nchi yao. Rais asikate tamaa aendelee kupambana na watu kama hawa. Hakuna kuoneana aibu!

Haiwezekani ndugu zangu katika nchi zingine, mtu anaimba wimbo wa matusi kumtukana Rais mwanzo mwisho anaachiwa! Nchi gani hii? Utawala gani huu? Wewe mtu unamtukana Rais unaachiwa? Aende Rwanda kule akaangalie au nchi za Kiarabu, watakunyonga! Wewe

unamtukana Rais wa nchi, wewe umekuwa nani? Uhuru gani? Demokrasia gani hii? Unaimba nyimbo, wewe nyimbo na mtu wa *studio* anarekodi nyimbo, ama kweli sio utawala huu! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wangenachia mimi dakika mbili niwaoneshe hawa! Haiwezekani! Kiongozi wa nchi anatukanwa na nyimbo, ukiisikia hiyo nyimbo ya Roma sijui Mkatoliki, ndugu zangu nyimbo ya aibu. Haiwezekani mtu unasiliza nyimbo kama ile. Halafu unamshabikia mtu! Haiwezekani! Kusema kweli ni makosa, ni kukosa adabu. Rais wa nchi hatukanwi popote pale. Haiwezekani! Nendeni nchi zingine, nenda Rwanda hapo, nenda Burundi, nenda *DRC* ukaangalie, watakushughulikia! Nyie mnacheka cheka hapa, haiwezekani kumchezea Rais namna hii. Huu ni utovu wa nidhamu. Huyu Rais anaheshimika, dunia nzima wanamsifu Magufuli. Leo nyle wenye ndiyo mnawona hafai kwenu, kote ukienda wanamsifu, Uarabuni wanamsifu, Ulaya wanamsifu, sijui ukienda...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ahsante kwa mchango wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii muhimu ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri Jenista na kaka yangu Mavunde kwa kazi nzuri wanayoifanya. Tunawashukuru kwa kutupa ushirikiano mzuri katika kuwashudumia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Magufuli, Mheshimiwa Makamu wa Rais mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi na dira ya miaka mitano ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mawili katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kipengele cha hali ya uchumi nchini ukurasa wa 13 mpaka 40 kuna mambo ambayo hotuba imeyazungumzia ningependa kuchangia mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala; kwenye mjadala sasa hivi kuna mjadala kuhusu *size* ya Bajeti ya Serikali. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017, Serikali ilitenga trilioni 29.5 na katika mwaka ambao unakuja wa Mwaka wa Fedha 2017/2018, bajeti hii itapanda kutoka 29.5 kwenda kwenye trilioni 31.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mijadala kuhusu *size* ya Bajeti ya Serikali naona Serikali kwa sababu dhamira yake na nia yake ni kutatua changamoto za Watanzania kwa kasi, si mbaya kuwa na malengo marefu na kwa vile Serikali ya Awamu ya Tano tunajua ina dhamira ya kuhakikisha inatumia vizuri fedha za umma, nadhani Waheshimiwa Wabunge tujikite kwenye kusimamia kile ambacho Serikali inakikusanya kama kinaenda kwenye kutekeleza miradi ya maendeleo. Sio mbaya kuwa na malengo *if you aim higher* na ukaweka jitihada ya ufanya kazi ili kwenda kwenye hayo malengo mapana ni jambo la kupongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ya Awamu ya Tano inaingia madarakani *TRA* ilikuwa inakusanya takriban bilioni 800, lakini Serikali ingependa ikae kwenye kusifiwa kwamba inatimiza malengo ya kila mwezi, basi tungejwekea *target* za bilioni 800, tunaendelea kupongezana kila mwezi lakini Serikali ikajipa *challenge* ikasema tujivute twende

kwenye trilioni 1.2. Kwa hiyo, unaona kwamba ni hatua nzuri, unakuwa na malengo marefu, lakini unajitahidi kwenda kwenye hayo malengo marefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo naiona kwenye uandaaji wa bajeti ni kwamba asilimia kubwa ya Watanzania, kikundi cha wananchi ambao wako vijiji, asilimia kubwa ya wale Watanzania ni kwamba uchumi unakua lakini hauwagusi wale asilimia kubwa. Kwa mfano, katika mpango wa maendeleo wa 2017/2018 na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukiangalia kwa upande wa kilimo kwanza kwenye ukuaji wa Sekta ya Kilimo 1.7% ni kidogo mno. Hatuwezi kuona *social economic transformation* kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Sekta hizi ambazo zinaajiri Watanzania walio wengi kama tutaendelea kupata ukuaji wa 1.7%. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuiomba Serikali katika Bajeti za Kisekta ambazo zinakuja, tuone bajeti ya kutosha imetengwa kwa ajili ya pembejeo, tuone kuna mpango wa kupata maafisa ugani wa kutosha ili vijiji vyetu vipate maafisa ugani, tuone bajeti ya kutosha kwenye kilimo cha umwagiliaji. Mwaka wa Bajeti wa 2017 ilitengwa hela kidogo sana kwenye kilimo cha umwagiliaji. Katika Bunge hili baada ya ukame ambao ultupata kule Karagwe, niliomba Serikali ije kwenye kata kumi ambazo zina vyanzo vya maji tutathmini kuona kama tunaweza kufanya kilimo cha umwagiliaji, lakini mpaka hivi sasa sijapata timu ya wataalam kufanya hii tathmini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ili tuweze kwenda kwenye uchumi wa viwanda na kwenda kwenye *middle income country status* lazima tufike mahali tuone jitihada za kibajeti zinazolenga kutoa bajeti ya kutosha kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili Watanzania wengi hawa ambao wanajishughulisha kwenye hii sekta tuweze kuwasaidia kujikwamua kutoka kwenye umaskini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mazao ya biashara, kodi kero 27 kwenye zao la kahawa tumeondoa kodi moja

tu ya ada ya leseni ya kusindika kahawa ya dola 250 tu. Tuko kwenye rekodi, kwenye llani tumeahidi kwamba tutaondoa hizi kodi kero kwenye zao la kahawa. Mheshimiwa Rais alikuja Kagera akaahidi kwamba kwenye bajeti hii ya 2017/2018 tutaziondoa hizi kodi kero. Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru ulikuja Karagwe tukaahidi lakini sijaona jitihada ya Serikali kuondoa hizi kero kwa sababu kwenye hotuba ya Waziri Mkuu hazitatajwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye kusaidia yale makundi ya wananchi ambao wako vijiji ni pia kuna haja ya kuangalia wajasiriamali wadogo na wa kati na kuweka mazingira wezeshi ili kuwasaidia kukua. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inatambua kwamba 56% ya wananchi ni nguvu kazi ya vijana, lakini kwa sababu tumekuwa na malengo ya kukusanya mapato ya kila mwezi kwa mfano, kumekuwa na *aggressive behavior* katika kukusanya mapato kiasi kwamba haya makundi ambayo tunategemea kuwasaidia kuwakwamua kutoka kwenye umaskini tunajikuta zile *aggressive behavior* za kukusanya kodi kwa mfano upande wa bodaboda, ukija Karagwe, bodaboda awe kwenye gulio, msiba au shambani, pikipiki zinawindwa na askari wa usalama barabarani kwa sababu wana *target* ya mapato kiasi fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo matokeo yake unakuta badala ya kumsaidia yule kijana ambaye tumeshindwa kumpatia ajira kwa sababu tatizo la ajira ni la nchi nzima na si Tanzania tu ni Afrika na dunia nzima, wale vijana ambao wanajiajiri tunatakiwa kuwawekea mazingira wezeshi ya kukua. Kama ame�iajiri kama bodaboda basi tumsaidie ili aweze kukua. Kwa hiyo, matokeo yake, kwa sababu ya *target* za mapato unakuta tunawaathiri yale makundi maalum ambayo tulitakiwa kuwasaidia kuwawekea mazingira wezeshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa, niende kwenye changamoto zlizoko kwenye Jimbo la

Karagwe na nimezileta kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ili nimwombe aweze kunisaidia yapate *attention* inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mradi wa maji wa Rwakajunju. Huu mradi ni ahadi ya muda mrefu, Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni tuliwaahidi wana Karagwe katika hii Serikali ya Awamu ya Tano tutatekeleza mradi huu. Serikali ikatenga dola milioni 30 kwenye Mwaka wa Fedha 2016/2017, lakini nashangaa kwenye bajeti ya mwaka huu 2017/2018, fedha hizi sizioni sasa sijui zimeenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakumbuka ulivyokuja karagwe tuliwaahidi wana Karagwe kwa vile zilikuwa zimeshatengwa kwenye bajeti ya mwaka uliopita, tukawaahidi pale tulikofanya Mkutano pale Kihanga tena ukamwomba Mkurugenzi wa Halmashauri aje kwenye jukwaa awaambie kwamba wananchi wa Kata ile ya Kihanga na wenyewe watapata huduma ile ya maji kutoka kwenye mradi wa Rwakajunju. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mradi huu usipotekelezwa kwa kweli kuna hali ya hatari huko mbeleni. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu anisaidie katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la elimu. Naipongeza Serikali katika elimu ya bila malipo, tunakwenda vizuri na Serikali inaendelea kurekebisha pale ambapo tunakwama lakini ili tuweze kwenda vizuri, naomba Bajeti ya 2017/2018, tutengete fedha za kutosha kwa ajili ya kuajiri walimu. Wilaya ya Karagwe peke yake tuna *deficit* ya walimu 840 wa shule za msingi, tuna *deficit* ya walimu wa sayansi 96.

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Nakuongeza dakika moja.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la afya. Katika malengo ya

Serikali ya kuwa na kituo cha afya kila kata nadhani ni malengo mazuri lakini hatuwezi kuyatimiza kwa muda mfupi. Nipende kuishauri Serikali angalau tulenge kuwa na kituo cha afya kwa kila tarafa ili katika kipindi cha miaka mitano tuweze kuonesha kwamba tuna malengo ya muda mrefu lakini katika kipindi cha miaka mitano tumeweza kuwa na kituo cha afya cha kila tarafa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na migogoro ya ardhi. Pale Kihanga tulipofanya mkuutano, zile hekta 2000 ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza Serikali irudishe kwa wananchi mpaka hivi sasa bado. Walienda pale wakasema tunawapa hekta 2000 lakini zimelenga sehemu ambapo wananchi tayari wanakaa, hazijatolewa kutoka kwenye *ranch* ya Kitengule na wenye ma-block, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu asiingilie katika hili suala ili tuweze kurudisha hekta 2000 kwa wananchi kama tulivyowaahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji wa vyama vyote imekwisha na wote wamechangia. Wengine wataendelea kesho naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.40 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 12 Aprili, 2017 Saa Tatu Asubuhi*)